ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.

8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando

17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake

26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
41.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
42.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
43.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
46.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
50.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
52.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
54.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
56.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
57. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
61.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
62.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
66.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
67.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
68.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
71.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Wanakwerekwe
74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 06 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 205

Uchomaji Moto wa Vibanda vya Wafanyabiashara Wadogo Wadogo

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Hivi karibuni wafanyabiashara wadogo wadogo wa Pwani Mchangani walichomewa moto vibanda vyao na watu wasiojuilikana kwa madai ya kwamba wafanyabiashara hao walivamia eneo hilo kinyume na utaratibu. Hatua hiyo, imesababisha hasara kubwa ikiwa ni pamoja na kukamatwa kwa washukiwa.

(a) Nini hasa chanzo cha tukio hilo?

(b) Je, wafanyabiashara hao walimiliki eneo hilo kisheria?

(c) Hadi sasa ni watu wangapi waliokamatwa na kupelekwa Mahakamani?

(d) Ni gharama kiasi gani ambayo wafanyabiashara hao wamepata kutokana na tukio hilo?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 205 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kusema kwamba kweli tukio lile la wafanyabiashara wadogo wadogo wa Pwani Mchangani walichomewa moto vibanda vyao na watu wasiojulikana. Kwa kweli kitendo kile kimeonekana kwamba si cha kibinadamu na kimelaaniwa vikali kabisa na wanajamii pamoja na viongozi wetu Wakuu walitembelea pale kwa ajili ya kuwapa faraja wale waliopatwa na mkasa ule.

Mhe. Naibu Spika, tukio hilo limeripotiwa Mahakamani na watu 7 wamekamatwa kwa kushtumiwa kwamba ndio chanzo cha tukio lile na hasara iliyokisiwa inafikia shilingi 63,154,000/=. Kwa kwa suala hili liko Mahakamani, basi ninamshauri Mhe. Mjumbe tusubiri mpaka hatimaya ya Mahakama iweze kutuamulia pamoja na kujua kwamba walimiliki ardhi au vyenginevyo watu wale na mustakbali wa mzima wa Mahakama.

Nam. 198

Msaada wa Wafadhili katika Bajeti ya Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Zipo taarifa kwa nchi Wafadhili wakiwemo *World Bank* zimeamua kuisaidia
Bajeti ya Tanzania ya mwaka huu wa 2011/2012 kwa kiwango kikubwa cha
Fedha, kuliko viwango vilivyotolewa kwa bajeti zilizopita na kwamba zaidi ya *Dola* m*illioni* mia nane na arubaini (*US$ 840m*) zitatolewa kufadhili miradi ya wananchi yakiwemo yale maeneo ya Muungano.

(a) Msaada huo unahusu vipi Zanzibar kama sehemu ya nchi mbili za Muungano tutapata kiasi gani kati ya hizo?

(b) Fursa za kujitangaza na kuomba misaada hupatikana pamoja na viongozi kushiriki katika ziara na mikutano ya Kimataifa kama vile mikutano ya uchumi na kadhalika. Hivi karibuni ulifanyika Mkutano wa Uchumi wa Dunia (*World Economic Forum*), ambao ulifanyika Afrika ya Kusini. Je, nchi ya Zanzibar iliwakilishwa na nani wakati Tanzania iliwakilishwa na Rais Kikwete.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi Nam. 198 lenye kifungu (a) na (b) naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Washirika wa Maendeleo kumi na mbili (12) wamekubali kuisaidia Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kupitia bajeti ya mwaka 2011/2012 kwa jumla ya Dola za Kimarekani 556 milioni na sio 849 milioni. Msaada huo ni sawa na shilingi bilioni 834/= kwa ajili ya kutekeleza MKUKUTA kwa Tanzania Bara na MKUZA kwa Zanzibar. Msaada huo wa fedha umeongezeka kwa shilingi bilioni 34 ukilinganisha na ule uliotolewa mwaka 2009/2010.

Mhe. Naibu Spika, fedha hizo zimegawika kama ifuatavyo:-

(i) Mikopo bilioni 199.78

(ii) Misaada bilioni 473.11 na

(iii) Misaada ya Kisekta bilioni 161.11

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Zanzibar tukiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tutafaidika na msaada huo kwa kupata asilimia 4.5 ya fedha yote ambayo haiendi kwenye sekta. Hivyo, Zanzibar itapata shilingi bilioni 30.28 kutoka katika mikopo na misaada isiyo ya kisekta.

(b) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kushiriki kwetu katika mikutano mbali mbali ya Kimataifa kunatoa fursa kwa Zanzibar kujitangaza na kutafuta misaada. Mkutano wa Uchumi wa Dunia kwa Afrika uliofanyika Mjini *Cape Town*, Afrika Kusini mwaka 2011 ulikuwa na lengo la kubadilishana uzoefu juu ya maendeleo ya kilimo Barani Afrika. Kwa bahati mbaya, Zanzibar katika mkutano huo hatukupata mwaliko, hivyo hatukuweza kushiriki.

Hata hivyo, Mhe. Jakya Mrisho Kikwete ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwepo kwake katika Mkutano huo ni kutuwakilisha Watanzania sote.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu ya ufafanuzi ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Kwa kuwa Mhe. Waziri alikiri kwamba fedha ambazo zimeahidiwa ni mikopo, misaada na misaada ya kisekta.

Vile vile zipo taarifa pamoja na shutma kwa wananchi kwamba Tanzania wanapokuwa nje wanatumia fursa ya Muungano kujiombea hii misaada ya kisekta hata zile sekta ambazo si za Muungano, kama vile kilimo.

Je, Zanzibar sisi tunafaidika vipi wakati msaada unakuja kwa kilimo Tanzania na wala si jambo la Muungano?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, kiutaratibu Serikali ya Muungano au watendaji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaweza kwa mujibu wa Katiba kwenda nje kuomba mambo mbali mbali ambayo si ya Muungano, kwa maana ya matumizi kwa upande wa Tanzania Bara. Halikadhalika watendaji kutoka SMZ wanao uwezo wa kwenda nje kuomba mambo ambayo si ya Kimuungano kwa matumizi ya Zanzibar.

Lakini tutakapokaa Tanzania au ndani Tanzania tukawaita Mabalozi au wafadhili ama washirika wa Maendeleo tukaomba misaada kwa ajili ya mambo si ya Kimuungano na ikapitishwa katika *GBS*, kiutaratibu fedha zile na sisi Zanzibar tunapaswa kuzipata. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa msingi huo nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe kuwa suala hili ofisi yangu imeliona na tutalifuatilia, ili tuweze kuona na sisi kiasi gani tunaweza kufaidika. Kwa kweli fedha zinazopitishwa kwenye *GBS* za kisekta na Zanzibar nayo ifaidike. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na ufafanuzi mzuri alioutoa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwa kuwa amekiri kwamba kulikuwa na kiasi cha shilingi bilioni 161 ambazo ziliingia kwenye misaada ya kisekta ambazo Zanzibar pamoja na kwamba si shughuli za Muungano, mara nyingi kutokana na kuambiwa haitambuliki Kimataifa imekuwa ikikosa fursa za kuomba moja kwa moja na badala yake Tanganyika ikitumia jina la Muungano imekuwa ikifaidika.

(a) Je, Mhe. Waziri analiambia Baraza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itachukua hatua ya kudai *share* yake ambazo ni takriban ni bilioni 7.25 ikiwa ni mgao wa asilimia 4.5.

Mhe. Naibu Spika, naliuliza hili kwa sababu fedha hizi zinatosha kabisa kujaza yale mapengo ambayo Wizara ya Afya katika bajeti yake ilituambia hapa. Kwa mfano, tungepata *ICU*, fedha za kununulia madawa pamoja na mambo mengine mbali mbali. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atachukua utaratibu gani kuzidai hizi bilioni 7.25/= ikiwa ni share yetu ya 4.5 katika hii misaada ya kisekta ya bilioni 161/=. *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa mwenyewe amekiri ni kwamba inavyopaswa iwe ni kuwa Zanzibar, kwa sababu kuna mambo ambayo si ya Muungano ambayo mara nyingi ndio yanayoingia kwenye misaada ya kisekta.

Je, serikali itachukua hatua lini ya kushirikiana na nchi wafadhili kuanzisha utaratibu na kuwa na *Consultative Group Meeting*, yaani ni Mkutano wa Mashauriano baina ya nchi Wahisani wa Maendeleo na Mashirika ya Kimataifa na Zanzibar.

Hivyo, Zanzibar kama Zanzibar kwa mambo ambayo si ya Muungano iweze kuwasilisha mahitaji yake na kuweza kukadiriwa kile ambacho tunachoweza kukipata, hivyo kufaidika moja kwa moja kwa misaada ya kisekta kama vile Tanganyika wanavyopata. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango Maendeleo:

(a) Mhe. Naibu Spika, ningefarajika sana kama ningelizidai fedha hizi. Lakini kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwanza nataka kuzifuatilia kama fedha hizi za kisekta zimekuwa *time* na *project*, basi nguvu za kufuatilia zitakuwa ni ndogo.

Lakini ikiwa zimo kwenye *basket* na zinaweza kwenye katika sekta yoyote ile, yaani hazikuwa *allocated* kwenye miradi, basi pale tunaweza kuzifuatilia na tuweze kuona wenzetu watufahamu na kama hili tayari wameshazi-*allocate* kwenye bajeti yao, basi katika miaka ijayo pia na Zanzibar waiangalie kwenye sekta mbali mbali.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimueleze Mhe. Mjumbe kwamba mimi nakubaliana naye moja kwa moja kwa Zanzibar kufanya *Consultative Meeting* na Wafadhili mbali mbali, ili kuweza kuwaeleza mahitaji yetu mbali mbali katika sekta tofauti.

Kwa hivyo, hivi sasa ofisi yangu tayari imeshaanza maandalizi na matarajio yetu mpaka hivi sasa kama mambo yatakwenda vizuri, basi tunategemea mnamo mwezi wa *September* kuwa na Mkutano huu wa Pamoja baina ya sisi na wafadhili. *(Makofi)*

Nam. 186

Wakulima Waliothirika na Ukame

Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny: Mhe. Viwe Khamis Abdalla) – Aliuliza:-

Hivi karibuni katika mwezi wa Januari na Machi 2011 Masheha wetu walipokea agizo kutoka Afisi za Wakuu wa Wilaya kuorodhesha majina ya wakulima, ambao mazao yao yameharibika ama kwa ukame au maradhi. Tangu kuorodheshwa kwa majina hayo hakuna hatua iliyochukuliwa hasa kwa wakulima wa muhogo na migomba.

(a) Je, serikali ilikuwa na nia gani juu ya zoezi hilo?

(b) Katika kufanikisha kilimo katika Shehia/Kijiji, kwa nini serikali inashindwa kukamilisha zoezi la kusambaza mabwana na mabibi shamba kila Kijiji au Shehia.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 186 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli wakulima wengi walipata taathira ya jua kali katika mazao na Wizara ya Kilimo na Maliasili inatoa pole kwa suala hilo na kuwataka wawe wastahamilivu. Hata hivyo, wizara yangu ilitaka waorodheshwe wakulima walioathirika katika zao la mpunga tu.

Hivyo, wizara imewasaidia wakulima hao katika mabonde yote. Tani 24 za mbegu ya mpunga zilitolewa bure kwa wakulima walioathirika na huduma ya uburugaji wa maeneo yao ilifanyika kwa baadhi ya wakulima bila ya malipo.

Mhe. Naibu Spika kuhusu mazao mengine kama muhogo na migomba , hata katika mashamba yetu ya Idara ya Utafiti pia yaliathirika kwa jua kali na hivyo, haikuwa rahisi kwa wizara kutoa msaada wa mbegu za mazao hayo.

Wizara ya Kilimo siku zote imekuwa na wataalamu wa *organ*, yaani mabwana na mabibi shamba katika ngazi ya sheha na vijiji. Wataalamu hao wamo ndani ya Muundo wa Wizara na wanatoa taaluma kwa wakulima. Changamoto iliyopo ni kuwa kazi za kilimo zimetanuka sana na muamko wa wakulima umekuwa mkubwa, kiasi ambacho wataalam waliopo hawajatoshele mahitaji.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu imo katika utaratibu wa kuajiri vijana wapya waliomaliza Mafunzo ya Kilimo katika Chuo cha Kizimbani, ili kukidhi mahitaji yaliyopo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, katika mazao mengine ambayo yameharibika kama alivyojata Mhe. Waziri si mihogo na migomba tu, bali katika Jimbo langu la Micheweni au wananchi wangu walilima mtama kwa wingi na kama tunavyojua kuwa eneo la Micheweni mvua zake ni za kuvizia, kama vile Mvua za Masika na bahati mbaya mvua nyengine zote huwa Micheweni hazifiki.

Katika kilimo kile cha mtama walicholima wakulima wa Micheweni, basi mtama ule kwa bahati mbaya umevamiwa na wadudu na wakulima wengi wa Micheweni mtama wao umeharibika na wala hawana tamaa ya kuvuna labda ni mkononi tu.

Je, kwa kuwa hilo Mhe. Waziri analijua na eneo la Micheweni kama tunavyojua ni sehemu moja ya ukame. Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia wizara yake imejipanga vipi kuwasaidia wananchi wa Micheweni ambao mtama wao umeharibika.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, mtama, mahindi, njugu na kadhalika sikutaja. Lakini kwa Agizo la Mhe. Rais mtama, mahindi na mbegu za njugu zilipelekwa Pemba ikiwemo Jimbo la Micheweni na hivi karibuni kwenye ziara ya Mhe. Rais wakulima wa jimbo lake baadhi ya eneo walitoa malalamiko na hapo hapo wizara ilifanya jitihada za kuwapelekea mbegu za mtama.

Kwa hivyo, naweza kukiri kwamba pengine si wakulima wote wa jimbo lake wameweza kufaidika na mbegu hii iliyotolewa na serikali na hilo linawezekana. Vile vile nakubaliana naye kwamba wakulima wengi wa jimbo lake waliathirika.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile msimu umeshapita, hivyo ninachoweza kumuahidi ni kuwa wizara itafanya jitihada ya kupima taathira iliyotokea kwenye jimbo hilo na kutuzama uwezekana wa kuweza kuwasaidia wakulima hao kama dhamira ya serikali ilivyo.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Ili Mabibi na Mabwana Shamba waweze kutekeleza shughuli zao ipasavyo katika kuwahudumia wakulima na kwa kuwa watendaji hao muhimu hupangiwa shehia au sehemu zaidi ya moja.

Je, wizara ina mpango gani wa kuwapatia vipando angalau baskeli, ili kuweza kuwarahisishia shughuli zao muhimu.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, ni kweli hivi sasa Mabibi na Mabwana Shamba wengine wamepangiwa zaidi ya Shehia moja na serikali inayo dhamira ya kurekebisha hali hiyo.

Vile vile kuhusu suala la vipando ni kweli wizara inao upungufu mkubwa wa vipando aina zote kama vile magari, pikipiki pamoja na hizi baskeli ambazo anazozizungumzia Mhe. Mjumbe.

Lakini kwa ajili ya Mabibi na Mabwana Shamba hivi sasa kwenye maghala yetu tunazo baskeli nyingi sana tena za kutosha. Kwa hivyo, hao ambao watakaoajiriwa basi wote wataweza kupatiwa baskeli na jitihada inaendelea kufanywa na serikali kuongeza vipando vya moto kwa ajili ya maafisa wengine wa wizara yangu. *(Makofi)*

Nam. 6

Sera ya Serikali ya Kuchangia Huduma ya Elimu

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa). (Makofi)

Nam. 160

Msaada kwa Wakulima wa Mwani

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa). (Makofi)

Nam. 34

Tatizo la Maji kwenye Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 122

Utoaji wa Mikopo ya AK na JK

Mhe. Bikame Yussuf Hamad – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huchukua juhudi mbali mbali za makusudi kiuchumi na kimaendeleo kwa wananchi wake. Miongoni mwa juhudi hizo ni uanzishwaji wa Mfuko wa AK na JK kupitia Benki ya *PBZ*.

Kwa kuwa wananchi walipewa mikopo hiyo hawakurudisha kama ilivyotarajiwa.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kukabiliana na wananchi hao, ili lengo lililokusudiwa lifikiwe?

(b) Ni vigezo vipi vilivyotumika wakati wa kutoa mikopo hiyo?

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, nilitegemea na hili lingeondolewa kwa sababu nimeshajibu sana maswali kama haya. Lakini naomba kwa heshima na kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 122 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Mjumbe kwa kuwa muulizaji sana wa maswali kwa

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kama alivyokuwa Mhe. Rashid Seif Suleiman na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wakati uliopita. *(Makofi)*

(a) Lengo la kuanzishwa Mfuko wa AK na JK ni kuwasaidia wananchi hususan wa kipato cha chini waweze kujikwamua kiuchumi kwa kujiajiri katika biashara zitakazosaidia kunyanyua kipato chao.

Kwa bahati mbaya baadhi ya wananchi waliokopa wamekuwa wagumu kurejesha mikopo hiyo na hivyo, hurudisha nyuma juhudi za serikali za kuwafaidisha wananchi wengi zaidi kupitia mikopo hiyo. Serikali imechukua hatua mbali mbali kukabiliana na tatizo hilo ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa. Miongoni mwa hatua ambazo serikali imechukua ni:-

- Kuwatia wakopaji kupitia kwa Masheha wao na kuwataka walipe;
- Kuwaandikia barua wakopaji hao za kuwataka walipe madeni yao;
- Kumfuatilia mkopaji mmoja mmoja katika eneo husika;
- Kuwapa barua za kuwaita idarani pamoja na kuwataka wajikubalishe kwa maandishi kulipa madeni yao na
- Kuwajulisha kwamba watakaoshindwa kuwajibika katika kulipa mikopo waliyochukua watachukuliwa hatua za kisheria.

(b) Vigezo vilivyotumika wakati wa kutoa mikopo ni kama vifuatavyo:-

- Muombaji wa mkopo awe Mzanzibari
- Awe na Umri usiopungua miaka Kumi na Nane (18)

- Awe amejaza fomu ya maombi iliyopita kwa Sheha
- Awe ana mradi ambao tayari ameuanzisha.

Pamoja na kuwa na vigezo hivyo, maamuzi ya mwisho juu ya muombaji kupatiwa mkopo au laa unategemea na matokeo ya tathmini inayofanywa kuhusu mradi husika ulioombewa mkopo huo.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Je, Mhe. Waziri kutokana na kadhia hii iliyoipata serikali mfuko huu unatuahidi kutakuwa endelevu au ndio mwisho?

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, katika majibu yangu ya maswali yaliyotangulia nimekuwa nikieleza hivi kwamba Mfuko huu ulikuwa na matatizo kama aliyoyaeleza Mhe. Mjumbe pamoja na urejeshaji wa mikopo hiyo. Kwa kweli tumejitahidi sana wakati ule kuifuatilia, lakini tulishindwa na hasa kupitia Benki ya *PBZ* waliona mkopo aliyochukua ni mdogo na ufuatiliaji wake unakuwa ni hasa kubwa.

Hata hivyo, hivi karibuni kama mwezi mmoja uliopita kupitia Benki Kuu ya Tanzania, *PBZ*, wizara yetu pamoja na wale viongozi katika sekta mbali mbali wanaohusika na mikopo hiyo, basi tuliwaita na kufanya vikao vya pamoja. Vile vile fedha hizi tulizizuia kuzitoa kwanza na zile zilizotolewa zilikuwa karibu shilingi bilioni 1.4/= na zilibakia nyengine shilingi bilioni 2.2/=.

Lakini kutokana na kikao hicho hivi sasa mikopo hiyo tayari imeanza kutolewa na itaendelea na *Inshaallah* itaendelea pamoja na kuongezewa Mfuko wake zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kweli watu wanapotaka kukopa hizi fedha ambazo zimeletwa kwa makusudi kwa ajili ya kuwasaidia wanyonge ambao tayari wameshaanzisha miradi ya kujiendeleza, basi kujaza fomu pamoja na washiriki wanaoshirikiana kwenye mikopo hiyo ni pamoja na Sheha, Mkuu wa Wilaya pamoja na Benki ya Watu wa Zanzibar.

Kwa bahati mbaya pamoja na kuwa Sheha ndiye mtu wa mwanzo ambaye anayewajua watu wake. Lakini Benki ndio muamuzi nani apewe na yupi asipewe na kwa vyovyote husababisha lengo lililokusudiwa kuwa na kasoro.
Kwa hivyo, Mhe. Waziri haoni kuwa ni vyema akafanya utaratibu mkopo huu ukawemo kwenye mamlaka yake, ili usumbufu huu usitokee tena.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, aliyoyasema kweli waliyalalamikia wananchi huko nyuma na tukayafuatilia na kuona kwamba upo ukweli mdogo ndani yake. Lakini hata hivyo, huo mdogo hatukuweza kuudharau. Kutokana na kikao tulichofanya Mhe. Naibu Spika, sasa hivi bado tumewaachia masheha waendelee na kazi hiyo, kwa sababu wananchi wale wanawajua wao katika maeneo yao. Hata hivyo, bado wizara yangu sasa itakuwa karibu zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali kufuatilia, kusimamia na kuona kwamba yule aliyepewa hakupewa kwa upendeleo au kwa sababu nyengine yoyote kwa lengo la kupata mkopo huo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba kujua Mhe. Waziri hivi sasa ni wangapi ambao hawajalipa na ni wangapi ambao wameshalipa.

Lakini jengine Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuwa serikali imetoa tu fedha bila ya kutoa taaluma.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, hivi sasa kama nilivyosema awali kwamba jumla ya fedha ambazo zimetolewa mkopo zimefika shilingi bilioni moja na laki nne. Jumla ya pesa hizi zilikuwa shilingi bilioni tatu laki sita, shilingi milioni mia sita zimetolewa na Mfuko wa AK, shilingi milioni mia sita zimetolewa na Mfuko wa JK na kilichobakia ilikuwa PBZ wakiongezee pale, yaani zile pesa za Mfuko wa AK na JK zilikuwa ni *guarantee* kwa ajili ya kupata mkopo ule.

Baada ya kutolewa 1.4 bilioni kilichorejeshwa hakikuzidi shilingi milioni mia nne, ndio maana yake tukafanya vikao na tukazuia na nina furaha kusema sasa hivi mikopo hiyo inalipwa vizuri na inaendelea na tusiwe na mashaka yoyote.

Suala la pili sikulifahamu vizuri namuomba Mheshimiwa alirejee kidogo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, nilimuuliza Mhe. Waziri ni wangapi ambao hawajarejesha ule mkopo waliopewa na ni wangapi ambao wamesharejesha mkopo waliopewa. Wizara yake au serikali haioni kuwa imetoa tu fedha bila ya kutoa taaluma kwa wale walengwa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, hivi sasa moja katika kazi ambayo inafanyika katika wizara yetu kwa kushirikiana na benki tunaendelea kutoa taaluma. Ni kweli walipokopa wananchi mwanzo walisikia tu kwamba kuna mikopo ya AK na JK wakafuatana na kwenda kuchukua mikopo ile bila ya kupewa taaluma. Kwa sababu ni vizuri kabla hujatoa mkopo kwanza uelewe kile mwananchi anachokifanya katika eneo lake, ukishakielewa unampa taaluma na ndio maana sasa hivi tunapita katika maeneo yote kuwapa taaluma na wale waliobahatika wakanialika nikenda katika majimbo yao.

Moja katika jambo ambalo nasisitiza ni kwamba kabla hatujatoa fedha zile tunahitajia kutoa mkopo si kwa wakopaji wa Mifuko ya AK na JK hata Mfuko wa kujitegemea pamoja na Mifuko mingine ambayo tunatoa vile vile. yake hawa. Kupitia mabenki tunatoa taaluma hizo, *SACCOS* mbali mbali wamekuwa wakipata taaluma. Kwa hivyo, hilo tutalipa kipaumbele na katika bajeti yangu nimelieleza wazi kwamba kazi ya msingi ambayo tutaifanya katika kipindi hiki cha miaka mitano kila wakati tutakuwa tunatoa taaluma kwa wananchi wetu ili waweze kufaidika na mikopo ile na walipe bila ya kupatiwa bughdha za aina yoyote.

Nam. 169

Taasisi Binafsi Kuwanyanyasa Wafanyakazi

Mhe. Kazija Khamis Kona – Aliuliza:-

Kwa kuwa serikali hutoa wito kwa wananchi kujiajiri wenyewe. Na kwa kuwa vijana wengi wanaofanya kazi katika hoteli husumbuliwa na waajiri hawa kutokana na sababu mbali mbali.

Je, Mhe. Waziri, serikali ina mpango gani wa kuzisimamia Taasisi za Watu Binafsi hususan hoteli ili kukomesha unyanyasaji wa wafanyakazi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 169 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kutanguliza maelezo mafupi juu ya suala hili kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa ni kweli kwamba serikali yetu imekuwa ikitoa wito kwa wananchi wetu kujiajiri wenyewe ili kupunguza tatizo la ajira nchini. Aidha, sheria zetu za kazi na miongozo ya kimataifa ya mambo ya kazi zinasisitiza ajira zenye heshima au staha na zinakataza aina yoyote ya ubaguzi na udhalilishaji katika sehemu za kazi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Sheria ya Ajira Nam. 11 ya mwaka 2005, imekataza unyanyasaji wa aina yeyote kama nilivyotangulia kusema, kwa wafanyakazi walioajiriwa pamoja na wote ambao wamo katika hatua ya kuomba kazi. Hivyo, mwajiri yeyote anayesumbua na kuwanyanyasa wafanyakazi ni makosa kisheria na akibainika hatua za kisheria zinapaswa kuchukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, katika kusimamia hili kikamilifu, wizara yangu imeimarisha shughuli za ukaguzi katika sehemu za kazi ikiwemo maeneo ya hoteli za kitalii. Aidha, tumeongeza mashirikiano na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi na Jumuia ya Waajiri katika kuwaelekeza waajiri juu ya wajibu wao wa kisheria wakulinda haki za wafanyakazi, ikiwemo kutowanyanyasa. Tumeendelea kutoa elimu juu ya Sheria za Kazi kupitia vipindi vya kila wiki kwenye vyombo vya habari. Pia tumekuwa tukiwakutanisha waajiri na waajiriwa pale panapotokea migogoro kwa lengo la kuwasuluhisha na kujenga mahusiano mema katika sehemu zao za kazi.

Mhe. Naibu Spika, napenda kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba mwezi wa Februari mwaka huu, wizara yangu ilishachukua hatua kwa baadhi ya waajiri kutoongeza muda wa vibali vyao vya kazi. Waajiri hao waliohusika ni pamoja na Hoteli ya Lagema, Hoteli ya Kempinski, Hoteli ya Pwanimchangani na *Spice Island Hotel*.

Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa wito kwa wananchi wote wanaofanya kazi katika sekta binafsi na za umma kutoa taarifa haraka wizarani kupitia Kamisheni ya Kazi pale matendo ya ukiukwaji wa haki za wafanyakazi pamoja na unyanyasaji katika kazi unapojitokeza. Aidha, wizara itaendelea na juhudi yake ya kuelimisha waajiri na wafanyakazi kuhusu sheria za kazi ili kuweza kusimamia vyema utekelezaji wake.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna baadhiya mahoteli hawawafungishi mikataba wanaowaajiri? Na kama unakubaliana na mimi, wizara yako itachukua hatua gani kuhakikisha wanaoajiriwa wanapewa mikataba yao.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, nakubaliana wewe mama. Hatua ambazo tutazichukua Mhe. Naibu Spika, tumeaza sasa hivi kupitia mikataba yote ya wafanyakazi na tuansema wafanyakazi wowote, mahala popote walipo kama wameajiriwa wasikubali kuajiriwa bila ya kuwa na mkataba.

Tatizo linalotokea Mhe. Naibu Spika, mtu hutaka kazi apewe, sasa anapotaka kazi huambiwa tutakulipa hiki na kwa vile ana shida ya kazi anakubali, lakini ni kinyume na sheria ya kazi kwa mujibu wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*). Huwezi kumuajiri mfanyakazi popote pale katika sekta binafsi au sekta ya umma kama mfanyakazi yule hana mkataba tena wenye uhakika na wa kudumu au wa muda mfupi ambao mnakubaliana wenyewe.

Kwa hivyo, hilo tunalifanyia kazi, hivi sasa wafanyakazi wote pamoja na katika mahoteli na viongozi wote wa sekta mbali mbali za binafsi na umma tumetoa maelekezo ili kuwe na mikataba na Alhamdulillah nashukuru watendaji wanaohusika na ukaguzi wa wafanyakazi wanapita huko sasa hivi na wametuletea kesi kama hizo ambazo Mhe. Mwakilishi ameziona. Kwa hivyo, tutajitahidi na

Mwenyezi Mungu atatujalia tutaweka hali nzuri kwa wafanyakazi wetu nao wapate kazi za heshima na za uhakika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa inavyoonekana sasa hivi hakuna sheria inayowalazimisha waajiri kuwajazisha mikataba wale waajiriwa. Je, wizara yake Mhe. Waziri itafanya utaratibu gani kwa kuanzisha au kufanya marekebisho ya sheria ili wale waajiri iwalazimishe kuwajazisha mikataba wale wanaoajiriwa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, sheria zipo tatizo ni utekelezaji, kama vile tunavyoambiwa tukiendesha pikipiki au vespa tuvae *helmet* na watu hawavai. Kwa hivyo, tatizo ni utekelezaji wa ile sheria yenyewe. Tunachofanya sasa hivi ni kuwabana hao wanaowaajiri ambao hawawapi mikataba kwa sababu sheria ipo na zinaeleza kwamba mkataba wa miezi mitatu pengine muda mfupi, miezi sita au mwaka, miaka miwili kuna taratibu zake zimeelezwa wazi wazi kwenye sheria hiyo na namna ambavyo tunawajibika kuitoa.

Mhe. Naibu Spika, labda kitu kimoja ambacho kinaweza kuwa kina-*flexibility* kidogo ni kiwango cha chini cha kumlipa mfanyakazi wa chini katika sekta binafsi ambacho hicho kinangojea waziri atoe tamko baada ya kupata ushauri wa Kamati ya Ushauri wa Mishahara. Kwa hivyo, huwa inabadilika, kwa mfano wenzetu Tanzania Bara mfanyakaiz wa chini uko mkataba kabisa amejaza kwamba, endapo anaajiriwa nyumbani kama ni *domestic worker* anawajibika kama atalala na kula pale pale basi atapatiwa shilingi 20,000 kwa mwezi, kama hatolala pale yaani anafanya kazi na kuondoka anapewa shilingi 65,000; isipokuwa hili la chakula ni la kibinadamu tu, lakini hasa ni lile la kulala.

Kwa sababu hata hawa ambao wanafanya kazi majumbani wanapewa chakula na mshahara wao wanapata ule ule waliokubaliana kati ya muajiri na mfanyakazi mwenyewe

anavyojikubalisha, lakini tatizo tumebaini hata hao wafanyakazi wanaofanya kazi humo majumbani wengi hatuna mikataba. Sasa na hilo tunaliangalia na tujiandaeni tulioajiri vijana wafanyakazi nyumbani huko lazima tuwape mikataba, vyenginevyo wanaweza kwenda kutushtaki wakadai haki zao kwa sababu nao wanataka hifadhi wale. *ZSSF* na wao walipie vile vile ili wakimaliza muda wa miaka miwili angalau wajue wanaondoka na kitu gani. Kwa hivyo, Mhe. Naibu spiuka, naomba kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba sheria zipo tatizo ni ufuatiliaji wa sheria zenyewe.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la nyongeza amekiri kama sheria ipo lakini ufuatiliaji ndio umekuwa mdogo. Je, atakubaliana na mimi kama wananchi wanaoajiriwa bila ya kuwa na mikataba hao wanafanya kwa sababu hawajui sheria. Kama wanafanya hivyo kwa kuwa hawajui sheria, lakini atakubaliana na mimi kuwa wawekezaji wao huwa wanajua sheria hiyo na wanaajiri hivyo kwa ajili ya kuwanyima wananchi haki yao ili wasiwapatie. Je, kwa sababu Mhe. Waziri kakiri sheria ipo wizara yake imechukua hatua gani za kufuatilia na kujuwa wawekezaji wanaowafanyia unyambi wananchi na kuwachukulia hatua za kisheria kama sheria inavyotaka.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, nimeeleza katika majibu yangu kwamba tumechukua hatua. Kwa mfano, Hoteli ya *Africa House*, Meneja yule alikuwa ananyanyasa wafanyakazi. Lakini wafanyakazi wenyewe kwa sababu kizazi kilichokuwepo sasa hivi ni tofauti na vizazi vilivyopita wanatambua mambo mengi ni kuhimizana tu, ndio maana wito huu tunaoutoa kwamba ikitokea unyanyasaji wa aina yoyote waje katika wizara ianyohusika hatua zitachukuliwa.

Africa House Hotel Meneja aliyekuwepo alikuwa ananyanyasa wafanyakazi, wafanyakazi siku moja wakajikusanya wakaja pale wizarani walifika mpaka ofisini kwangu, hatua tuliyoichukua tumesimamisha kibali na yule mama tumemuondosha hapa,

hatuwezi kukubali Mzanzibari akanyanyaswa. Lakini tunatoa wito kwa wananchi pamoja na vijana wetu ambao wanatafuta kazi katika maeneo mbali mbali wasikubali kuajiriwa tu bila ya mkataba, lakini tunarudi pale pale Mhe. Naibu Spika, kutokana na haja ya kupata ajira ana hiari asijaze mkataba ili apate chochote pale aondoke nacho. Mimi nasema kwamba hili ni suala zito sana na linahitaji umakini, ni vyema wafanyakazi wetu wastahamili ili wapate mikataba, vyenginevyo wataendelea kunyanyaswa na watapokuja kulalamika hawatakuwa na haki kwa sababu hawana mkataba.

Sasa kazi tunayoifanya sasa hivi ni kuwaelimisha hao wananchi kwa ujumla kupitia vyombo vya habari, redio na magazeti na maeneo mengine. Tunajitahidi kufanya hivyo ili kutoa wito kwamba kila mmoja aweze kufahamu hilo kabla hajaajiriwa awe na mkataba wake.

Nam. 28

Barabara ya Gombani - Vikunguni

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Gombani (*Korea*) kupitia Gombani ya Kati hadi Vikunguni, ni kiungo muhimu katika vijiji vyote vya Jimbo la Wawi, na kwa kuwa katika barabara hiyo kuna daraja ambayo kwa sasa ni mbovu na kuna maeneo yanahitaji kuwekwa kalavati ili yaweze kupitika nyakati za mvua.

Je, ni lini serikali itaifanyia matengenezo barabara hiyo ili iweze kupitika.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 28 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa barabara ya Gombani (Korea) kupitia Gombani ya Kati hadi Vikunguni ni kiungo muhimu katika vijiji vyote vya Jimbo la Wawi. Kutokana na umuhimu huo, wizara yangu kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara Pemba itazifanyia matengenezo ya dharura pale hali ya fedha itakapo ruhusu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kushirikiana na Mfuko wa Barabara tuna matarajio ya kufanya matengenezo makubwa ya uwekaji wa kifusi, *culvert* na mengineyo. Malengo ya wizara yangu ni kuiunganisha barabara hii na barabara ile ya kutoka Vikunguni hadi kufikia eneo la Mzambarau Mboko kwa kuiunganisha na barabara ya Ole/ Kengeja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri ni lini hiyo hali itaruhusu ili wananchi wapate kujiandaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, mataratjio yetu kwamba katika bajeti hii inayopita Mfuko wa Barabara utatenga fedha kwa ajili ya ukarabati huo tunaoueleza.

Mhe. Salum Amour Mtondoo: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii na naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Katika Jimbo la Bububu kuna barabara iliyoanzia kwa Kisasi hadi Mashine ya Maji, Mwanyanya na kutokezea Kijichi. Barabara hii ilisaidia sana msongamano wa njia ya Bububu. Kwa kipande kidogo barabara hiyo ilijengwa na Wajapani kwa njia ya msaada, naomba kumuuliza Mhe. Waziri je, serikali ina mpango gani wa kuimaliza barabara hii.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe swali linahusu barabara ya Gombani Korea halihusiani na Bububu tafuta utaratibu mwengine.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika nakushukuru sana, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mhe. Jaku Hashim amesema kwenye bajeti hii ni mategemeo yake kwamba Mfuko wa Barabara utatenga fedha kwa ajili ya matengenezo wa barabara ile iliyotajwa na Mhe. Saleh Nassor. Lakini ukiangalia Bajeti ya Serikali mradi pekee wa barabara mwaka huu ni Mgagadu/ Kiwani. Je, suala hili litatengwa lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, wakati nilipojibu swali la nyongeza la Mhe. Jaku nilichokieleza kwamba fedha hizo tuna matarajio kutengwa katika Mfuko wa Barabara. Mfuko utatenga fedha hizo na makubaliano hayo na matarajio yetu kwamba fedha hizo zikipatikana tutatekeleza ujengaji wa barabara hiyo tuliyoieleza.

Nam. 168

Watembezaji Watalii Kuwaibia Watalii

Mhe. Kazija Khamis Kona - Aliuliza:-

Tunaishukuru serikali kwa kuwapatia vitambulisho maalum watembezaji wa watalii. Aidha, tunawapongeza watembezaji wote kwa kufuata sheria pamoja na uamuzi wao wa kujiajiri wenyewe na kusaidia pato la serikali la $50 kwa mwaka kwa kila mtembezaji watalii. Ingawa husumbuliwa na kukamatwa kwa madai ya kuwaibia watalii.

(a) Je, Mhe. Waziri ni vigezo gani vinavyotumika vya kuwakamata watu wanaotuhumiwa kuwa ni wezi.

(b) Kwa kuwa watalii hutembelea maeneo ya fukwe bila shaka watembezaji watalii hupatikana katika maeneo hayo. Je, Mhe. Waziri ni sheria gani inayowazuia watembezaji watalii kukaa ufukweni.

(c) Kama ipo, serikali imetenga eneo gani kwa watoa huduma hawa kufanya shughuli zao hizi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 168 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, serikali imeweka utaratibu wa kutoa vitambulisho kwa watembezaji watalii kwa lengo la kuwatambua wanaofanya shughuli hizo ili kupunguza kero wanazofanyiwa watalii na mapapasi. Kigezo kikuu kinachotumika na kusema kwamba mtembezaji wa watalii amewaibia watalii ni namna ya mtembezaji huyo alivyowapata watalii ambao atawatembeza katika vivutio vya utalii. Utaratibu unaokubalika ni ule wa kuwapata watalii kutoka mamlaka zinazokubalika (Kampuni za Kutembeza Watalii zilizosajiliwana Kamisheni ya Utalii).

(b) Katazo kwa watembezaji watalii kufanya shughuli zao katika maeneo ya fukwe liko katika mkataba ambao kila mtembezaji watalii hupaswa kusaini kabla ya kupewa kitambulisho. Napenda kukinukuu kifungu hicho,

"Mimi fulani bin fulani nathibitisha na kuweka saini katika mkataba huu kwamba sitofanya kazi kwa kukaa katika maeneo ya fukwe (*Beach*) za mahoteli, maeneo ya Uwanja wa Ndege, maeneo ya bandarini. Na maeneo yanayolingana na nitafuata maadili ya kazi ya kupokea wagenina kuwatembeza kutoka katika Kampuni ya Waongozaji Watalii inayotambulika kisheria au ruhusa ya kutembeza wageni na kamwe sitapokea wageni kutoka kwa mapapasi (*Beach Boy*) watu wa mapokezi au mfanyakazi yoyote wa

hotelini kwa ajili ya kuwapeleka katika matembezi kinyume na taratibu".

(c) Mhe. Naibu Spika, hakuna eneo maalum ambalo limewekwa kwa watembezaji watalii bali huwa ni waajiriwa wa makampuni ya kutembeza watalii na kwa wale ambao wanajitegemea wanaitumia Jumuia ya *"Zanzibar Tour Guide Association"* (*ZATOGA*) ambayo ndio yenye kuratibu shughuli zao zote. Inapotokea mtu, kampuni au taasisi yoyote inahitaji kutembezewa wageni wake huwasiliana na katibu wa umoja huo kwa kuwatembeza wageni wake bali si kwa kukaa ufukweni, mahotelini na sehemu zinazofanana kwa ajili ya kupata wageni ambao mara nyingi huleta picha mbaya kwa kituo cha utalii Zanzibar "*destination*" yetu.

Mhe. Isamail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, pamoja na suala hili la wanaotembeza watalii wana haja ya kupata vitambulisho maalum kumekuwa na mapapasi wengi ambao wamekuwa ni kero kwa wageni wetu wanaotembelea Zanzibar na badala ya kuwa kivutio imekuwa ni usumbufu ambao unapelekea hata watalii wengine kuona kwamba hawapati utulivu wanaouhitaji wanapotembelea nchi yetu. Je, wizara yake inachukua hatua gani kudhibiti suala hili na kuhakikisha kwamba wale ambao hawakuruhusiwa hawafanyi shughuli hizi na hawaharibu taswira nzuri ya nchi yetu kwa wageni wanaotembelea.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli Kamisheni ya Utalii ikishirikiana na wizara tumekuwa na utamaduni wa kila mwaka kukaa kitako pamoja na washiriki au wadau wote wanaohusiana na masuala ya utalii ili kutathmini na kujenga mwelekeo mpya wa namna gani ya kuendesha utalii. Vile vile huwa tunashirikisha Jeshi la Polisi pamoja na vikosi vingine ili kuona namna gani tunaweza tukalinda mapapasi kwa usalama wa watalii.

Kitu hicho tumeshakifanya mwaka huu na nataka kumwambia Mhe. Mjumbe kwamba tumeandaa utaratibu mwengine mpya ambao utaanza hivi karibuni. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe ondoa wasi wasi imani yangu kwamba mambo yote yatakaa sawa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuwa hizi sheria za kuwahujumu hawa mapapasi imepitwa na wakati. Kama unakubaliana na mimi ni lini sheria ambayo itaweza kuwadhibiti mapapasi hao kuletwa kwenye Baraza hili tukufu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, hiyo ni moja katika mikakati yetu vile vile ambayo siwezi kusema kwanza wenyewe wakaja wakasikia imo ndani ya mikakati yetu. Kwa hivyo, ondoa shaka Mhe. Mjumbe.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwa kuwa wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ni wizara ambayo imagusana na wizara mbali mbali. Je, atakubaliana nami Mhe. Waziri kwamba imefika wakati sasa hivi kukusanyanya na wizara ambazo zimehusiana na wizara yake ili kuhakikisha kwamba hawa mapapasi ndio wanaoharibu utalii na baadhi yao ndio wanaowaibia watalii.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, nakubaliana naye ni kweli na ndio moja ya sababu tukajenga mikakati mingine mipya. Hilo suala ni suala zito, lakini hata hivyo tumelitafutia ufumbuzi na ninamhakikishia kwamba haya masuala yote yatamalizika mara tutakapomaliza bajeti hii tutaanza mikakati yetu mipya na tumejenga mkakati mwengine mpya wa uendeshaji utalii Zanzibar.

Nam. 71

Majenereta ya Dharura

(Mheshimiwa aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 181

Viwanja vya Mombasa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mnamo mwezi Disemba 2010 na mwezi Januari mwaka 2011, Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati aliamua kufuta viwanja vilivyotolewa kihalali na Serikali katika eneo la Mombasa kwa Mchina. Katika kufanya hivyo, Mhe. Waziri alitumia mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa vifungu 55 na 56 vya Sheria ya Ardhi Nam. 12 ya 1992. Hata hivyo, hakuna taratibu yoyote kati ya taratibu zilizoelezwa kwenye vifungu hivyo ambazo Mhe. Waziri alizifuata.

(a) Mhe. Waziri, kwa sababu taratibu za kisheria hazikufuatwa huaoni kuwa uamuzi wake wa kufuta hati za viwanja hivyo ni kinyume na sheria na kwa hivyo ni batili.

(b) Kwa sababu hiyo, Je, Mhe. Waziri utakubaliana nami kuwa viwanja hivyo ni halali kwa wananchi waliopewa na Serikali kwa mujibu wa sheria, kuwa bado wana mamlaka ya kuvitumia.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 181 lenye (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Serikali iliamua kuvifuta viwanja vya Mombasa kwa Mchina kwa mujibu wa Mpango Bora wa Matumizi ya ardhi, eneo hilo limepangwa kuwa eneo la wazi (*open space*) na kwamba kwa namna hiyo hairuhusiwi kwa mtu au watu kulitumia eneo hilo kwa matumizi yoyote ambayo yatakwenda kinyume na mpango huo.

Mhe. Naibu Spika, ufutaji huo ni halali na hakuna mtu au taasisi itakayoruhusiwa kuanzisha ujenzi katika eneo hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri atakubaliana nami kuwa ni waziri wa mwanzo tokea kuteuliwa ni muda mfupi tu ndiye waziri unayeongoza kuvuta viwanja. Unaweza kutueleza ni viwanja vingapi ulivyofuta mpaka sasa pamoja na *lease* na umezigawa vipi.

Pili, waliotoa viwanja hivyo pamoja na *lease* walikuwa hawajui kazi zao.

Tatu huoni serikali kuwa utaitia hasara kwa kutokujua ardhi kutokana na sheria za nchi hii.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu zake inawezekana kwamba waziri mimi ndiye ninayeongoza kwa kufuta viwanja, lakini viwanja hivi navifuta kwa mujibu wa sheria kwa sababu sheria imekiukwa wakati vilipotolewa.

Pili, inawezekana kwa alivyozungumza yeye kwamba waziri aliyetangulia labda amekuwa laini, mwepesi kuvitoa hivyo viwanja. Lakini nataka nieleze kama alivyojibu Mhe. Naibu Spika, kwenye swali lake mama kwamba eneo lilofutwa viwanja ni eneo lilokuwa kisheria kwamba ni eneo huru.

Kwa bahati mbaya vimetolewa viwanja, sio kwa bahati nzuri. Waziri mimi najitahidi kufuata utaratibu, kufuata sheria na kanuni ambazo

mimi nimezikuta na hizo ndizo ninazozitumia, sijabadilisha kanuni wala sheria. Kwa hiyo kama moja aliacha, mimi natekeleza. Kwa hivyo hilo ninalolifanya ni sahihi, lakini suala la tatu sikulifahamu namuomba alirejee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri huoni kufuta viwanja hivyo ni kinyume na sheria za nchi hii.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, naomba nilijibu swali hili kwamba Mhe. Jaku alipouliza swali lake alivitaja vifungu vya sheria nilivyovitumia kuvifuta viwanja hivi. Kwa hivyo sio kinyume cha sheria ni kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kuwa ni Waziri makini anayefuata sheria na kaamua kufuta viwanja. Nampongeza sana.

Sambamba na hatua hiyo ya kufuta viwanja ambao wameathirika ni wale waliopewa viwanja na Serikali hii ya Mapinduzi Zanzibar. Lini atachukua hatua ya kuwajibisha wale waliotoa viwanja kinyume na utaratibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mhe. Hija kwa suala lake zuri alililoliuliza na litawapa faida wengi watakaonisikia nikilijibu.

Mhe. Naibu Spika, nilipofika katika Wizara hii nilikuta kuna matatizo mengi sana ya viwanja. Ingawa bado kuna matatizo ya maji, kuna matatizo ya umeme na kadhalika. Lakini matatizo ya viwanja yanaongoza. Ninahakika mpaka nitaondoka katika Wizara hii bado matatizo ya viwanja yatakuwa yanaendelea.

Mhe. Naibu Spika, jana ulikuwa umekaa pale nimekuona wakati Mhe. Abubakar anafanya majumuisho hotuba yake. Alilizungumza tatizo la yule mzee aliyopewa nyumba na tajiri wake, nyumba ile ikataifishwa kinyume na taratibu, ikawa *declare* kwamba

imetaifaifishwa kinyume na taratibu. Nyumba ile ikauzwa kinyume na utaratibu. Jana Mhe. Abubakar alisema hili suala atalifuatilia kwa nguvu zake zote na aliyehusika au waliohusika atawawajibisha kwa kuwapeleka katika vyombo vya sheria. Ndio maana nikasema tatizo hili litakuwepo na litaendele.

Mimi nilipofika katika Wizara hii nilifanya marekebisho makubwa na hii ilikuwa ni hatua ya mwanzo ya kuwawajibisha wale waliokuwa wanakwenda na Kanuni na taratibu za ugawaji wa ardhi na usimamiaji wa viwanja. Ningefanya marekebisho na nilipata hujuma nyingi kwa maneno kwamba nimemng'oa simba na masharubu yake. Ni usemi wa wananchi waliokuwa wanazungumza.

Mimi sikufanya hivyo, niliwaondosha na niliwabadilisha kwa mujibu wa sheria na taratibu za kazi. Niliwaondosha wafanyakazi ambao walizoea kuikorofisha Wizara hii na nikawaweka wale wengine ambao nashukuru hivi sasa tunakwenda vizuri.

Hatua ya pili kama itatokea kwamba kuna makosa ya jinai, sasa nitashirikiana na Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Abubakar kulizingatia hilo na hapo hatua zitachukuliwa. Ahsante sana.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2011/2012
Wizara ya Afya

(Majadiliano yanaedelea)

Mhe. Asaa Othman Hamad: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema kuweza kukutana tena asubuhi hii.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Afya kwa umahiri wake aliouonesha jana kitabu kikubwa kilichojaa matumaini ya Wazanzibari kwa mwaka 2011/2012. Alitumia masaa 2:10 hongera sana mwalimu. Niipongeze Wizara kupitia kwake Mhe. Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi wanayokabiliana nayo siku hadi siku kuwatumikia Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, nipongeze kwa kwazi nzuri ya miradi na programu kama vile Malaria, Kichocho, Matende na Mabusha kwa kiasi kikubwa tumepata mafanikio. Lakini kwa hospitali yangu ya Wete pamoja na mafanikio haya, napongeza vile vile kwa kuondoa tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama kwa hospitali ile.

Mhe. Naibu Spika, afya ni uhai. Sasa hivi Zanzibar tumekabiliwa na tatizo kubwa la wimbi la magonjwa mbali mbali. Wataalamu wanatwambia kila mtu mmoja akiwa na kilo za uzito wa X basi atakuwa na kilo kumi ni sumu ndani ya mwili wake. Sumu hii inachangiwa na vyakula mbali mbali tunavyokula bila ya utaratibu na kutokufanya mazoezi ya viungo.

Mhe. Naibu Spika, naiyomba Wizara ya Afya iendelee na kutushauri kadiri inavyowezekana ili jambo hili lieleweke kwa kila mmoja wetu na umuhimu wa mazoezi na upimaji wa afya zetu siku hadi siku.

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, kuna wimbi la ugonjwa wa saratani. Niliwahi kusikia wataalamu wa magonjwa haya wakasema kwamba wagonjwa wanaoripoti pale Dar-es-Salaam Ocean Road asilimia arubaini wanaathiriwa na tumbaku. Matumizi ya tumbaku yana hasara kubwa kwa afya ya mwanadamu. Wakaendelea kusema kutibu mgonjwa wa saratani anahitaji kutumia milioni 4 na ushei lakini haijawa ni uhakika kwamba atapona.

Mhe. Naibu Spika, matumbaku pamoja na sigara, Zanzibar sasa hivi vijana ni kwa kasi kubwa hatimaye inakwenda kwenye bangi.

Ningeshauri na kuiomba Wizara ya Afya itafute namna angalau sheria itakayoweza kupunguza matumizi ya sigara hasa hadharani ama kwenye vyombo vya usafiri.

Mhe. Naibu Spika, wavutaji wa sigara hawachagui maeneo aidha kuna mtoto mchanga, kuna mama mjamzito vyovyote vile muda umefika atawasha sigara. Nadhani kutunga sheria ni kuwanusuru Wazanzibari ni kuinusuru serikali gharama ya kuwatibu watu wakaoathirika na magonjwa haya yasiyokuwa ya lazima kupitia tumbaku. Kulikoni tukasema uhuru wa mtu lakini uhuru wa mtu usiathiri pia maisha ya mtu nadhani itakuwa tupo sahihi.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mazuri mengi ambayo wizara imefikia na matumaini ya kitabu hiki. Mimi bado nitakuwa na masikitiko kwa wizara hii kwamba bado hawajataka kuona umuhimu wa uwiyano wa hospitali zetu hizi za Unguja na Pemba katika mgawanyo mzima wa fedha za kimaendeleo.

Mhe. Naibu Spika, wewe mwenyewe ni shuhuda, Waziri aliyekuwa na dhamana ya Wizara hii tulifika mahali tulipopafika juu ya mgawanyo na akakiri kwamba sasa angefuata utaratibu ule tuliokubaliana. Miradi ya maendeleo ipo kote kote na inaumuhimu pande zote mbili za visiwa. Hospitali ya Wete imerithiwa tokea ukoloni. Sasa hivi mapokezi ya wagonjwa, mahitaji ya huduma katika hospitali ile yameongezeka kufuatana na ongezeko la watu. Majengo ni mafinyu sasa hivi, hivyo wangeona hawa wenzetu wanaotoa mgao huu wa miradi ya kuendeleza majengo yale au ukarabati yanapewa umuhimu unaofaa.

Mhe. Naibu Spika, uendeshaji wa miradi ya maendeleo Afisi Kuu Pemba, mwaka huu ulioishia June, walipewa 176 milioni. Mwaka huu 2011/2012 Mipango Sera Utafiti wana 46 milioni. Uendeshaji na Utumishi 69. Afisi Kuu Pemba kwenye bajeti wana mapungufu ya 71 milioni ambazo zingewawezesha na wao angalau yale amaeneo ambayo sasa hivi yanahitaji yapate afuwa wangeweza kumudu. Lakini hayakutiliwa kitu, hata kama tulivyozoea kuambiwa

kwamba fedha zinazotengwa Unguja kwenye miradi mbali mbali ndio hiyo hiyo zinazopelekwa Pemba pale zinazohitajika. Kama hivyo inafanyika ni kwa nini ikwame miradi ile kule Pemba.

Kuna majengo ambayo sasa hivi yanahitaji ukarabati mkubwa kama sio ujenzi. Lakini hayakutiliwa fedha. Hali hii Mhe. Naibu Spika, Waziri mwenye dhamana na Wizara hii mimi ni mwalimu wangu. Ni mwalimu wangu mara mbili, tatu. Nisingependa kusema vibaya sana mbele yake. Lakini sitowatendea haki wananchi kama wizara yake itaendelea na utaratibu huu. Nikimwambia sitokubali mimi nipate jibu.

Mwaka jana waziri alikubali kwamba atatoa mgao kwa Idara zote kwa mujibu wa mahitaji na kwa mujibu wa fedha zitakavyopatikana. Leo limerudiwa hili hili maana yake kuna mtu au kuna watu hawataki yaendelee yale ya kule Pemba ndani ya Wizara yake. Jambo ambalo na mimi hilo sitokubali. Mhe. Waziri nikisema nitazuia fungu hili nipate jibu sahihi. Miradi ya maendeleo kuna maeneo pale kuna vijana wameletwa juzi nyumba za kukaa hawana, tunasaidia kuwapatia maeneo. Kuna majengo kama vile ya miradi, sasa hivi yanahitaji kufanyiwa ukarabati, pesa hazikuoneshwa hapa.

Mhe. Waziri akiniletea jibu kwamba fedha zilizokuwepo Unguja ndizo zitakazopelekwa Pemba. Kwa nini hivi sasa zisionyeshwe. Kama ndivyo hivyo fedha zilizotengwa Unguja ndizo zitakazotenda shughuli za miradi Pemba ilikuwa leo hapa tuone kwenye kitabu. Wakuu wa Idara hizo Pemba fungu lao ni hili, lakini hivyo haikufanywa. Mhe. Waziri atakaponipa jibu hilo la kunitajia Pemba miradi yao wakuu wa vitengo, akizitaja mimi nitakubaliana naye. Vyenginevyo hapa kwanza nitazuia fungu hili kwenye bajeti yake.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme wenzetu Wizara ya Afya wana kazi nzito, wanahitaji kupatiwa fedha kadiri inavyowezekana serikali ikubali kwamba zinahitajika na kuna matumizi. Tunapoteza wataalamu na madaktari wa wizara hii kutokana na huduma duni tunazowapa. Utafiti unaonesha kwamba tuna madaktari nje ya

Zanzibar ni 216. daktari bingwa wa maradhi ya moyo ni Mzanzibari yupo Swizaland. Hali hii kadiri inavyoendelea sisi tunasomesha tukishasomesha watu wanaondoka na sababu ya kuondoka inajulikanwa.

Nadhani wakati umefika. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais wewe tuko na we kwenye Baraza hili Tukufu serikali iyone kwamba kuendelea kupoteza madaktari wetu, wataalamu wetu ni hasara kwa Zanzibar yetu. Madaktari hawa au wahudumu wote wanakutana na maeneo magumu katika shughuli zao za kila siku. Maeneo hatarishi wanayofanyia kazi, mishahara yao duni na hata yale maposho ambayo yangewapa matumaini nayo hawayapati.

Mhe. Naibu Spika, tuitizame Wizara ya Afya kama vile tunavyoitizama Wizara ya Elimu, tunavyoitizama Wizara ya Kilimo. Tunahitaji Wazanzibar wawe na afya bora waweze kuzalisha mali. Uchumi wetu utajengwa na watu wenye afya. Wakiwa wabovu hawataweza kufanya kitu itakuwa ni hasara tu kila siku kutafuta pesa kutibu wagonjwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya salamu hozo kwa serikali niseme mimi mwakilishi wa watu wa jimbo la Wete bado sijafurahishwa sana na namna ya ajira ya Wizara hii. Wahudumu ni muhimu kwa maeneo yao. Na watendaji wengine wana umuhimu wao, wahudumu wanafanya shughuli za usafi na kadhalika. Kwa kule kwetu sasa wahudumu wanafanya mpaka kazi za nesi, ajira haifanywi.

Mhe. Hahi Omar Kheri hayupo lakini salamu azipate. Tunahitaji Wizara ya Afya tunaomba hilo waajiriwe wahudumu na wazanzibari. Ule mtindo uliozoeleka uwe basi, kupitia Masheha wakafanya vituko, hii lugha inaeleweka. Tafadhalini tunaomba hatutaki turudi tunapotoka. Wenye haki za ajira nchi hii ni Wazanzibari wenyewe ilimradi ame *qualify*. Sheha kumpa kitambulisho asiyekuwa na haki akampa haki, huu mtindo ufe basi. Mhe. Makamo unatusikia tunasema hatutaki turudishwe tulikotoka.

Wazambia anapewa kitambulisho cha Mzanzibari, mwanangu miye anasoma Mbweni anakataliwa kupewa kitambulisho kile ninae hivi sasa yupo. Naomba sana hali kama hii inatukasirisha sana. Kumpa mtu mirathi isiyokuwa yake, Mungu kakataza na sisi pia tunakataza. Sisi wanadamu tulioumbwa na Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, baada ya hayo ni machache kutokana na mengi yaliyopo, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja anijibu ni namna gani miradi ya maendeleo Kisiwani Pemba imepata *location* yao. Sitaki jibu zao zipo Unguja. Baada ya kusema hayo nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante ndugu Wajumbe kabla sijamkaribisha Mhe. Mtondoo naomba nitoe taarifa kwamba tunao wanafunzi wamekuja kututembelea hapa kutoka Skuli ya Sekondari Ndijani wamekuja kusikiliza michangio naomba wasimame pamoja na mwalimu wao. Ahsanteni sana kaeni.

Mhe. Salum Amour Mtondoo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na miye kuchangia machache katika Wizara ya Afya. Kwanza naomba kumpongeza Mhe. Waziri kwa jitihada yake kubwa hasa ukakamavu aliotuonesha jana. Inadhihirika kwamba babu bado huyo mzima.

Vile vile napenda kumpongeza kwa moyo aliyotuonesha wakati wa hospitali ya Mnazi Mmoja ina matatizo ya maji kwa kipindi kifupi kuweza kufanikisha tukapata maji. Ni mfano bora wa kiongozi mzuri. Tunamshukuru sana babu kwa kutumalizia shughuli hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kupitia hotuba ya Mhe. Waziri jana,. naanza kuchangia katika ukurasa wa 17 kitengo cha afya ya Wafanyakazi. Tumekuwa na matatizo hasa kwa upande wa mikahawa yetu, pamoja na mama nitilie wetu. Mikahawa yetu baadhi yao ipo katika hali mbaya ya kiafya. Naiyomba wizara iwe na jitihada za makusudi. Wengi wetu huwa tunaponea katika mikahawa hii, uzuri wa mikahawa hii pale unapoingia sehemu ya kulia. Lakini ukenda jikoni

hakutamaniki. Tunawaomba wahusika wanapofanya ule ukaguzi wao wapitie na jikoni. Hayo maji kidogo yanatutia wasi wasi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 40 umegusa hospitali ya Kivunge. Kivunge ni hospitali yetu ya Wilaya ni sawa na hospitali ya Makunduchi. Hali ya hospitali ya Kivunge ipo katika hali mbaya sana, kuanzia majengo hata mambo yake ya ndani. Jana nimehudhunika sana na maelezo niliyoyapata katika hospitali ya kivunge. Kwa kiasi fulani nimelia wivu kwa maendeleo waliyoyapata wenzetu wa Makunduchi. Wananchi wa Kaskazini na wao wanaomba hospitali ya Kuvungwe itizamwe kwa sababu inatusaidia sana kuhudumia wananchi wetu kule.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nitaigusia hospitali ya Mwembeladu katika ukurasa 53. Hospitali hii inaisaidia sana hospitali ya Mnazimmoja akina mama wanakwenda pale kujifungua. Lakini tukizungumza hivi sasa hivi hospitali ya Mwembeladu haina *heater* ya maji ya moto kwa akina mama baada ya kumaliza shughuli zao za kujifungua, vyandarua kwa akina mama na watoto wanaozaliwa hakuna, kwa hivyo imo katika hali mbaya.

Mwisho napenda kugusia katika maelezo ya Naibu Waziri, wakati wa Maswali na Majibu. Tuligusia sana hospitali zinazojengwa na wananchi kupitia majimbo yao. Wananchi wameamua kujenga hospitali baada ya kugundua tatizo. Mfano mzuri mimi katika jimbo la Bububu katika Shehia ya Mwanyanya kwa moyo mmoja wananchi wameamua kuwasaidia wananchi wa Kibweni na Mwanyanya, japokuwa kuna hospitali ya karibu ya KMKM. Lakini kutokana na utanuzi wa mji ulivyokuwa sasa, hospitali hii itawasaidia sana ndugu zetu kupata huduma pale.

Mhe. Naibu Spika, kidogo nimepatwa na wasi wasi kutokana na jibu alilojibiwa Mhe. Subeit wa Micheweni kwamba wamejenga hospitali lakini hospitali hii sasa haitosaidia kitu. Kwa hivyo naiyomba Wizara ithamini nguvu za wananchi, kwa sababu mtu

kutwambia hospitali yetu ya Mwanyanya sijui tuifanye nini. Kwa hivyo, tunaiomba wizara kuzijali zile nguvu za wananchi ili kuwapunguzia masafa kwa kufuata huduma ya afya, kwa sababu huduma ya afya ina umuhimu wake.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Bububu tuko pamoja kuichangia wizara hii.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Afya. Kwanza nataka nimpongeze Mhe. Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kukubali kuwaongeza wafanyakazi mishahara kwa asilimia 25. Kwa hivyo, natoa hongera na huu ndio ubinadamu kwa sababu binadamu wakati anapofanya kazi wajibu wake afurahishwe. Pia napongeza wizara zote hususan Wizara ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Wizara ya Makamo wa Pili wa Rais na Wizara nyengine zote zilizobaki.

Mhe. Naibu Spika, pia nawapongeza Wajumbe wote wa Baraza hili la Wawakilishi waliochangia na wasiochangia. Mimi nikianza katika hotuba hii nije katika ukurasa wa 80 kuhusu mradi wa afya, uzazi na mtoto.

Mhe. Naibu Spika, mzazi anahitajika sana kupewa kipaumbele katika kuhudumiwa juu ya mambo yake ya afya. Mhe. Naibu Spika, pia mtoto anahitajika kuhifadhika katika mambo ya afya na kuhudumiwa, kwani mtoto ndio mlezi wa wazee hapo baadaye. Kwa hivyo, mtoto tukimuhifadhi pamoja na mzazi nafikiri ndio huduma zitakuwa nzuri. Hivyo, mimi napongeza sana katika kitabu hiki kwamba amepewa kipaumbele mtoto pamoja na mzazi kwani mzazi ndiye mama na mtoto ndiye muhifadhi wa wazee wa baadae. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kitabu chake hiki alichokitunga nahakikisha kwamba Wizara ya Afya itawahudumiwa sana watoto na wazazi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nataka niipongeze sana wizara hii kwa kuisafisha Hospitali ya Mnazi Mmoja, mimi wakati ninapotembea kwenye hospitali hiyo hivi sasa iko safi na nzuri. Kwa hivyo, nawapongeza kwa hilo. Mhe. Waziri ningeliiomba Wizara ya Afya hivi sasa ichukue hatua ya kutuelimisha juu ya madaktari tuliokuwa nao hapa Zanzibar ni kidogo tunategemea sana madaktari wa nchi za nje.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa tunategemea sana madaktari wa nchi za nje basi hasara itatupata sana kwa sababu ile fedha ambayo tunakusudia kuwapa madaktari wetu wa hapa itabidi tuwape madaktari wa nchi za nje. Kwa hivyo, serikali pamoja na wizara hii naiomba iongeze vyuo vya kusomeshea watoto wetu katika sehemu hii ya afya kwani kituo kimoja kilichoko Mbweni ni kidogo hakikidhi haja.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri kuwa hivi sasa nchi yetu ya Zanzibar imekuwa tena sana hasa katika Mkoa wa Kaskazini “A”. Mhe. Naibu Spika, Mkoa wa Kaskazini “A” hivi ina watu wengi ukilinganisha na mjini. Kwa hivyo, mimi naomba Wizara ya Afya ijenge kituo cha kusomeshea afya katika Mkoa wa Kaskazini “B”. Mhe. Naibu Spika, Mkoa wa Kaskazini hivi sasa umekuwa na vijana wengi waliomaliza kusoma.
Mhe. Naibu Spika, ikiwa tutapata kituo cha kusomeshea watoto wetu elimu ya afya, basi tunaweza tukapata ajira na sisi Mkoa wa Kaskazini. Kwa sababu Mkoa huo ni mkubwa lakini umetupwa bado uko nyuma katika hii miradi ya kusomeshea. Mhe. Naibu Spika, wakati nachangia bajeti ya Mhe. Waziri Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nilisema kwamba na kule Kaskazini kiweko kituo cha kuzimia moto, kwa sababu Mkoa wa Kaskazini umeshakuwa mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, katika Mkoa huo sasa hivi kama kutaungua nyumba basi itakuwa ni hatari, kituo kilichowekwa kule Fukuchani ni kwamba hakuna gari itakayoweza kukidhi haja. Kwa hivyo, mimi hapa natilia mkazo katika Wizara ya Afya kuwa tujengewe kituo cha kusomeshea elimu ya afya katika sehemu yetu ya Kaskazini “A”.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nikiendelea na mchango wangu ni kuwa hivi sasa tumekuwa na magonjwa mengi sana, magonjwa mengine hayatibiki. Kwa hivyo, naiomba wizara hii iweze kuchukua utaratibu juu ya kuweza kuchukua hatua ambayo ya kuwapima wananchi kila baada ya miezi kwa sababu hivi ugonjwa tuliokuwa tunao hivi sasa unakuwa mara kwa mara.

Mhe. Naibu Spika, pia kitabu hiki kinatuhimiza sana kujikinga na maradhi ya kichocho. Mhe. Naibu Spika, maradhi ya kichocho yameenea sana, zamani ilikuwa ni katika sehemu zenye mito tu, lakini hivi sasa mpaka zile sehemu ambazo hazina mito basi zina maradhi haya ya kichocho. Kwa hivyo, naiomba wizara hii ichukue hatua ya kuangalia wananchi kwa kuwapima ili maradhi haya yasiweze kuambukiza zaidi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nataka niihimize wizara yetu hii kwani hivi sasa imepata kiongozi mahiri. Mhe. Waziri kwa ukakamavu wake ninahakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar watakuwa na afya nzuri, tena watakuwa na maendeleo mazuri. Vile vile naiomba wizara yetu hii Mhe. Waziri awaangalie na wale ma-*orderly* na wao ni watu ambao wanabeba mzigo mkubwa sana katika kutuuguza. Kwa hivyo, katika bajeti hii asimtazame daktari mkuu tu, pia na wale ma-*orderly* ambao wanatupokea sisi lazima na wao awaangalie sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuheshimu wakati wako mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe naunga mkono bajeti hii mia kwa mia.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi hii ya leo kutujaalia uzima na afya na hivyo kutupa fursa ya kuendelea kuchangia bajeti ya wizara mbali mbali leo tukiwa tumeingia katika Bajeti ya Wizara ya Afya. Pili, nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi

hii ya kuchangia bajeti hii muhimu sana katika wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wale wote ambao wamempongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri, na safi kabisa. Jana nilikuwa nikimtania nje pale baada ya kumaliza kusoma hotuba kwamba tangu tumeanza kupokea hotuba hii ndio hotuba ya kwanza ambayo pia mbali ya kujumuisha mipango yake, lakini pia imetaja changamoto zake ambazo inakabiliana nazo.

Mhe. Naibu Spika, ikawa namtania kwamba katufanya kiasi ambacho hata yale ya kuyazungumza sisi tayari ameshayazungumza yeye. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba yale matatizo ya msingi ambayo inaikabili sekta hii basi ameyazungumza yeye. Hiyo inaonesha ujasiri wa kukubali kwamba kuna matatizo ambayo bila shaka tunapaswa kukabiliana nayo. Kwa hivyo, nampongeza sana yeye na wafanyakazi wake wote wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya.

Pili, Mhe. Naibu Spika naomba vile vile nimpongeze yeye na msaidizi wake yuko makini Naibu Waziri Dk. Sira Ubwa Mamboya kwa kutuonesha mabadiliko katika kipindi kifupi ambacho ameingia katika kuiongoza wizara hii. Naomba niyapitie haraka haraka tu kwa sababu mara nyingi tunakuwa wepesi wa kulaumu, lakini huwa hatutaki kutoa sifa pale ambapo zinastahiki. Mimi naomba nisiwe katika hao.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nipongeze kwa kuona masuala kama tatizo la maji katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na Mwembeladu limepatiwa ufumbuzi, suala la usafi tunaona kuna mabadiliko haidhuru bado kuna kazi inataka kufanyika zaidi. Lakini pia juzi nilikuwa na mtu ananiambia kwa mara ya kwanza ameona baada ya miaka mingi hospitali kunateremshwa mizigo ya ma-*file* na vyeti. Kwa hivyo, nikurejea katika utaratibu wa zamani kwamba kila mgonjwa anakwenda pale na file lake na utaratibu wa kuwa na rikodi zake kamili katika utaratibu ulozoeleka katika mahospitali.

Mhe. Naibu Spika, pia wametwambia katika hotuba yao humu kuwa wanakusudia kufanya utafiti kwa kile walichokiita *quality assessment* tools kwa kuhakikisha kwamba wanapata kupima wananchi wanapokea vipi huduma zao. Hili ni jambo zuri kwa sababu yale manung'uniko ambayo wananchi wanayo na wanakabiliana nayo kila siku pale wanapokwenda kufuata huduma hizi watapata kuyaeleza na uongozi wa wizara utapata kujua na kuweza kuyachukulia hatua.
Mhe. Naibu Spika, mimi niwapongeze kwa kulizungumza tatizo ambalo limekuwa muda mrefu Kisiwani Pemba la kukosa wafanyakazi wa sekta ya afya na kuweza kupeleka wafanyakazi 161 katika mwaka huu tunaoendelea nao. Katika jumla ya pongezi Mhe. Naibu Spika, wewe na mimi ni mashahidi tukiwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala tulipotembelea lile jengo la Mkemia Mkuu wa Serikali. Nafurahi kwamba katika bajeti hii ametwambia kwamba serikali hatimae imewapatia jengo katika Kiwanda cha Sigara cha zamani, wizara imepanga kulifanyia matengenezo. Pia kuleta kwa mara ya kwanza sheria itakayokuwa inaongoza shughuli za Mkemia Mkuu. Katika mlolongo huo wa pongezi niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Waziri Mugheir na Mhe. Rais Karume kwa juhudi kubwa walioichukua katika kuleta ule Mradi wa Kupambana na Malaria tukitaka tusitake tukubali ukweli kwamba kiasi kikubwa malaria kiwango chake kimeshuka sana hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, hayo ni mambo ambayo naomba niyapongeze sana kwa wizara hii katika mambo ambayo tumeyaona yameanza kuonesha muelekeo. Katika wizara hiyo hiyo haidhuru sio suala lao moja kwa moja naomba niipongeze sana taasisi binafsi ya *Zanzibar Outrich Program* (ZOP) ambayo imekuwa ikishirikiana sana na wizara hii kutoa huduma na kutafuta misaada kwa watu mbali mbali ili kuwawezesha kufidia yale ambayo wizara kutokana na bajeti yake ndogo inashindwa kuyatimiza.

Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizo sasa niseme binafsi nimesikitishwa sio na wizara hii, nimesikitishwa na kitendo

ambacho nakiona sijui nikiite vipi cha serikali katika *allocation* nzima ya bajeti kwa wizara hii. Mhe. Naibu Spika, nimebahatika kufanya mchanganuo wa bajeti ambazo zimetolewa kwa wizara, ofisi, mashirika na taasisi mbali mbali zilizomo katika kile kitabu kikubwa cha makisio. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya imetengewa bajeti yake yote ni bilioni 13,270,000,000 ambayo ni kama asilimia 3.6 ya bajeti yote.

Mhe. Naibu Spika, jambo hili limenipa mashaka kwani tunaposema katika bajeti hii Waziri wa Fedha alipokuja hapa akasema kwamba kipaumbele cha kwanza cha bajeti ya mwaka huu ni afya, lakini halafu hakiji-*reflect* katika *allocation* ya bajeti, ndio tunasema nini Mhe. Naibu Spika. Nilikuwa nazitizama hapa Wizara ya Afya hata tusipochanganya kwa mfano ukiichukua Ofisi ya Rais Ikulu ukaichanganya na vikosi vyake vya SMZ na Tawala za Mikoa itakuwa nini, lakini tusiende hivyo hata ukichukua kile kimoja kimoja kila moja kwa *allocation* yake vilivyo katika kile kitabu, basi wizara hii ni ya tano.

Mhe. Naibu Spika, ya kwanza ambayo imeongoza hapa ni Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Hii imechukua asilimia 19 ya bajeti yote. Wizara ya pili ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tatu ni Mfuko Mkuu wa Serikali, nne ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano halafu ndio inakuja Wizara ya Afya. Mhe. Naibu Spika, wizara hii imepata kama asilimia 4.8 hizi ni hesabu za haraka haraka nilizozifanya. Kwa hivyo, najiuliza huku tunaambiwa kuwa kipaumbele cha bajeti hii ni Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, hii wizara inayosimamia shughuli hii na shughuli zake tofauti na shughuli nyengine huzikuti zimetapakaa, ukiona labda masuala ya ukimwi nyingi zimejikita hapa. Kwa hivyo, mbona hii bajeti ya *allocation* hailioni hilo tatizo. Mimi nitaomba hili nipate maelezo bahati mbaya Mhe. Waziri wa Fedha hayupo lakini bila shaka atakuja kutupa maelezo kutoka katika serikali.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa kuna maeneo kama nilivyosema kwa wizara hii mimi sitaki kulaumu sana kama nilivyosema kwa sababu nimeona changamoto ambayo wamekabiliana nayo na jitihada wanazozifanya uongozi mpya wa Wizara ya Afya. Lakini naomba tuwasaidie kuyakamilisha baadhi ya maeneo ambayo tunadhani yanapaswa kutizamwa.

Mhe. Naibu Spika, moja ni kuwa pamoja na kusifu tunaweza kuona angalau kuna mwelekeo wa zile *procedure* za hospitali kueleweka. Lakini naomba bado uongozi wa wizara hii ulitizame suala hili, tunapokwenda katika hospitali zetu ule mpangilio hasa kwamba ukifika unapokelewa hapa, halafu unapata utaratibu huu mpaka unamaliza taratibu zote, hauonekani ama kuwepo au kama kuwepo kufuatwa au kama kueleweka pia.

Mhe. Naibu Spika, nilibahatika ingawa sio bahati nzuri sana kwenda ku-*attend* mgonjwa Mwenyezi Mungu amrehemu Maalim Iddi Abdalla Farahani siku alipopata ajali. Mhe. Naibu Spika, tumekwenda pale na familia yake Hospitali ya Mnazi Mmoja mara unaambiwa rudi x-ray, mara hii imeshakamilika kafanye tena ya pili, hii peleka juu, mara unaambiwa ngoja kwanza weka juu. Ni kwamba vile uongozi wa ile hospitali haujui ule taratibu kwamba tukenda *x-ray* ni kwamba *x-ray* zote zimalizike, halafu ukiambiwa mpeleke katika wodi ndio suala hilo limalizike. Lakini zile taratibu hazionekani kama zinaeleweka vizuri.

Mhe. Naibu Spika, pia pana suala la upungufu ulo uliotajwa wa watendaji kwa sababu inafika pahala, juzi Dk. Sira alisema hapa kwamba wanaohudumia wagonjwa wanakuwa wanajazana pale. Hilo ni kweli lakini mara nyengine sisi tukiwapeleka wagonjwa tunatakiwa ubakie pale ili usaidie. Ni utaratibu wa hospitali ukenda kwamba madaktari na wahudumu wengine wachukue jukumu la kumuhudumia mgonjwa. Lakini mazoea katika hospitali zetu unaambiwa mgonjwa sasa hivi mpelekeni akapige *x-ray* nyinyi wenyewe mlompeleka ndio mnaopewa machera mumpeleke kule. Kwa hivyo, tutakuwa tunalaumu watu kama wanajazana, lakini

unapokuwa na mgonjwa ambaye yuko katika hali mbaya huwezi kulikwepa hili. Kwa hivyo, naomba Mhe. Naibu Spika, hili moja la *procedure* za hospitali liangaliwe vizuri.

Mhe. Naibu Spika, jengine pia Mhe. Waziri aendelee kuangalia suala la kukosekana kwa uaminifu kwa baadhi ya watendaji wa hospitali zetu. Unakwenda unatafuta dawa unaambiwa dawa hakuna, lakini ukitoa chochote basi mfanyakazi pale pale anakupatia dawa ile. Mhe. Naibu Spika, kuna tukio moja nafikiri Mhe. Waziri mwenyewe alipelekewa, nafikiri alilifuatilia akalichukulia hatua. Mhe. Naibu Spika, kuna muuguzi pale hospitali ambaye alikamatwa kuhusu suala hili, sijui mtu huyu alimchukulia hatua gani. Kwa hivyo, nasema hili bado linaendelea kuwa usumbufu kwa watu wengi naomba pia litazamwe.

Mhe. Spika, vile vile kuna kero nyengine kuna malalamiko kwamba katika sehemu za wazazi hasa ile sehemu ambapo mama tayari yuko katika hali ya kutaka kujifungua, huwa kuna wafanyakazi wanaume wanaingia kule na hili kina mama zetu wanalipigia kelele sana. Mhe. Naibu Spika, mimi nasema hili naomba walitupie macho ili kama tatizo hili lipo liweze kuondoka.

Mhe. Naibu Spika, nataka niipongeze sana hii hatua iliyotajwa katika ukurasa wa 14 wa kitabu kwa kuvikamilisha Kituo cha Afya cha Kwamtipura na Mpendae na kuvifikisha katika daraja la pili ili visaidie kupunguza msongamano katika hospitali kuu ya Mnazi Mmoja. Kwa muda mrefu sana tumekuwa tukijiuliza hili, kuwa lini serikali itaona umuhimu wa kuweka vituo katika baadhi ya maeneo mengine ya mji ili kupunguza msongamano katika hospitali kuu na kuweza kutibiwa katika maeneo hayo. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nataka nilipongeze sana.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo kuna masuala haya yamezungumzwa katika ukurasa wa 46 juu ya kuongezeka kwa maradhi haya yasiyo ya kuambukiza. Ametaja pale Kisukari, Saratani, Moyo na Kibofu cha Mkojo. Mhe. Naibu Spika, ni kweli

tunaoishi katika jamii sote tunajua kwamba maradhi haya siku hizi yamekuwa yanaongezeka sana katika nchi yetu. Kwa hivyo, hili nataka kulitilia mkazo kuwa kuna haja ya kufanya utafiti juu ya chanzo cha kuongezeka kwa maradhi haya.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo nataka kulizungumzia suala hili la saratani. Mhe. Naibu Spika, cha kuongezeka kwa maradhi haya.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo nataka kulizungumzia suala hili la saratani. Mhe. Naibu Spika, mimi nilibahatika kupeleka mgonjwa katika Hospitali ya *Ocean Road* Dar es Salaam alikuwa na tatizo la kensa. Mhe. Naibu Spika, ukenda pale Wazanzibari wanaokwenda kupata huduma hiyo ni wengi sana, na kusema kweli wanadhilika kwa sababu gharama zake za kwenda kuifuata ile huduma pale ni kubwa sana. Pale matibabu ni bure lakini ile dawa inayotumika pale inabidi uilipie.

Mimi nilipeleka wangu ile dawa ilikuwa inagharimu kama shilingi laki moja na elfu ishirini sijui sasa hivi inafika kiasi gani, huyu ndiye aliyeandikia kima kidogo sana cha dawa, mbali kama kila baada ya wiki tatu urudi inabidi uende halafu urudi tena Zanzibar. Kwa hivyo, kwa jumla unatumia pesa nyingi sana, mimi nakumbuka nilipomtibu wangu nimetumia si chini kwa ile *round* ya mwanzo kama milioni tano. Kwa hivyo, mfikirie mwananchi wa chini ambaye hamiliki hata mlo wake unamwambie ghafla amekutikana mgonjwa ana suala hili anaweza kumuhudumia vipi mgonjwa wake.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nasema hili lipewe umuhimu na nakumbuka Mhe. Rais katika hotuba zake nyingi amekuwa akisisitiza kwamba moja katika mambo ambayo anataka kuyapa kipaumbele ni kuona kwamba hospitali yetu inakuwa na kituo cha kutibu au kufanya uangalizi wa maradhi hayo. Kwa hivyo, naomba hili tulitazame sana tena kwa kina zaidi.

Mhe. Naibu Spika, katika jambo limenipa hudhuni sana katika zile changamoto ambazo amezitaja Mhe. Waziri mwenyewe ni suala

zima lile la bajeti ya ununuzi wa dawa. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba serikali au nchi yetu nzima dawa tunazotegemea imekuwa zile za kugaiwa na *DANIDA*. Pamoja na kuwa na bajeti ya bilioni mia sita na kumi na tatu, tunashinda kuipata 1.5 kukamilisha ununuzi wa mahitaji yetu ya madawa yote Wizara ya Afya itoe milioni 700 badala ya bilioni 1.5, yaani tumempa nusu ya mahitaji yake. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naweza kusema kuwa kipaumbele cha bajeti hii ni afya, lakini hata bilioni 1.5 na hapa kinachohitajika cha ziada ni kama milioni mia nane kukamilisha. Hivyo kwa nini tushindwe?

Mhe. Naibu Spika, hili naomba sana serikali na Waziri wa Fedha akija aambiwe hapa akatafute kifungu chochote ikiwa kile cha semina au safari za nje katika Wizara ya Fedha ili apunguze huko na aongeze hapa katika bajeti hii ya Wizara ya Afya ili huduma zile za madawa ya msingi ziweze kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kuna maeneo haya ambayo naomba ayatupie macho. Mhe. Naibu Spika, mimi ni tofauti na wenzangu, mimi napongeza sana uamuzi wa wizara hii kwa kutoa wito kwa wana siasa na wananchi kwa jumla kuacha kujenga vituo vya afya vya ziada. Moja katika tatizo letu Mhe. Naibu Spika, tunapenda kutanua majengo haya yakawa mengi, lakini kuyahudumia tunashindwa hata maskuli yalikuwa ndio hivyo hivyo. Chanzo kimoja cha kuporomoka kinakuwa ni hicho, unaongeza majengo lakini kuyahudumia huwezi. Kwa hivyo, mimi naomba wizara katika hili itoe agizo la kusimamisha ili kwanza hivi tulivyovijenga viimarishwe vipatiwe vifaa, vipatiwe huduma. Kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba kwa sasa hivi tulivyo ile *requirement* ya kwamba ndani ya kilomita tano pawe na kituo cha afya tumeshaifikia. Kwa hivyo, hebu tukamilishe hivi ambavyo tunavyo halafu ndio tujenge vyengine.

Mhe. Naibu Spika, pia naiomba wizara itupie macho suala la kuibuka kama uyoga kwa hospitali za watu binafsi. Je, vinakidhi mahitaji haya kwa sababu kama havikidhi mahitaji vinaweza vikaja

vikabadilika, badala ya kuwa vituo vya kutibu vikawa vituo vya kwenda kuwamaliza watu wetu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba hili walitazame sana ili kuweza kuboresha sekta afya na mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka nigusie kidogo tu suala hili la afya ya jamii.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini hata haya maradhi mengine utaambiwa kwamba yanaongezeka ya kisukari, kibofu cha mkojo, saratani pengine yanakuja kutokana na kutozingatia misingi ya afya ya jamii. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kitengo hiki kiimarishwe sana, ukaguzi lakini na huduma za msingi katika jamii mambo yakuwa na vyoo, kuweka usafi wa mazingira, mambo ya kukagua kupitia Bodi ya Chakula, Madawa na Vipodozi, kuhakikisha kwamba yale misingi mikuu ya kutunza afya zetu kwa kukagua vitu hivi inazingatiwa ili nchi yetu ijenge taifa lenye afya kama wanavyosema watu kuwa afya ni utajiri.

Mhe. Naibu Spika, tukifikia hatua hiyo itakuwa tumejenga taifa la wazalishaji watakaochangia katika kukuza uchumi wetu. Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema naiunga mkono bajeti hii mia kwa mia lakini zaidi nawaombea kama nilivyosema Wizara ya Fedha iangalie wapi ipunguze ili waongezee bajeti wao wapate tija ya msingi. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutufikisha hapa. Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii na nawashukuru Wizara ya Afya kwa kutuletea hotuba yao hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwapongeza madaktari na wafanyakazi wa Hospitali ya Makunduchi, ni nzuri na ni safi kwa mazingira yake. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hospitali hii katika Kamati yangu ya Ustawi wa Jamii tulipoitembelea tuliipa sifa na tukaipongeza sana kwa kufanya kazi vizuri. Mhe. Naibu Spika nitakuwa sio mwingi wa fadhila kwa kutoipongeza Hospitali yangu ya Jambiani kwa

wafanyakazi wake kwa kufanya kazi vizuri za kutoa huduma nzuri za kuwahudumia wananchi wake, naomba waongezewe ma-nurse.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wafanyakazi wanajitahidi kwa kutoa huduma zao vizuri hususan manesi na wauguzi ningeomba Wizara yako iwaongezee maslahi yawe mazuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa ongezeko la maradhi ya presha na sukari ni mengi je, Mhe. Waziri umefanya utafiti gani wa maradhi haya na ikiwa umeuona utafiti ya maradhi haya ningeomba utupe elimu ya kutuelimisha.

Mhe. Naibu Spika, tatizo la mama wajawazito hospitali ya Mnazi Mmoja tuliliona na tumeona linaongezeka wanapojifungua kwa kupasuliwa siku hadi siku na hapo zamani haikuwa hivyo, je ni tatizo gani ambalo linajitokeza ningeomba Mhe. Waziri atufafanulie.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wauguzi wako ambao wanafanya kazi ya unesi katika kazi zao huwa wanawatolea maneno yaliyokuwa sio mazuri wagonjwa, ningeomba wizara yako iwaone wafanyakazi hawa na kuwarekebishe watumie lugha nzuri wanapokuwa na wagonjwa hawa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi sina mengi ile naunga mkono hotuba hii mimi na wananchi wangu wa Wilaya ya Kusini mia juu ya mia. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia kidogo kuhusiana na bajeti hii ya Wizara ya Afya, kwanza namshukuru Alla kutupa uhai na uzima na kutupa toufiki ya kuzungumza.

Mhe. Naibu Spika, mimi napenda niikumbushe serikali kwamba katika miaka ya nyuma ya hivi karibuni kulipitishwa azimio kule Nigeria linaloitwa *Abuja declaration* ya kwamba nchi za Kiafrika katika kujenga afya za watu wao basi bajeti zao za afya zielekee

kwenye asilimia 15 ya bajeti za serikali, mimi nilikuwa katika baraza hili muda wa miaka mitano iliyopita na nilikuwa nikifuatilia sana kwa sababu nililazimika kuandika *speech* kama waziri kivuli. Bajeti ya Wizara ya Afya katika kipindi chote cha miaka mitano haikuzidi asilimia 6.5 ya bajeti ya serikali hivi sasa ndio inapungua zaidi katika hii.

Sasa naiomba sana serikali iangalie vigezo ambavyo wataalam waliokutana kule Abuja walivipendekeza kwa madhumuni maalum, katika kujenga taifa lenye afya na lenye uwezo wa kujituma afya ni kitu muhimu sana, kwa hivyo moja katika jambo ambalo wataalam wa bajeti wanalieleza ni namna serikali inavyotoa vipaumbele wakati wa kupanda bajeti zake. Inaonesha serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado haijaitambua sekta ya afya kwamba ni muhimu katika kupanga bajeti yake.

Mhe. Naibu Spika, ni muhimu serikali iangalie sana katika kugawa rasilimali siku moja kuna mtu alikwenda katika njia anatembea kwenda na safari zake akamkuta mtu kajishika tumbo na huku analia akamuuliza nini akamwambia naumwa na tumbo sana kwa sababu leo ya pili sijala mie, basi akampa pole pale akaendelea na safari yake. Katika sehemu nyengine njia hiyo hiyo akamkuta mtu kajishika tumbo vile vile analia akamuuliza nini akamwambia laa nimeshiba sana nimevimbiwa, sasa akamwambia kwa nini wewe una vyakula vingi hukumpa yule mwanzako mwenye njaa si nyote mngekuwa salama na tumbo lisingekuuma, kwa hivyo Serikali ikiwa haitoangalia sana wale walioshiba watakuja kuumwa na matumbo na wale wenye njaa wataumwa na matumbo na wote wataelekea hospitali kutafuta dawa na dawa zitakuwa na gharama.

Kwa hivyo tunaomba katika kugawa rasilimali waangalie sana suala hili sekta ya afya Mhe. Naibu Spika, imeowana na mambo matatu, Kwanza elimu ya afya, kabla mtu hujampa kinga au tiba lazima aelewe misingi ya afya kwa hivyo mimi napenda nisema kwamba naomba Wizara ya afya iangalie sana utaratibu wa kutoa elimu ya

afya kuanzia maskulini na katika maeneo mengine. Kwa sababu nyendo hizi zinasaidia sana katika kupunguza gharama.

Lakini la pili tuje kwanye kinga nashukurusana kwamba kuna miradi mingi inajitokeza ya kushughulikia kinga, lakini na sisi wizara ya afya tulitilie mkazo sana suala la kinga kwa sababu vile vile wataalam wengi wanakubaliana kwamba linapunguza gharama kubwa ya tiba, kama tutajikinga mimi nafikiri kama hivi sasa tuangalie kila mmoja kapungua gharama ya kununua dawa za malaria, kwa sababu ilikuwa ndani ya mwezi mmoja uwe na bajeti maalum ya kununua dawa za malaria.

Kwa sababu akishikwa mtoto mmoja mama nae anashika, na mdogo nae anashikwa, sasa fedha kama zile zinatumika katika kutoa lishe, kwa hivyo tukihakikisha kwamba tunafanya kile kitengo cha kufuatilia maradhi tukihakikisha kwamba maradhi haya tunayafuatilia na tunapata kinga yake kitapunguza gharama kubwa ya matibabu lakini tutapata ile *main power* ya kwenda kufanya kazi nyengine na kuweza kuzalisha.

Mhe. Naibu Spika, tuje kwenye tiba kama walivyosema wenzangu kunaanza kuonekana mabadiliko makubwa isipokuwa kama ili niliyoitaja mwanzo tu kurudishwa nyuma na bajeti ya serikali, lakini wizara yenyewe inaonyesha imechamka vizuri. Lakini mimi napenda kutoa maelezo haya kuna baadhi ya mambo ndani ya hospitali zetu iitwe Mnazi Mmoja, iitwe Chake-Chake au iitwe Makunduchi, lakini kuna mambo lazima kila hospitali yafanyike, kwanza usafi hii haihitaji hospitali iwe pahali fulani, pili kama hospitali sio vile vituo vya afya zinalaza wagonjwa. Sasa hebu tufanye utaratibu wa kujipatia angalau magodoro na mabetshit yetu.

Mhe. Naibu Spika, mabetshiti ya hospitali kikawaida yanaoshewa madawa kwa hivyo yako salama kuliko lile betshit ambalo litatoka pahali popote tu, lakini pia yatampa nafuu yule mgonjwa sasa wewe fikiria unapeleka mgonjwa tayari kuna watu wawili juu ya kitanda na yeye akalale hapo hapo kweli atapona huyo, sasa mimi nafikiria

bora tungalishusha magodoro chini kuliko kuweka watu wawili wawili au watatu. Kwa sababu yale ni matatizo kidogo tungetizama aina yengine nafikiri tukiteremsha magodoro chini kiongozi anayekuja pale anaona kwamba liko tatizo hapa, lakini siku anayotembelea Mhe. Rais wagonjwa wengine wakaambiwa upesi upesi nendeni kwenu hiyo inatokezea hospitali wasidanganye, akija Mhe. Rais waweke vile vile wagonjwa walivyo na ikiwa Waziri atakosa kazi sisi tutakuja kumtetea hapa kwamba kafanya kazi yake kwa sababu ndivyo wagonjwa walivyo Rais akawaone.

Lakini kuna suala baada ya kuweka usafi, vifaa, lakini suala la *staff* ikiwa wapo waonekane na kama hawapo vile vile waonekanane kwamba hawapo, hususani nyakati za usiku katika hospitali zetu kuna matatizo kidogo nyakati za usiku hebu tuliangalie vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye vitambulisho mara nyingi waswahili wanasema nazi mbovu harabu ya nzima, inaweza kuwa na madaktari au manesi wengi tu hawana matatizo ya maneno maneno lakini kuna wawili watatu kwa sababu ya hulka zao lakini hakuna vitambulisho hawavai kitu, kwa hivyo mimi nilikuwa napiga kelele sana ufike wakati wavalishwe vitambulisho mtu amjue huyu ni nani aliyemtukana. Lazima akivae kama kaenda hakuvaa kitambulisho chake ndio anayetukana huyo, maana yake sasa hivi hivi vitambulisho vimekuwa ni rahisi mno kuweza kupatikana kiasi kwamba hata ikifanyika semina ndogo tu unaweza kupewa kitambulisho cha siku moja ukaondoka ukenda zako sikwambii mfanyakazi.

Sasa Wizara ya afya kwa kuta tuliipigia kelele kama miaka mitatu hivi watayarishe vitambulisho vya wafanyakazi wao wavivae tukenda tena katika bajeti ijayo tutakuwa hatuwafahamu tena, labda vinatayarishwa vya dhahabu kama vinatayarishwa vya dhahabu basi inawezekana vikachukua miaka mingine mitano, lakini hivi hivi vya kawaida haiwezekani.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nimuulize Mhe. Waziri kuna mabadiliko gani katika maabara yaliyotokea hususan haya maabara ya uchunguzi wa kensa, kwa sababu siku za nyuma hapa kama walivyosema wenzangu hapa kwamba kensa inabidi uende Dar es Salaam, lakini tukapewa taarifa kwamba utaratibu upo na wengine wameshakwenda kusoma wa kuja kuchunguza zile damu na vile nyama za binaadamu ili ziweze kutizamwa kama zina kensa au laa. Jee, maabara hii sasa imeshafikia kiwango hicho au lini itafikia kiwango hicho, kwa sababu bila ya kuwa na nyenzo za uchunguzi sidhani kama tutaweza kuweka hicho kitengo cha kensa itakuwa hatuwezi kufikia huko.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri pamoja na *improvement* iliyotokea. Jengine tunapongeza juhudi za wizara za kupata mashine za kisasa ambazo ni za uchunguzi, mwaka 2006 mpaka 2007 ilikuwa ukienda kule Mnazi Mmoja kupiga *x-ray* ziko zile zile za zamani za kuchukuliwa filamu na nasikia siku zile kile kiwanda kilikuwa kimeshafungwa. Lakini nashukuru kwamba kuna *improvement* sasa kuna *X-ray* za kisasa na mashine nyingi, lakini suala langu liko hapa ni ufanisi wa kiasi gani uliopatikana wa kuweko *seat scan* na mashine hizo jambo ambalo lingelishindikana katika kipindi kilichopita, ili tukaiambia serikali kwamba kutokana na kuwepo kwa mashinde hizi pamoja na ughali lakini tumeweza kusaidia haya na haya mutupe fedha, pengine sisi hatui-*convince* hii serikali kwamba zile mashine zinasaidia zipo tu pale, lakini kama ingekuwa na tathmini inayofanywa pale kwamba tulipokuwa kwenye *x-ray machine* ya aina hizi tulikuwa na uwezo wa kufanya haya na haya, lakini tulipopata hizi sasa hivi tumekuwa na uwezo wa kufanya hili na hili limeongezeka kwa hivyo serikali isione tabu kutoa fedha za kuongezea ufadhili wa kununua zile mashine.

Mimi nimeingia wasi wasi kidogo kuna hii bodi ya ushauri ya hospitali binafsi kwa kazi zake inazozifanya kwa nini nikasema hivyo, ukifuatilia vyombo vya habari katika hospitali za Bara za binafsi karibuni kumetokezea wimbi kubwa la udanganyifu katika hospitali tena kuwadanganya wagonjwa, wanasema wana mashine

wanapima wala haipimi, walasijui dude gani wala halifanyi wanakwenda kule kudanganywa na mgonjwa ukimdanganya ina maana unamuua.

Je, bodi hii ya ushauri wa hospitali binafsi inafanya kazi za aina gani inashauri au inakagua vile vile hospitali na mashine zake kwa sababu karibuni Mhe. Naibu Spika, kumbe hili ni suala la ulimwengu mzima kwamba hizi hospitali za binafsi ni kwa ajili ya fedha za watu, kwa hivyo wanazipamba pamba kule alikuwa akizungumza mtaalam mmoja wa kiuchumi Saudi Arabia basi wamefanya mpaka suti za Hospitali, yaani mgonjwa anapewa nyumba pa kukaribisha wageni zote kwa kuzifanya kwamba utalipa pesa hii nah ii. Kwa hivyo hizi hospitali za binafsi zina *characteristic* ya kuchuma zaidi kuliko kutubu wakati mwengine hii ni mfumo wa ulimwengu mzima. Hii ni mpango wao kwa hivyo je nazo hizi zinachunguzwa ili watu wetu wasije kwenda kule tu lakini na wao wawe wanapata matibabu yanayostahiki.

Suala jengine ambalo ninalo nashukuru sana katika kitabu cha Mhe. Waziri ametaja ile *laboratory* yetu tuliyokuwa nayo kule *Pemba PHL* na kazi zake inazozifanya, mimi nauliza tu kwa sababu kuna tafiti nyengine ni za Wizara je tunaitumia vipi ile maabara ile na inatusaidia nini katika kuiona kwamba hizi tafiti zetu na sisi tunazifanyia pale ili kuijengea uwezo ile maabara na pia kupata uwezo mzuri zaidi wa kuona kwamba tunaweza matokeo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe bado dakika tano,

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakwenda kuna tatizo moja nililoliona humu katika kitabu, inawezekana Mhe. Waziri labda alisahahu karibuni hivi tuliuliza suala kuhusu hospitali ya wagonjwa wa akili kule Pemba, sasa katika kitabu mradi wa ugonjwa wa akili haikutaja ujenzi ule wa hospitali, lakini mimi nilikwenda kukipitia kitabu hiki cha bajeti ya serikali mwelekeo wa hali ya uchumi na mpango wa maendeleo wa mwaka 2011/2012. Ile hospitali jengo limo linaendelea sasa

nawauliza Mhe. Waziri kipi kilichokuwa *write,* jengo linaendelea katika eneo la Wete la ujenzi kama ilivyotajwa humu au halipo na haliendelei kama ilivyosahauliwa katika kitabu cha Mhe. Waziri. Kwa hivyo naomba ufafanuzi hapa kidogo kuhusu hili jengo la hospitali ya ugonjwa wa akili, kwa sababu wananchi wetu kwa kweli wanateseka sana na kama tujuavyo hali ya umasikini ilivyo na hali ya mambo ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, suala la mwisho mimi ninalozungumza ni kuiangalia hospitali ya Mnazi Mmoja kama ni hospitali ya rufaa, mimi nafikiria tungeliita hospitali ya rufaa kwa jina sio tatizo lakini tungelitizama *characteristic* za hospitali ya rufaa, hospitali ya rufaa ingakuwa bora isingelikuwa ile iliyozoeleka kwa sababu wagonjwa wengi wanaokwenda pale wanakwenda kwa mazoea. Sasa unajua ku- *transform* kitu na kukianzisha kitu ni vitu viwili tofauti, tunaweza kui *transform* ile kwamba ni hospitali ya rufaa lakini jamii haikubali kamba ile ni hospitali ya rufaa, kwa sababu wameizoea ni hospitali yao tokea huko tulikotoka sijui mwaka iliyoanzisha hiyo.

Halafu la pili hospitali ya rufaa inahitaji eneo la *expansion* na pale Mhe. Naibu Waziri juzi kakiri hapa kwamba haina eneo la utanuzi wa hospitali.

Lakini la tatu ni kwamba tuna madaktari ambao ni mabingwa ulimwenguni wanataka kuja kutusaidia kwa magonjwa haya ambayo yanatusumbua hapa, pengine kinachozuilikana ni kwa sababu hapana *feasibility* zilizoanzishwa. Sasa mimi naomba kwa *long time program* ya Zanzibar hebu tutizame hatuwezi kuanzisha hospitali ya rufaa ambayo mgonjwa hawezi kwenda kule wa kawaida mpaka apelekwe, kwa sababu hospitali ya Mnazi Mmoja hata ukimwabia ya rufaa mgonjwa wa kawaida atakwenda tu ameshaizoweya ile wewe ukiweka bububu yeye atakuja Mnazi Mmoja, ukiweka Mlandege atakuja Mnazi Mmoja, Ukiwaka Mazizini atakuja Mnazi Mmoja. Hebu tuangalieni hakuna njia ya kujenga hospitali ya rufaa ambayo mgonjwa hatokwenda isipokuwa kwa kupelekwa kwa cheti.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja na nimalizie hapa ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika mimi kilio changu kiko pale pale kwenye *I.C.U* hiki ni kitengo muhimu sana kwa binaadam nasema tuangalie nini maana ya *I.C.U,* mtu akishafikishwa pale ni *fifty fifty* ni akhera au duniani, hii inaonekana Wizara ya Afya haijawa *serious* tusidanganyane kitengo kimeharibika si chini ya miaka mitatu na kuendelea hivi sasa na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na hizi *cost* zake tunazopea ni kubwa sana na sisi tumeshajaribu kufuatilia, zimetokea kampuni mbili hapa kujitokeza na hakuna chochote kilichojibiwa kuhusu *I.C.U* kampuni hizo mbili tayari zimejenga *I. C. U* Morogoro na hospitali ya Mbeya.

Leo *I.C.U* ile atokee kiongozi wetu muhimu apate mtihani pale usiku ndege haiwezi kutua tutampeleka wapi, itabidi apelekwe *I.C.U* wakati *I.C.U* yenyewe haipo pana bodi tu ya *I.C.U* sanamu tu lililokuwepo kule ndani, leo *I.C.U* kuna hatari bora mgonjwa wa Mnazi Mmoja nje kuliko kumpeleka mle mna mitungi ya gesi hatari tupu isiyosemeka, kuna mikokoteni sijui virikwama vidogo vidogo vimewekewa michupa ya gesi kweli ndio *I.C.U* leo karibu miaka mitatu tokea kuharibika hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na serikali.

Vifaa vya *I.C.U* kuna vifaa vyengine vidogo vidogo tu vinashindwa kuangaliwa kuna *A.C* mbili ni bei gani zinafika labda ni milioni moja laki nane au milioni mbili zimeshinda, leo madirisha yanafunguliwa nje kule upepo utoke nje kwenye miti ni *I.C.U* kweli ile, *A.C* zimekaa tu mle ndani wanachezea joto. Mitungi ya gesi ile ikija kuripuka tutawafanya nini wale wagonjwa jamani, leo miaka mitatu tunarudia nyimbo hii hii imekuwa ni wimbo wa taifa kuhusu *I.C.U* hakuna jitihada zozote zilizochukuliwa.

AC kiasi gani wananchi wanaumia bure kwa kitu gani hili ni jukumu wajumbe wenzangu tunalibeba kwa Mwenyezi Mungu sio kitu cha

kufanyia masihara tutakwenda kuulizwa. Mhe. Naibu Spika, tumechukua dhima za watu sisi kwenye migongo ya watu huu wadhifa leo upo kesho haupo huu, tunaringia pumzi tu za kuazima leo ya mwisho *I.C.U* mgonjwa anachekiwa pumzi vipi huwezi kuamini, anawekwa mdomo hapa kwenye pua zinatoka pumzi au hazitoki ni *I.C.U* kweli hiyo.

Mhe. Naibu Spika, tuache hapo tuje sehemu ya wazazi jana Mhe. Waziri namwambia unayo taarifa katika hospitali yako kuna baadhi ya wagonjwa wanakosa huduma za upasuaji, wanakwenda pale utapoa kwa ufadhili wake na ukarimu wake yule mtu mwenyezi Mungu amsaidie anakopesha vitu leo anataka kupigwa vita mtu yule ndio tunakwenda mbele au tunarudi nyuma, ndio maendeleo tunayotafuta kweli haya. Tuwa wawazi mtu kama yule anajitolea kwa uchungu wa nchi hii Utapoa pale usiku saa sita au saa tano anakopesha vifaa ili ukapate huduma leo anapigwa vita mtu yule si tutauana hivi hivi. Serikali ni wananchi na wananchi ndio serikali.

Lao mzazi ana uchungu anakwenda pale anataka kuzalishwa anaambiwa laki moja na nusu atazaa kabla hiyo mamba yake haijawa, kwa sababu ni mzigo juu ya mzigo unapiga tu. Mhe. Waziri najua wizara umepewa muda mfupi sana na maendeleo yako tumeyaona.

Nimpe pole kidogo ile wizara ngumu na Mwenyezi Mungu atakusaidia. Jitihada zako tumeziona lakini tuwe *serious* hichi kitengo cha *ICU* amepewa juzi tu leo miaka mitatu na zaidi *ICU* haijafanya kazi. Serikali itahitaji shilingi ngapi kushughulikia suala hili sio tunaweka rehani maisha yetu. Mhe. Naibu Spika, mimi nataka maelezo kuhusu *ICU*.

Mhe. Naibu Spika, kuna kilio chengine cha *theatre* kitanda cha *orthopaedic* hakipo, kilio *sanction machine* kila wodi inataka mashine yake, *ventilator machine* hamna, dawa za *anesthesia* hamna. La mwisho kabisa zile nguo za wafanyakazi hamna, gozi hamna, nyuzi za kuyeyushia hazipo. Kuna mashine tayari

zimeshaharibika mle sijui mmechukua hatua gani mpaka sasa hivi. Mhe. Naibu Spika, hii nazungumza kwa uchungu sana kuhusu kitengo cha *ICU*, hili ni jukumu letu.

Mhe. Naibu Spika, jengine maposho ya madaktari, madaktari tunawaumiza maposho yao hawapewi na hichi ndio chanzo kikubwa wizara ikawa haifanyi vizuri. Huyo mtoto akitokea wa kwanza skuli basi hupata zawadi. Ni mtihani mkubwa huu Mwenyezi Mungu atusalimu salama.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Fedha mwenyewe hayupo hapa, bajeti wanayopewa wizara hii kwa kweli wanaonewa hawa watu pesa hazikidhi, bajeti ni ndogo. Tusiwatupie mizigo tu wakati uwezo wao wa kufanya kazi unaonekana. Mhe. Naibu Spika, naomba bajeti yao iangaliwe tena kwa jicho la huruma. Tunataka kuifanya hospitali ya rufaa huku mambo chungu nzima hamna tutafika kweli huku, hesabu inaanza moja haiwezi kuanza tatu.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho nimshauri Mhe. Waziri kwamba hawa waandishi wa habari wanapokuja wakataka taarifa muwape msiwazuie hii inakusaidieni nyinyi, sio mtoe taarifa wewe, Naibu Waziri na Katibu Mkuu. Mhe. Naibu Spika, Waswahili wanasema "Mficha uchi hazai". Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa na mimi kutoa mchango wangu mdogo katika Wizara ya Afya ambayo ni wizara muhimu sana kwa binadamu wote.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu mimi utakuwa wa kijumla jumla. Kwanza kabisa napenda nimpongeze Mhe. Waziri kwa juhudi zake alizonazo na pia niungane na wenzangu nimpe pole kwa majukumu mazito ambayo wamepewa.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuondoa tatizo la maji katika hospitali ya Mnazi Mmoja ingawa kuna changamoto nyingi zinazotukabili.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda niishukuru sana Wizara ya Afya kutokana na mishahara ya wafanyakazi iliyoibiwa katika hospitali ya Micheweni na nilipiga kelele sana kipindi kilichopita, leo hii nathubutu kusema kama wafanyakazi wote hawadai tena wamelipwa zile pesa zao.

Mhe. Naibu Spika, jengine napenda niipongeze *NGO's* ya Mama Shadya kwa kutujengea wodi ya wazazi kule Micheweni. Mhe. Naibu Spika, katika kipindi hichi tulichonacho Wizara ya Afya imekusudia kuongeza *facility* katika wizara yake. Pamoja na bajeti finyu ambayo ni ndogo kama wanavyosema wenzangu lakini kwa umuhimu wa wizara hii basi ilikuwa bajeti yake iwe ni kubwa kwa sababu imebeba jamii ya watu wote wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika kunyanyua huduma za matibabu katika hospitali zetu wizara imekusudia kuzifanya hospitali zile za cottage kuwa ni hospitali maalum ya Vitongoji, Kivunge, Micheweni pamoja na hospitali iliyopo Makunduchi.

Mhe. Naibu Spika, katika kukuza hili namuomba Mhe. Waziri katika hospitali ile ya Micheweni pamoja na kuazimia kukuza iwe ni hospitali ya kuhudumia wilaya nzima. Kwanza napenda nimuarifu kama hivi sasa sio hospitali ya wilaya lakini inahudumia karibu wilaya mbili maana kuna watu wanaotoka Wilaya ya Wete wanakuja Micheweni. Kwa hiyo, shukurani zangu za dhati ni kukusudia kuifanya kama sasa iwe ni hospitali ya wilaya.

Sasa Mhe. Naibu Spika, sasa namuomba Mhe. Waziri azingatie mambo yafuatayo. Mhe. Naibu Spika, kwanza ile hospitali ni ndogo sana, wodi za kulaza wagonjwa ni ndogo sana. Kipindi kilichopita nilizungumza sana kuhusu wodi ya wazazi na wodi ya kulaza wagonjwa wa kawaida lakini hili tatizo la wodi ya wazazi sasa limeondoka. Lakini nilitoa mfano wodi ya kulaza wanaume ina vitanda vitano na hii hospitali tunataka kuifanya ya wilaya. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kabla ya hizo huduma nyengine basi

aiangalie kwa jicho la rehema ili tuongezewe ile hospitali kwa ajili ya kuondoa yale matatizo madogo madogo yaliyopo.

Mhe. Naibu Spika, jengine kule kuna mashine ya *x-ray* nzima lakini kwa bahati mbaya haina daktari, daktari mpaka atoke sijui Mkoani au wapi tena aje kwa wiki mara moja au pengine wiki mbili hajapita. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kwa sababu ile *x-ray* iliwekwa kwa ajili ya kuwapunguzia safari ndefu wananchi wa Micheweni afanye kila jitihada inayowezekana tupate daktari ili ile azma ya serikali ifanikiwe.

Mhe. Naibu Spika, jengine pale kilijengwa chumba kwa ajili ya kutumia kwa operesheni japo ndogo ndogo, lakini hakiwezi kuwa chumba cha operesheni kama hakina zana. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako atuone kama safari tunayotoka Micheweni kwenda Wete au Chake-Chake ni ndefu sana. Ili kile chumba kiwe kweli chumba cha upasuaji basi tupate hizo zana ambazo zitakuwa zinafanya hiyo kazi na pia tupatiwe daktari wa kuhudumia hizo huduma zilizopo.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine Mhe. Waziri alizungumza kwamba Micheweni walifanya utafiti na kugundua kama Wilaya ya Micheweni watu wengi wana ugonjwa wa vikope. Namshukuru sana Mhe. Waziri kufanya hivyo na akajua. Sasa namuuliza Mhe. Waziri baada ya kufanya utafiti na kugundua serikali imejipanga vipi ili kufanya jitihada ya kupunguza huo ugonjwa wa vikope na ikiwezekana kuutokomeza kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kipindi kilichopita cha bajeti nilimueleza Mhe. Waziri kama Micheweni kuna tatizo la wagonjwa wa kupooza viungo vya miguu na ikawa watu hawawezi kutembea na huu ugonjwa nilimwambia kama unachukua sehemu kubwa ya wananchi wa Micheweni na ni sugu. Mhe. Naibu Spika, bahati nzuri Mhe. Waziri alithibitisha kama ni kweli na akasema hapa Maziwang'ombe kulikuwa na watu wengi walikuwa wanadai hizi fimbo za miguu.

Lakini nikamwambia mheshimiwa naomba kupitia kwako serikali ifanye utafiti na igundue ni tatizo gani na ikishagundua itoe elimu kwa wananchi ili kuinusuru hii hali. Kwa bahati nzuri au bahati mbaya mpaka leo hii ninavyozungumza katika vitabu hivi vya bajeti sijaona kama kulifanywa huo utafiti na kugundua kuna tatizo gani. Kwa hiyo, pia nalirudisha tena kumuomba Mhe. Waziri suala hili kama alikuwa hajalifanyia utafiti basi atwambie na kama ameshalifanyia utafiti atueleze hapa tujue kuna tatizo gani.

Kwa sababu nilimueleza Mhe. Waziri kuna ugonjwa wa miguu na ugonjwa wa uziwi, watu walio wengi wanakuwa viziwi, sasa tunataka tujue tatizo gani linalosababisha. Kwa bahati mbaya Mhe. Naibu Spika, mpaka ninavyozungumza sijapata hiyo taarifa na bado hali ya watu kupopoteka miguu bado ipo. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri afanye utafiti wa kuwasaidia wananchi wa Micheweni kuondokana na tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mchango wangu utakuwa wa kijumla jumla nazungumza sasa kuhusu huduma zinazotolewa na madaktari wetu. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri asichelewe kupita mara kwa mara katika hospitali zetu kama alivyoanza mapema asichoke njiani kwa sababu madaktari wana kazi nzito ya kuwahudumia wananchi wetu. Lakini kuna madaktari wengine kama alivyosema mwenzangu kauli zao si nzuri kwa watu wanaowahudumia. Kwa sababu inafika saa tatu daktari hajenda kazini, ukenda ukizungumza nae daktari anakwambia mwite Juma Duni aje akuhudumie.

Mhe. Naibu Spika, kauli zinazotolewa na watendaji wako si nzuri, kwa hiyo nakuomba uwaelimishe watendaji kama wao wako pale kwa ajili ya kuwahudumia wananchi. Haki ya Mungu tusifanye masihara. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri bado ana kazi nzito apite awaelimishe zaidi watu wake kwa sababu kupita kwake basi wanakuwa na hofu zaidi. Mfano ulio dhahiri kwamba siku mnayosema leo mwende hospitali na wakishakuwa na uhakika kama leo Mhe. Waziri anakuja basi hospitali hata kama ina uchafu gani

itasafishwa mpaka itarambwa ukifika ukaikute safi kabisa. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kila mara awe na jitihada ya kupita na kuwahimiza ili ile hali ikiwa nzuri ni sifa kwako, ni sifa kwa serikali yetu na ni sifa kwa wizara nzima.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki niendelee sana namuomba Mhe. Waziri anipe majibu hayo atakapokuja na namuuliza kwa roho safi kabisa, atakaponijibu nitafurahi sana kupata majibu mazuri. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii, naunga mkono wizara hii naiomba serikali ione kama hii ni wizara mama inahudumia wananchi wote. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako hili nikiwa na afya njema. Pia nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote jinsi walivyoichambua bajeti yao hii vizuri. Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 32 katika kutekeleza ahadi za Rais wa Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2010/2015 Wizara ya Afya imekusudia kuziimarisha hospitali nyingi za Zanzibar ikiwemo Chake-Chake, Wete na Mkoani.

Mhe. Naibu Spika, mbali na malengo mazuri ya Wizara ya Afya naomba niseme hali ya hospitali ya Wete inahitaji kuimarishwa sana. Mhe. Naibu Spika, hivi sasa mbali na jitihada za wafanyakazi lakini bado hali ya madaktari inahitaji kufanyiwa marekebisho na inakatisha tamaa.

Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu sasa hospitali ya Wete ina tatizo la daktari wa upasuaji. Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na ahadi je, Mhe. Waziri ahadi hii imefikia wapi ya kututafutia daktari wa upasuaji pale hospitali ya Wete.

Lakini Mhe. Naibu Spika, ukosefu wa madaktari katika hospitali ya Wete basi rufaa kupeleka wagonjwa Chake Chake na Mkoani

litakuwa ni zoezi la kawaida. Mhe. Naibu Spika, pia naomba niseme katika hospitali hiyo hiyo ya Wete ina tatizo kubwa la madaktari bingwa wa maradhi ya kike ambalo linaleta usumbufu mkubwa kwa wagonjwa wa mkoa mzima wa kaskazini.

Mhe. Naibu Spika, tukiendelea kukosa madaktari wa kutosha katika hospitali ya Wete basi namuomba Mhe. Waziri afanye mambo muhimu yafuatayo. Aidha, aongeze *ambulance* kwa wingi na mafuta ya kutosha ili zitumike kwa kukimbizia wagonjwa kutoka hospitali ya Wete kwenda Chake Chake na Mkoani. Mafuta hayo wasije wakachangishwa wagonjwa kwa sababu hali zao ni duni hawana maisha mazuri wala hawana uwezo wa kulipia michango ya magari. Au kama si hivyo ajitahidi Mhe. Waziri atutafutie madaktari bingwa atuletee ndani ya hospitali ile ya Wete.

Mhe. Naibu Spika, naomba niipongeze serikali kwa kutupatia mashine nzuri mpya na ya kisasa ya kusafishia meno katika hospitali ya Wete. Kwa sababu ni muhimu sana kuweka mashine kama ile ambayo si lazima watu kila wakati wang'oe meno, wakati mwengine linakuwa jino lina athari ndogo tu linaweza kurekebishwa. Tatizo lililopo Mhe. Naibu Spika, mashine ile imefungwa lakini haikufungwa vizuri kwa maana hiyo haifanyi kazi kwa sasa. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie ni lini atatuletea wataalam wa kuifunga mashine ile pale ili wagonjwa wa hospitali ya Wete na Mkoa mzima wa Kaskazini wapate tiba nzuri ya meno bila ya kusafiri kwenda eneo jengine.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza ahadi hizo hizo za Rais pamoja na bajeti hii pia yamo maelezo ya kuziimarisha hospitali zilizoko mijini na vijijini. Mbali na kuwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu alisema hapa kwamba hospitali za vijiji ziimarishwe zilizopo kuliko kujengwa nyengine. Lakini pia namuomba Mhe. Waziri atazame na ajali zile nguvu za wananchi pale ambapo wananchi wenyewe walijitahidi kujenga kituo cha afya na kuangalia ule umbali uliopo kati ya kile kituo walichokijenga wananchi na huko wanakokwenda hospitali.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe mfano, kuna kijiji cha Mjini Kiuyu Wilaya ya Wete Jimbo la Ole, masafa yake kutoka Mjini Kiuyu mpaka kwenda kwenye hospitali nyengine kwenye kituo cha afya ni masafa marefu yanafika kama kilomita nne na nusu au zaidi.

Mbali na hayo miundombinu yao ni mibaya sana kutoka Mjini Kiuyu kuja barabarani hasa mtu akiwa katika hali ngumu ya maradhi. Mhe. Naibu Spika, nataka niseme katika maeneo ya watu wanaoishi baharini au karibu na pwani mara nyingi yanatokezea matatizo ya maradhi ya miripuko. Mhe. Naibu Spika, pahala kama pale ipo haja ya serikali kuona zile nguvu za wananchi walizojitegemea wenyewe wakajenga kituo kile mpaka kufikia kuezeka, sasa hivi wakiendeleze serikali kupitia wizara kwa kuwasaidia wananchi wa kijiji kile ili wapate tiba nzuri bila ya kuhangaika.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kwenye usafi katika mahospitali yetu ingawaje wenzangu wameshasema lakini kila mmoja anasema kwa vile alivyoona mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, nataka Mhe. Waziri akubaliane nami kwamba usafi ndani ya mahospitali yetu ni wa msimu, utakaposikia anakuja Waziri au Rais hospitali zitasafishwa, mashuka yatawekwa vizuri na madaktari wote watakuwa wanakaa pale makini sana kwa kusubiri hilo. Lakini pindi ikiwa hakuna hilo mgonjwa ananyanyuka anawekwa mgonjwa mwengine zaidi ya wagonjwa watatu na shuka lile haliondoshwi pale sasa baada ya kujitibu unaongeza maradhi.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri akubaliane na mimi kama mgonjwa ni sawa sawa na mtoto anahitaji kuhudumiwa, kubembelezwa katika hali zote. Baadhi ya madaktari au wahudumu ndani ya mahospitali yetu kauli zao si nzuri, wana kauli mbaya, wanawadhalilisha wagonjwa, inafikia hali mgonjwa bado anaumwa lakini hutamani arudi nyumbani kuliko kubakia pale hospitali akitafuta matibabu.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri awapitie watendaji wake kwa muda maalum na awape semina maalum ya jinsi ya kuwalea wagonjwa, kwani na wao pia ni miongoni mwa binadamu na iko siku na wao wataumwa na wataona ile raha ya kuumwa na kulazwa pale hospitali. Mhe. Naibu Spika, hakuna hata mmoja anayependa kuondoka nyumbani kwake na kwenda kulala hospitali, hata mtu akenda hospitali jua tayari ana tatizo na ndio maana anakwenda pale akapate huduma.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine naomba Mhe. Waziri atufahamishe kwa sababu unakwenda kupeleka mgonjwa wako hospitali unaandikiwa dawa dirishani ukifika dirishani hakuna dawa utaambiwa wewe dawa hizi nenda duka fulani. Je, duka fulani hilo ulilioambiwa uende dawa zile wamezipata wapi kama hazitoki pale pale hospitali. Hili linaonesha wazi kama ule uaminifu wa madaktari wetu baadhi si mzuri, wanachukua dawa zetu zile wanafungua *pharmacy* zao zinakwenda kupelekwa kule na ndio maana ukifika unaambiwa kanunue dawa.

Mhe. Naibu Spika, tatizo hili linaongezeka na linaongeza matatizo kwa sababu sasa hivi wananchi wamechukulia uzoefu wa kuwa hospitali hakuna dawa, kila mtu anajinunulia dawa tu haendi hospitali na dawa zile baada ya kutibu maradhi anajiongezea maradhi mapya.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri aliangalie hili kwa makini na alichukulie hatua ili kuwapa afya njema wananchi wetu wa Zanzibar kwa jumla. Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia mimi na wananchi wangu wa Wilaya ya Wete naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu na naomba uniachie dakika 30 nimalize kwa sababu ni Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake.

Mhe. Naibu Spika, si tatizo mwakilishi kuunga mkono hoja ya serikali, lakini inakuwa tatizo pale ambapo hapana sababu ya kuunga mkono. Sasa kabla ya kuendelea mbele naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa jinsi alivyotumia masaa mawili na kidogo kwa ajili ya kuwasilisha hotuba yake. Kwa kweli amemudu kwamba afya yake nzuri labda ni kwa sababu ya huduma nzuri za Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, mimi mtazamo wangu wa kwanza nataka nizungumzie hotuba ya Mhe. Rais ambayo aliitoa humu ndani ya Baraza tarehe 11 Novemba, 2010. Mhe. Naibu Spika, katika hotuba hiyo Mhe. Rais alituainishia mambo kama matano juu ya huduma ya afya. La kwanza Mhe. Rais kwenye hotuba ile alizungumzia kuyaenzi na kuyalinda malengo ya Mapinduzi kwenye sera ya Afya. Lakini pili akazungumzia jukumu la serikali hii iliopo juu ya kulinda na kuendeleza sera hiyo ya Afya kwa maana ya matibabu bure. Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Rais akazungumzia hali ya ushirikishwaji wananchi katika huduma hizi za afya.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais pia hakusahau na alisema serikali hii itasimamia kwa nguvu zote uimarishaji wa hospitali ya Mnazi Mmoja kwa maana ya kuipandisha hadhi kuwa hospitali ya rufaa. Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Rais alizungumzia hali ya kuanzisha kitengo maalum kwa ajili ya maradhi ya figo, moyo na saratani kwa Wazanzibari ili wasiende nje kutibiwa na kuharibu fedha za serikali.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kwa upande wa hotuba ya Mhe. Rais kwa upande wa afya alizungumzia haja ya wahudumu wa afya kuwa na lugha nzuri kwa wagonjwa. Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako nataka nianzie hapa ambapo wenzangu wamezungumzia. Wazanzibari wengi wanalalamika kwamba baadhi ya madaktari na wauguzi wanakuwa na lugha isiyopendeza. Tumekuwa tukipata kesi hizo na kwa kweli zinasikitisha. Lakini nimejaribu kutafuta *hansard* mbali mbali nimeona kwamba labda hii ndio taaluma ya afya ilivyo, pengine hii lugha ya jeuri kidogo, lugha ya kuchomekea ndio taaluma yao sina hakika.

Mhe. Naibu Spika, nikiangalia majibu ya Naibu Waziri Dk. Sira Ubwa Mamboya kila mwakilishi aliyejaribu kuuliza suala la afya majibu yake yalikuwa hayapendezi kwa mujibu wa *hansard* nilizonazo. Sasa napata tabu kuona kwamba hii ndio taaluma ya afya ilivyo ukiwa na shida ya kiafya ujibiwe jeuri, hivi ndivyo taaluma ya afya inavyoelekeza. Mhe. Naibu Spika, unapojibiwa kwa sentensi moja tu hatufanyi, hatwendi, nadhani hayo si majibu ya wagonjwa wala wanasiasa.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye mapato. Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana Wizara ya Fedha iliwatengea Wizara ya Afya kukusanya shilingi bilioni 52. Kwa busara za kamati na uongozi wa wizara hii tukaona kwamba haiwezekani Wizara ya Afya ichangie shilingi bilioni 52 na tukawashauri watafute vianzio vyengine, wakatuonesha wao Wizara ya Afya kwamba wana uwezo wa kuchangia shilingi bilioni 532. Ni kusema kwamba kumbe uwezo wa kukusanya fedha nyingi Wizara ya Afya upo. Mhe. Naibu Spika, swali langu la kwanza miaka yote hiyo kwa nini fedha hizi hazikukusanywa, kama zinakusanywa zinapelekwa wapi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mtazamo wangu maadam wizara imekiri kwamba ina uwezo wa kukusanya shilingi bilioni 532 hakuna sababu ya hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa chafu, kukosa gozi, kukosa nguo za wafanyakazi. Mhe. Naibu Spika, kwa mtazamo wangu pana tatizo la menejimenti ya hospitali ya Mnazi Mmoja na lazima kama serikali yenye uwazi tuambieni ukweli. Mhe. Naibu Spika, mimi ninapozungumza huwa nazungumza kwa nia safi, nikiondoka hapa sina tatizo na mtu. Lakini wajibu wangu kama mwakilishi niliyekula kiapo ni lazima niseme ukweli, atakayeona kuwa ni makero sawa yeye na makero yake. Mimi ukifanya vizuri nitakusifu, ukiharibu nitakuambia ndio *principle* yangu sio nyengine.

Kwa hivyo, kwa nini tukusanye milioni 537, lakini leo tunaona wafanyakazi hawana nguo, nguo inafuliwa ikauke ndio mtu avae, haiwezekani ni lazima nidhamu ya kazi isimamiwe. Hii ni kauka nikuvae Mhe. Naibu Spika, na mimi sioni sababu hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye mchanganuo wa mapato ambao Mhe. Waziri ametuomba tumuidhinishie bilioni 10.7 kama ni kazi za kawaida na mishahara na *other charges*, hakuna tatizo. Tutamuidhinishia kwa sababu ni lazima wafanyakazi wapate maslahi yao. Lakini amesahau kutuomba kumuidhinishia pesa za miradi ya maendeleo kutoka kwa wahisani na huu ndio mtazamo hasa wa Wizara ya Afya. Unapowahoji kuhusu pesa ya malaria, anakuambia wafadhili, pesa ya ukimwi wafadhili na *any public money* ambayo inaingia humo ni *public money* ya wananchi.

Hapa Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hakutuambia kwamba tumuidhinishie shilingi ngapi kutoka kwa wafadhili, kwa msimamo ule wa kuomba hii fedha kumbe si yetu, hii fedha ni yetu. Fedha inayoingia hapa ni fedha ya wananchi na ni fedha ya halali ni lazima Baraza la Wawakilishi waidhinishe na ni lazima *PAC* wakaguwe. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hapa hakutuomba, namkumbusha kwamba utuombe ukifika. Ulituomba bilioni 2.5 za serikali, lakini hukutuomba bilioni 11.2 za wahisani ambazo ni lazima Baraza la Wawakilishi waidhinishe na lazima uzitumie na sisi tuzikaguwe.

Mhe. Naibu Spika, la kusikitisha kwenye miradi ya maendeleo ambayo kwenye hotuba ya Rais na hotuba ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo afya ni sekta moja muhimu, lakini imetengewa asilimia 18 tu ya fedha za ndani, asilimia 82 ni wahisani kutoka nje. Halafu tuambiwe kwamba hizi sekta zimepewa kipaumbele, ni kudanganyana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Spika, hatuwezi kutenga asilimia 18 tukajisifu kwamba tumewekeza katika sekta ya afya. Ni jambo ambalo haliwezekani na ni wazi kwamba watendaji wetu wa Wizara ya Afya hawatofanikiwa

hata hatua moja. Mhe. Naibu Spika, ushahidi wa hilo, mwaka jana hapa kwenye huduma ya afya ya akili walitengewa milioni 90, lakini hata shilingi moja haikuingia. Watu wanaandika bajeti kiasi cha kuwafurahisha wafadhili tu, lakini haina ukweli na bajeti kama hiyo ni bajeti ambayo ni ngumu sana na ni bajeti ya kusikitisha.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema nia ya serikali katika sekta ya afya zaidi ni nadharia, haijaamua kuwekeza kwenye sekta ya afya. Mhe. Naibu Spika, kwa mfano, mradi wa ukimwi peke yake umetengewa milioni 4.3 kwa maana ya asilimia 32, hiyo ni wizara ya afya tu. Wakati kuna ukimwi wizara zote, kuna Tume ya Ukimwi ambayo tumeianzisha kwa kazi hii. Mradi mmoja tu wa ukimwi Wizara ya Afya umetengewa bilioni 4.3 asilimia 32 ya bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Afya. Lakini tumetengea asilimia 11 ya miradi ya watoto mama na waja wazito kwa asilimia 11, ni kiasi gani serikali hii ilivyokuwa haijatilia umuhimu suala la mama waja wazito na hata wanawake.

Mhe. Naibu Spika, kwa utafiti wangu wa haraka haraka, mradi wowote ambao unatoa pesa za moja kwa moja, ndio mradi ambao watendaji wetu wanaupa kipaumbele. Mhe. Naibu Spika, sioni sababu ya kwamba ikiwa kila wizara ina kifungu cha ukimwi, baadae kuna Tume ya Ukimwi, kuna *NGO's* na bado tuendelee kukusanya mapesa kwa ajili ya kutoa elimu ya ukimwi. Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari hao watapewa hiyo elimu na watu wangapi, ikiwa kila mtu anazungumzia ukimwi tu, hiyo elimu itakuwa mara ngapi tunapewa. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ushauri wangu fedha hizo zipunguzwe na zipelekwe Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhudumia huduma za mama na watoto pamoja na *ICU*.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu na bohari ya madawa zimetengewa asilimia 3 na bahati mbaya mafunzo mwenzangu huyu kapewa milioni 2. Mhe. Naibu Spika, ni mzaha, ni vichekesho na haiwezekani. Mhe. Naibu Spika, kwa mtazamo wangu Wizara ya Afya haijawa tayari. Bohari kuu ya madawa walihitaji milioni 1.5 ya madawa, lakini wametengewa

milioni 700. kwa mujibu wa maelezo yao wenyewe Mhe. Waziri wa Afya anasema hapa kwamba ili aijenge *ICU* basi apate milioni 800, kwa maana hiyo tutowe mapungufu ya bilioni 1.5 kwa ajili ya bohari, pamoja na *ICU*.

Sasa nikiangalia Mhe. Naibu Spika, mimi kama mimi, Wizara ya Fedha tu safari za ndani, mafunzo na safari za nje kwa wizara nzima ni bilioni 5.5 kwa wizara ya fedha tu peke yake, ndio mtuambie kwamba hamna uwezo wa kutengeneza *ICU* milioni 800 haiwezekani. Tuambieni ukweli kwamba hamna nia ya kutengeneza *ICU* na kwa maana hiyo mnakusudia watu wafe. Ninavyojua mimi kila wizara ina fungu la safari, sasa kwa nini muweke bilioni 5.5 kwa safari tu Wizara ya Fedha na baadae muwaambie watu hatuna uwezo, nchi changa. Sio kweli hamjakuwa na nia dhabiti ya kuwatetea wananchi kwa mujibu wa ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kwa msingi huo, mimi nisingekuwa mwakilishi kama sio mchango wa babu Juma, maana yake Baraza Kuu ndio lililonipitisha. Kwa hivyo, naheshimu sana msaada wake na uongozi wake, lakini kwa hapa sina *solution*, hapa siwezi kupitisha bajeti hii, kwa sababu nimewashuhudia wananchi wangu wengi wakifa kwa sababu ya *ICU* tu ambayo inahitaji milioni 800 na ukichunguza ni chini ya hapo. Kwa hivyo, mtuambie kwa nini hamtaki kutenga fedha hizo. Bahati mbaya Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hayupo hapa, lakini ni lazima atuambie, kwa nini atenge safari za mafunzo Wizara ya Fedha bilioni 5.5 halafu akose kutoa milioni 800 za *ICU* haiwezekani kabisa.

Vyenginevyo Mhe. Naibu Spika, mnatuambia kuwa kazi ya serikali hii ni kutembea na kuzunguka. Lakini haiwezekani kuwa watu wana shida, wanakufa kwa maradhi, halafu watu watembee tu waende nchi za nje, kwenda kufanya nini. Hii sio nchi ya watu 22, hii ni nchi ya watu milioni 1,200,000. Kwa hivyo hakuna haja ya watu kutembea kiwa ni wagonjwa, lazima Mnazo Mmoja ishughulikiwe tupate majibu. Vyenginevyo hatuwezi kupitisha bajeti hii. Mhe. Naibu Spika, najua nikizungumza safari za nje watu wataumia, hata

mimi nataka nitembee lakini ni lazima tuangalie afya na maslahi ya watu.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kusema kwamba Malaysia nilipelekwa na *CAG*, sikupelekwa na Wizara ya Fedha. Mhe. Naibu Spika, ninachosema fungu la hazina la Wizara ya Fedha pamoja na fungu zima la Wizara ya Fedha wenyewe limechukua zaidi ya asilimia 32. Kwa hivyo wizara ya fedha peke yake ina asilimia 32 ya bajeti kuu ya serikali. Lakini Wizara ya Afya ina asilimia 4, haiwezekani. Mnafanya nini ikiwa watu ni wagonjwa au maiti mnafanya nini. Mhe. Naibu Spika, mimi naona kadiri tutakavyozungumzia hapa Mnazi Mmoja basi utatokwa na machozi, ni lazima tukubaliane kwamba hii ni bajeti ambayo tunadanganyana, hamna lengo la kutengeneza maslahi ya wananchi kiafya.

Mhe. Naibu Spika, sina haja ya kuzungumza sana. Nasema tu kwamba siungi mkono hotuba hii mpaka nipewe majibu sahihi, ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nikazungumza machache sana katika Wizara hii ya Afya. Mhe. Naibu Spika, nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, na watendaji wake wote kwa kazi ngumu tuliyowapa kwa kuwahudumia wananchi wote wa Zanzibar, kwa sababu naamini wizara hii haikubakisha mtu, kwa sababu kwa kuwa Wazanzibari wote naamini huwa wanaumwa, basi huduma yao au afueni yao wataipata kupitia wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nianze moja kwa moja kwa kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa nia yake ya kutaka kuboresha huduma za afya Zanzibar. Hili kama alivyosema mchangiaji aliyepita kwamba alituthibitishia wakati alipokuja kulizindua Baraza letu la Wawakilishi. Alieleza nia ya serikali kuboresha huduma za afya, kuweka hospitali za wilaya, lakini vile vile na hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kuifanya kuwa ya rufaa.

Mhe. Naibu Spika, nikianza na hospitali ya Mnazi Mmoja wajumbe wenzangu wamelisemea sana na mimi sio vibaya nikaweza kusemea kwa sababu tunahitaji tupate huduma bora. Mimi naanza moja kwa moja katika suala zima la utumishi wa umma. Mhe. Naibu Spika, bado tuna kazi pevu sana tena tuna kazi pevu kwa sababu, katika suala zima la utawala bora na utumishi wa umma, ukiwacha maslahi ya wafanyakazi lakini vile vile na uwajibikaji. Tunashukuru sana serikali yetu imefanya semina hivi karibuni, kwa ngazi ya mawaziri, makatibu wakuu, wakurugenzi. Nadhani iko haja kusogeza taaluma hii na kwa watendaji wetu, bado Mhe. Naibu Spika, suala la lugha kwa madaktari wetu au wahudumu wetu bado ni mtihani.

Mhe. Naibu Spika, nadhani labda tushauri katika hiki Chuo chetu cha Afya hapa Mbweni kuwe kuna somo maalum la namna ya kumuhudumia mgonjwa yaani ile kumuhenga henga na kumbembeleza. Mwenzangu Mhe. Farida Amour alizungumza vizuri sana katika suala zima la kumuenga enga mgonjwa. Mgonjwa anakuwa kama mtoto mdogo na mtoto mdogo anapolilia kitu unatakiwa ujaribu kumpa lugha ya kuweza kuridhika, hata kama kile kitu hajakipata, lakini apate ile lugha itakayoweza kumridhisha.

Mhe. Naibu Spika, bado vijana wetu au wahudumu wetu katika suala zima la kuwahudumia wagonjwa wetu bado katika suala la lugha tuna mtihani mkubwa. Kwa hivyo, katika suala zima la utumishi wa umma na Mhe. Waziri kaunda wizara safari hii maalum ya utumishi wa umma, sasa utumishi wa umma na utawala bora kila mmoja kuwajibika katika nafasi yake. Kwa hivyo, suala hili sio la leo ni suala la muda mrefu, limeshaota mizizi au limeshafanya ukoko, kwa hivyo nadhani sasa hivi tunahitaji tupate pauro na reki kwa ajili ya kukokoa huu ukoko.

Nawaomba sana waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wajitahidi sana, wafanye muda angalau wa kupitia pitia angalau kidogo wale watendaji wetu wanaweza wakaona kwamba kumbe haya tunayoyafanya kumbe viongozi wetu wanatupitia na wanaweza

wakayajua. Kwa hivyo, tunaomba sana suala la lugha katika hospitali yetu hasa ya Mnazi Mmoja ambayo ndio tunalaza wagonjwa wengi kidogo hili tulifanyie marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nizungumze katika baadhi ya maeneo kwenye hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Nimejaribu kuangalia katika hivi viambatanisho ambavyo tumepewa kuwa humu kuna makusanyo ambayo katika kiambatanisho c, kinasema

Kifungu 24

Kiambatisho c

"makadirio ya makusanyo ya mapato ya mwaka 2011/2012". Kifungu 24 Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, hapa wizara inategemea kukusanya karibu milioni 537. Sasa fedha hizi tulitegemea, kama kweli zitaweza kukusanywa fedha hizi, basi mambo mengi madogo madogo kama walivyosema wenzangu, kama vile magozi wanavyoita wataalamu, lakini kwa sisi waswahili tunaita mabendeji na mambo mengine madogo madogo sio ya kuweza kuyakosa. Lakini vitu hivi mara nyingi vinakosekana katika hospitali yetu. Sasa hizi fedha zinapokusanywa sijui zinatumika kwa matumizi gani.

Vile vile nikiangalia kiambatanisho hiki Mhe. Naibu Spika, kuna suala zima katika kifungu 14.5.001 malipo ya *X-Ray*. Hapa inasema mwaka 2009/2010 kuna deshi, yaani hakuna maelezo yoyote kilichokusanywa. Mwaka 2010/2011 kuna deshi hakuna kilichokusanywa mpaka mapato halisi Julai/Aprili 2011 pia kuna deshi na katika asilimia kuna ziro, ina maana kulikuwa hakukusanywi kitu. Lakini katika *X-Ray* tunalipa, sasa haya mapato mbona hayakuainishwa hapa. Sasa pengine sikufahamu vizuri Mhe. Waziri aje kunisaidia wamekusudia kitu gani.

Mhe. Naibu Spika, kwenye mapendekezo na makadirio ya mwaka 2011/2012 kuna makadirio ya makusanyo milioni 15 katika *X-Ray*,

sasa haya makadirio ya milioni 15 wakati huku nyuma hakikuainishwa kilichokusanywa, ina maana kulikuwa hakuna pesa zilizokuwa zikikusanywa na kama zilikusanywa kwa nini zisioneshwe katika maandishi haya. Mimi hapa nilikuwa nahitaji ufafanuzi.

Vile vile katika kifungu 14.5.001 kiambatanisho hiki hiki c kinasema kwamba

Kifungu 14.5.001

"mapato mengineyo".

Haya mapato mengineyo tunajua kuna haya waliyosema wenzangu sijui ya malipo ya kitanda, ambapo Naibu Waziri alituambia sio kitanda sijui mambo mengine. Inaonesha haya ni makusanyo mengine mengi. Hapa tumeambiwa kwamba tunategemea kukusanya milioni 35, lakini huku katika miaka 2009/2010 hakikuoneshwa kitu chochote. Sasa hapa nilikuwa namuomba Mhe. Waziri akija anipe maelezo.

Vile vile nakuja katika suala la *ICU*. Mhe. Naibu Spika, mimi Mhe. Waziri ni rafiki yangu sana *JD*, Mhe. *JD* wenyewe wanawake huko mitaani wanamwita *JD*, sijui kama jina hili analisikia au vipi, kama analikubali na mimi rafiki yangu *JD*. Lakini Naibu Waziri ni swahib wangu mkubwa sana, lakini inaonesha waziri hajafanya jitihada. Ninasema hajafanya jitihada kwa kitengo cha *ICU*. Kwa sababu sisi tunasikia mitaani.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina jirani yangu mmoja aliwahi kusema siku moja. Kulikuwa na mzazi wake alikuwa amelazwa pale, akasema kwa kweli hiyo *ICU* yenyewe wala hakuna chochote anapigwa hayo mafeni tu, tena anamuambia rafiki yake pale mama watoto wangu, anamuambia bora ningekuja kumuweka hapo ukumbini kwako, hilo feni angalau kidogo pengine angekuwa anapata upepo kuliko huko *ICU*. Sasa mimi nikamwambia hapana,

hii inaonesha nyinyi hamjui mambo ya udaktari kule ndio anapata huduma. Lakini jana baada ya kupata jawabu kuwa *ICU* haifanyi kazi ndio nikazivuta zile kumbukumbu zangu nikasema alaa! Kumbe kule *ICU* hakuna kitu du! Mhe. Naibu Spika, hapa bado hatujawa tayari. Hapa nitamuomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atowe kauli ya serikali. Mhe. Waziri suala la *ICU* ni aibu kutegemea wafadhili waje kututengenezea chumba cha *ICU* na ukiangalia pesa zenyewe ziko wapi.

Mhe. Naibu Spika, jana tumejaribu kuzungumza kwenye bajeti ya Waziri wa Katiba na Sheria, kuna fedha zimetengwa kule katika fungu la Wizara ya Fedha kwa ajili ya utengenezaji wa majengo. Muhimu kujenga afisi ya Wizara ya Katiba na Sheria hiyo hiyo, fedha tunazo tumetenga katika fungu la serikali, lakini tumeshindwa kutenga fedha kwa ajili ya *ICU*. Mhe. Naibu Spika, hapa sote tumeletwa na wananchi na wananchi watatuona waheshimiwa wao hatuna maana pesa mbili, kwamba juzi tumepitisha maslahi bora ya wafanyakazi, wizara ya utumishi wa umma, sio kuwafurahia watumishi wa serikali wanapokuwa wazima tu, wanapokuwa wabovu mtu amepatwa na tatizo la kwenda *ICU*. Mhe. Mjumbe mwenzangu kawasemea viongozi wakuu, suala la *ICU* tusiwaangalie viongozi wakuu peke yao ni wananchi wote, *ICU* kumbe chumba ni kitupu. Kwa hapa tunataka kauli ya serikali vyenginevyo bajeti hii hatuipitishi wala hatuipitishi. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niseme tatizo letu waafrika tumezowea kusaidiwa. Hili neno wafadhili limeshatuharibu sisi akili zetu. Kuna fedha za msamaha wa madeni, kuna fedha za *MMDRA*, sijui kama *MDRE* au *MDRA* watajua wenyewe mawaziri. Lakini fedha hizo ni pesa za msamaha wa madeni, serikali zetu zimesamehewa na sisi Zanzibar tumo, tumeshanunua vitu vingi kumbe *ICU* mbovu, ina maana hatukuweka kipaumbele. Mhe. Naibu Spika, fedha zipo, mimi naamini katika fedha za msamaha wa madeni hatuna haja ya kusubiri wafadhili, wafadhili wameshatusamehe madeni hivyo fedha zipo. Mimi nikitoa mifano mingine iliyokuweko hai mtaniona labda siishi kusema.

Mhe. Naibu Spika, tunaweza kununua vitu ambavyo pengine tulikuwa hatuna haja ya kuvinunua kwa wakati huu. Juzi tumenunua magari mangapi mapya ya mawaziri, hayapungui kama saba au nane au kumi tukashindwa kutengeneza *ICU*. Ndio maana nikasema Mhe. Makamo wa Rais atakuja kutoa kauli tu, lakini waziri mwenyewe kashindwa kujenga hoja serikalini, milioni hizi 800 kwa ajili ya *ICU* kama unajenga hoja utaambiwa hili kata na hili kata tuweke *ICU*. Mhe. Naibu Spika, tunataka kauli ya serikali katika suala zima la kujenga *ICU*, vyenginevyo hapa patakuwa hapatoshi. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, namalizia naona unanitizama sana. Mhe. Naibu Spika, sitaki niwe mwizi wa fadhila, nashukuru sana kauli ya Mhe. Rais kwamba hospitali ya Kwamtipura wataimaliza, nawashukuru sana. Kwa kweli nawapongeza sana na madaktari wanaofanyakazi katika kituo cha afya cha Kwamtipura kwa kazi nzuri sana wanayoifanya.

Mwisho nataka niipongeze sana wizara kwa mradi wa majaribio katika hospitali ya Makunduchi. Mhe. Naibu Spika, kama hii *pilot project* inayofanywa na wizara sasa hivi kwa hospitali ya Makunduchi. Juzi mwenzangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub yeye ni mtu wa Kusini huko, alisifu sana, nimejaribu kufuatilia na Naibu Waziri ametupa majibu mazuri sana, akatuambia kwamba wanategemea kuwa sio zile huduma kutolewa bure pale, lakini wanategemea kuwafuata mpaka wagonjwa majumbani kwao. Mhe. Naibu Spika, kama tutafika hapo, basi tutakuwa tunawatendea haki sana wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, tunapokwenda nchi za wenzetu tunaona mtu anaumwa na tumbo nyumbani kwake, anapiga simu tu aah! Naumwa na tumbo basi *ambulance* imeshafika. Kwa hivyo, mimi nadhani hii *pilot project* ambayo inafanywa kwa hospitali ya Makunduchi naamini kama itaenea katika maeneo mengine, *Wallah* tutashukuru sana. Lakini haya yote yanataka nini kwanza tuwajenge imani

madaktari wetu, tuwajenge imani manesi wetu na wahudumu wetu kwa ajili ya kuweza kutoa huduma zilizo bora.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, kuna malipo ya madaktari. Kuna madaktari sasa hivi wamekuja wapo hospitali ya Mnazi Mmoja, katika ile kujaribu kuiangalia na kuifanya hospitali yetu iwe hospitali ya rufaa, lakini malipo yao ni madogo sana. Leo malipo ya daktari ni shilingi 2,000/=, hawa madaktari tunao wasomesha watakimbia wote, uzalendo utawashinda. Leo madaktari hawa kwa bahati nzuri mshahara wao unalipwa na SMT. Lakini sisi ukiangalia yale malipo yake, mtu pengine anakaa Mpendae na mwengine anakaa Nyarugusu, hakuna hata usafiri. Yale malipo maana yake ni kumwita daktari kuja kumuhudumia mgonjwa, ndio tunatengeneza hospitali ya rufaa, mpaka asubiri daladala usafiri hawana.

Mimi nadhani tungeandaa utaratibu mzuri, tungeandaa utaratibu wa usafiri maalum hasa kwa hawa madaktari wetu ambao watakuwa wanaitwa, ambao wao watakuwa ni kazi yao kwa sababu ya wito maalum ili waweze kuwa na usafiri wa haraka haraka. Naomba sana hawa madaktari ambao wapo ambao mshahara wao wanalipwa kutoka SMT na ambao wapo katika majaribio, mimi nadhani tungewatengeneza hawa. Kwa sababu hawa wameshaanza kulalamika, wakilalamika hawa wengine watakuja, wakikimbia hawa basi hao wengine hawatokuja. Ile dhana ya kuifanya hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa rufaa kwa kweli tutaikosa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli muda wako ni mdogo na tutaomba bajeti ya mwakani katika wizara kama hizi zinazohudumia wananchi angalau tupate siku tatu, lakini siku moja na nusu unazungumza hujamaliza unaambiwa basi, haya maneno mengine nitakwenda kuyasema wapi, nikayaseme Kwamtipura.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache nakushukuru sana, lakini nilikuwa naomba tupate kauli ya serikali na kauli yenyewe ni kwamba serikali itatoa fedha kutoka fungu la mfuko mkuu wa

serikali kwa ajili ya kujenga *ICU*, nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataallah aliyetuwezesha tukafika hapa salama na Inshaallah Mwenyezi Mungu atujaalie tumalize shughuli zetu salama.

Nakushukuru na wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi. Pia nawashukuru wote Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa kitabu chao cha hotuba ya bajeti kilichosomwa jana kilichopangika vizuri, kwa kuwa na nia safi kabisa ya kuweza kuwashughulikia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, mengi yameshasemwa nitazungumza kidogo tu. Mimi nitazungumzia katika hospitali ya Chake-Chake na maeneo mengine kidogo. Mhe. Naibu Spika, tuna matatizo katika hospitali. Katika mahospitali kuna matatizo na tukisema tusionekane kwamba tunaonea, lakini hatuonei ni wajibu wetu kusema, kwa sababu mwanadamu atakapoumwa na atakapokwenda pale hospitali anaomba apate mtu ili aweze kupata maliwaza. Lakini Mhe. Naibu Spika, tunafika pale madaktari wetu hawana habari ya wagonjwa wala kitu chochote.

Mhe. Naibu Spika, neno hilo nilikuja kulizungumza hapa katika mwaka 2008 kule katika Baraza kongwe tulikoondoka. Mara hii limejitokeza, juzi tu wala sijafika wiki, nafsi yangu mimi limefika mtoto wangu ameumwa, baada ya kuumwa mtoto yule akenda hospitali ya Kiuyu kwa muda wa siku tatu dawa zile alizopewa kutumia ikawa hali kwa siku ya tatu ikabidi akapoteza fahamu. Mtoto yule alichukuliwa akapelewa hospitali ya Chake-Chake ambayo iko katikati watu wa maeneo yote tunaitumia. Kufika pale akaandikiwa cheti mtoto akapelekwa kwa daktari, daktari akawaambia kamnunulieni dawa kisha muondoke naye. Daktari yule akaulizwa na yule dada yake aliyempeleka, huyu sisi kama ingekuwa nyumbani tunamuweza tusingemleta hapa. Jibu alilolitowa

yule daktari alimuambia kama una haja ya kitanda nenda kamuweke. Je, Mhe. Naibu Spika, hilo ni jawabu zuri, hilo sio jawabu zuri.

Mimi nilipigiwa simu pale kwa ajili ya kutuma pesa za dawa nikatuma akaenda kufuatwa daktari mwengine mwenye imani yake nyumbani kuja kumshughulikia mtoto yule, akanunuliwa ma-*drip*, madawa na akachomwa sindao na ilipofika muda wa saa 8 nikapigiwa siku tayari keshazinduka. Sasa hawa madaktari sisi tukizungumza sio kama tunazungumza hapa kuwa tunawaonea, tunazungumza tuna matatizo.

Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Chake-Chake mimi nimeshaiwekea mikwara hapa toka yuko Mhe. Mugheir kwa matatizo haya haya. Nilikwenda kulikuwa kuna mtoto kaanguka kwenye Mbungo. Nafika nasikia kelele kwenye hodi ya wanaume, mtoto roho inamkauka. Nikauliza ana nini nikaambiwa huyu mtoto ameanguka toka muda wa saa 5, daktari anasema kaumia sana, asipewe chai wala asipewe maji na gari haipo kapeleka maiti. Namwambia kapeleka maiti mbona gari nimeikuta imewekwa Michakaeni dereva huko wapi, alipopigiwa simu, simu imefungwa kwa kweli tulikaa pale mpaka saa 11:00 basi niliwaambia mtieni kwenye gari yangu kwa ajili ya kukimbilia hospitali.

Mhe. Naibu Spika, baadaye akapigiwa simu tena na alipokuja basi akaiweka gari na kutafuta kichochoro, kwa sababu ile gari tayari mimi nilikuwa nishaiona, basi akajibabaisha huku na kule, kwa sababu yule mwanamke ameshaambiwa achangie mafuta na tayari ameshakwenda Kangagani kwa miguu, amerudi kwako Mbuzini na ameshapewa fedha kwa ajili ya kuchangia mafuta kwenye *Ambulance*. Mhe. Naibu Spika, mtoto saa 11:00 bado hajapelekwa hospitali na hayo nilizungumza ni matatizo ambayo tunao.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, aweze kukaa nao watu hawa na kuweza kuzungumza nao, kwa sababu hatutaki tuwataje majina, isipokuwa jambo la ukweli basi tutalisema. *(Makofi)*

Vile vile suala jengine kuhusu Hospitali ya Chake-Chake na Mhe. Farida Amour Mohammed alisema suala la usafi na mimi mwenye yameshanikuta. Kwa mfano, mimi nilikwenda pale nilikuwa nikiumwa na pale hapana Chumba cha Waheshimiwa wala nani, yaani tunachanganywa sote pale.

Mhe. Naibu Spika, shuka linalowekwa kwenye kitanda basi wagonjwa wanne wameshaondoka na wewe unawekwa pale, kwa sababu kila mmoja na maradhi yake, sasa ikabidi nikachukuliwe mashuka kwa mtoto wangu na kuja kuekewa kitandani. Kwa hivyo, hata haya mashuka kukosha na kubadilisha baada ya kuondoka mgonjwa mmoja na kuwekwa mwengine hawawezi. Sasa tunapouliza wala hawana wanalolisema. Kwa maana hiyo, ikiwa hawana mahitaji, yaani mahitaji yao ni madogo basi hawa wapewe maposho yao na wazidishiwe ili wapate kuwashughulikia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nashukuru sana nilipata kusafiri kwenda nje. Kwa kweli wenzetu wanawashughulikia wagonjwa, kwa sababu daktari ndio kazi yake kushughulikia mgonjwa na amesomea fani ya Udaktari na asipokwenda mgonjwa yeye hana mshahara.

Kwa mfano, inapofika saa 11:00 nyote mnaletewa maji ya moto vitandani na kusafishwa na kupiga misuwaki mpaka wakati anapokuja daktari, basi nyote tayari mumeshasafishwa na baadaye kuna maziwa mnapewa kwa ajili ya kunywa, yaani saa 2:00 nyote mnakuja kutolewa kwa viti hata kama mtu anayo miguu yake kamili anaweza kutembea, basi viti vinaletwa na kuchukuliwa mgonjwa kwa ajili ya kwenda kukoshwa, kwa kweli anapembejea. Lakini leo unakwenda kukaa kitako unaumwa majibu unayoyapata si mazuri utakuwa hujengeki kiimani. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia kwenye hospitali zetu tujue kuna wagonjwa ambao hawajiwezi. Kwa mfano, mimi kila siku Hospitali ya Chake-Chake ipo *centre* na nilipo mimi, basi nikienda safari zangu ikiwa nipo Chake-Chake lazima niingie hospitali, basi hukuta matatizo

mengine sana, kama vile watu wanasongomana, mhudumu hayupo na ikifika saa 4:00 ameshatoka na atarejea saa 8:00.

Vile vile kile Chumba cha Kuhifadhia Maiti kiko nje ya watu wanaosubiri huduma, kwa kweli chumba hiki kipo pahala pabaya sana. Sasa hospitali nzima ile haikuonekana sehemu ya kutengwa Chumba cha Kuhifadhiwa Maiti mpaka kikawekwa njiani wanapokaa watu na wala si vizuri.

Pia nimelikuta jengine la watu ambao hawajiwezi. Mhe. Naibu Spika, daktari yuko mbali na mtu aliyefika pale na kigari chake na wala hawezi kumkuta mhudumu anakaa vipi na pengine ameletwa na mtoto hajui chochote na wala hajui aulize vipi na pengine huyu mwenye kupelekwa hajui kuuliza kitu chochote.

Sasa akitizama pale watu wanaingia na kutoka na inafika mpaka saa 6:00 yeye amekaa na mimi nimeshawakuta mara mbili na niliwauliza na kunieleza kwamba bado mahitaji kutoka kwa daktari hawajapata. Kutokana na hali hiyo, nianze kufuatilia daktari na mpaka nafika kumpata daktari ambaye hahusiki na maradhi yale, lakini angalau aweze kumhudumia mtu yule.

Kwa hivyo, tunaomba madaktari kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hayupo ambaye hatokuwa mlemavu, kwani sote ni walemavu watarajiwa. Kwa maana hiyo, watu hawa tuweze kuwajali na kuweza kuwapembejea na wala sio sisi tuweze kufanyakazi zetu kwa kuwa tunaweza kwenda na kurudi na yule yupo juani, ikiwa kuna mvua inamnyeshea hapo na wala kuna sehemu ya kupita na kigari chake, hivyo yeye amekaa na wala aelekee wapi. Kwa hiyo, naomba sana hospitali zote kwamba tuonekane. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Kitendo cha Watu Wenye Ulemavu katika Hospitali ya Chake-Chake na wakati uliopita niliomba tokea Mhe. Naibu Waziri Mhe. Sultani Moh'd Mugheir mpaka akawa Waziri wa Afya tunaona suala hilo. Kwa kweli sisi pale hakuna hata sehemu ya chumba cha nafasi kwa ajili ya watu kufanyakazi zao. Mhe. Naibu

Spika, ukienda pale utaona imani kwa sababu watoto wanakandwa viungo juani tena uwanjani wanatiwa mapiopio.

Kwa hivyo, tunaomba tuonekane wala hawa si vizuri majengo kama yale hayana sehemu kama vile vyumba viwili kwa ajili ya walemavu na kuonesha kuwathamini wale watu. Kwa mfano, kuna mashine nyingi sana ambazo tumepata kutoka kwa wafadhili kwa ajili ya kufanyia mazoezi, kutengenezea viatu soli, mashine za kutembelea pamoja na mambo mengine, yaani zimo na zimekaa zinaharibika na wala sijui huo mwaka tutakapopata sehemu ya kuziweka kama zitafanyakazi, kwa sababu zimeshafanya kutu. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, tunaomba tuonekane Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, basi tunakulilia kilio chetu utakapokuja ufike Hospitali ya Chake-Chake na tuonane na mimi nipigiwe simu tu basi nitakuja. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu kuhusu Daktari wa Viungo. Kwa kweli madaktari wote wametukimbia. Lakini tunaye Madaktari wawili ambao ni Dkt. Shaibu na Dkt. Khamis, hawa Mwenyezi Mungu amewajaalia wanasoma lakini wameganda pale kwa ajili ya kutuhudumia na hawa hawapati semina wala matembezi ama mafunzo, yaani hawendi pahala popote kwa sababu gani.

Mhe. Naibu Spika, hawa wanahudumia wagonjwa ambao ni walemavu kama wagonjwa wengine. Kwa hivyo, tunaomba Wizara ya Afya kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba ituone kwa jicho la huruma watu hawa na wao waonekane. *(Makofi)*

Vile vile hapo Hospitali ya Chake-Chake siku nilikwenda kuna chumba kimoja nyuma ya sehemu ya wagonjwa wa kifua, kuhusu watu wenye matatizo ya akili. Kwa kweli pale nilikwenda na nikamkuta mama mmoja analia mtoto wake ameletwa pale amefungwa kamba na ndani yumo mwengine milango inavunjwa zogo tu.

Sasa nikamuuliza, akaniambia mtoto wangu amechanganyikiwa, lakini nilipomwita daktari na kumuuliza, aliniambia Mhe. Raya Suleiman Hamad, aliniambia Mheshimiwa hawa watoto wengi tunaowapata wanachanganyikiwa na akili kwa sababu ya bangi. Mhe. Naibu Spika, ameniambia wagonjwa ni wengi sana kutokana na bangi.

Kwa hivyo, tunaomba kuwe na wito maalum kuhusu hawa watu na matangazo kwa ajili ya kuachana na mambo kama haya, kwa sababu mtu anajitafutia maradhi mwenyewe. Kwa mfano, kuna yale ambayo Mwenyezi Mungu amejaalia, sasa wao wakawa na mambo ambayo hayafai kuyatumia. Kwa maana hiyo, tunaomba tuwe *serious* na watoto wetu na wizara nayo itoe wito kamili juu ya watoto hawa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ninashukuru sana kwa sababu nilikuwa nikiumwa na ninamshukuru Waziri wa Afya aliyeondoka Mhe. Sultani Moh'd Mugheir, Katibu wake Mkuu Dkt. Saleh Jidawi, Waziri Kiongozi pamoja na Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi walinisimamia vizuri na nilipata safari kwa ajili ya kwenda kufanyiwa matibabu na baadaye nikarudi salama. Kwa hivyo, natoa shukurani zangu za dhati kwa watu hawa wote. *(Makofi)*

Lakini juzi tu nilikwenda hospitali na nilikereka sana na wala sikusema, kwa sababu nilikwenda pale kwa ajili ya kufanyiwa *registration* na kuweza kuniangalia, kwani tokea niliporudi huwa nikipiga picha za *X-Ray* na ile ya mwanzo ilirushwa kule na baadaye niliambiwa kila baada ya muda nipige zile *X-Ray*. Sasa nilipofika pale niliambiwa *X-Ray* labda nikapige Hospitali ya Al-Rahma, kwani kule juu ile mashine haifanyikazi na mapato yataingia sehemu nyengine. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, nilishindwa kupata kwenye *lift* kwa ajili ya kwenda juu na kuweza kupiga *X-Ray*. Kwa hivyo, tunaomba

kwamba huduma nyengine ziekwe karibu na wanajamii, ili waweze kutumia kwa urahisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, basi nikatoka nikenda kupiga *X-Ray* na tayari nikarudi pale, yaani muda wa siku tatu natembea nazo mkono Daktari wa Viungo hayupo. Sasa nikauliza Dkt. Rashid ambaye ni daktari wangu wa zamani, niliambiwa Mhe. Raya Dkt. Rashid amekwenda Masomoni labda uende Lugalo. Kwa hivyo, ni vyema wataalamu wetu wenye fani hizi tuwawezeshe wasitukimbie, kwa sababu nilikaa muda wa siku tatu sikumkuta daktari.

Pamoja na hayo, namshukuru Mwenyezi Mungu akanijaalia nikapata mtu mwenye huruma na kuweza kunielekeza basi nikaweza kuonana na daktari na nilipofika aliweza kuniangalia na namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba alinishughulikia vizuri nashukuru.

Kwa hivyo, naomba wawe *serious* watu wa hospitali na tukisema tusiambiwe kwamba tunawaonea, lakini mafao yao wapewe, ili waweze kujenga imani juu ya wananchi wa nchi hii, kwa sababu wagonjwa ni wengi na sote tunaumwa. *(Makofi)*

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika na wala sina mengi, nashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipata nafasi ya kuweza kuchangia Hotuba ya Waziri wa Afya, ambayo ni nzuri yenye maelezo ya kutosha na kila mtu amefahamu kilicho ndani. Vile vile nachukua nafasi hii kumshukuru Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote katika kuweza kuichangia Hotuba hii ya Waziri ambayo imetoa muelekeo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ugawaji mzuri au ugawaji wa kutosheleza kwa bajeti hii na kuweka *ceiling* ya mawizara yote.

Pamoja na hayo, tunashukuru kwamba chini ya Wizara ya Afya idara imepata *sub votes* ukilinganisha na wizara nyengine. Lakini hakuna zuri ambalo halina kasoro. Kwa hivyo, tunasema kwamba ugawaji wa rasilimali fedha lina mapungufu tena mapungufu yenyewe ni makubwa, ambayo yanahitaji kupatiwa ufumbuzi wa haraka, kulingana na idadi ya wakaazi wa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Mkemia Mkuu Zanzibar ametengewa shilingi 45,100,000/= na Mkemia wa Pemba ametengewa shilingi 7,396,000/=. Wakati mwaka uliopita 2010/2011 alitengezwa shilingi 16,841,000/=. Kwa hivyo, utaiona hiyo kasoro mwaka 2010/2011 shilingi 16,841,000/= na kipindi hiki ni shilingi 7,396,000/=. Mhe. Naibu Spika, ni hivyo na Idara ya Mipango Sera na Utafiti na hali kadhalika Idara ya Uendeshaji na Utumishi mambo yamekuwa ni hivyo hivyo.

Mhe. Naibu Spika, miradi ya Maendeleo Wizara ya Afya Unguja imetengewa jumla ya shilingi bilioni 2 na milioni 5, lakini kwa Pemba Mhe. Naibu Spika, hakuna mradi uliopangiwa kwa fedha za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, katika hayo ambayo kasoro zimejitokeza ni kwenye Huduma za Mama Wajawazito na Watoto hawakutengewa kitu pamoja na ujenzi wa madarasa mawili ya *Medical School* pia nao hawakutekewa kitu. Kwa hivyo, miradi yote ni muhimu kwa jamii, basi haikuwezekana kupatikana mradi wa maendeleo kwa jamii.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, wizara katika mgao wa fedha za mradi wa maendeleo ione kwamba hizo fedha ni kwa ajili ya maendeleo ya Pemba pamoja na Unguja pia. *(Makofi)*

Lakini jambo ambalo lililokuwa ni muhimu zaidi ni kwamba wizara ilikuwa ioneshe mradi wa Unguja na Pemba angalau kwa asilimia ngapi kwa Pemba na pia ngapi kwa Unguja na hayo yote

hayakutendeka. Kwa hiyo, mimi napenda kumuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, katika suala hili aliangalie kwa makini zaidi na alione na baadaye aweze kutupa maelezo kwa nini hali ikawa hivyo kwa sehemu mbali mbali zilioko kule Pemba.

Mhe. Naibu Spika, zaidi katika haya hii fedha yote badala yake huachwa kwa Mkurugenzi kwa ajili ya maamuzi. Kwa hivyo, sijui kama kufanya hivyo ni sawa au vipi fedha hizi hupewa mtu mmoja na kuweza kufanya maamuzi.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho basi aweze kubainisha haya masikitiko yetu ya fedha ambazo sehemu nyingi katika Wizara ya Afya hazikutengewa.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala la wagonjwa wa akili. Mhe. Naibu Spika, kwa Pemba kitengo hiki kipo, lakini huwa hakifanyikazi sawa sawa kama inavyotakiwa. Kwa mfano, ni pale tu wagonjwa wanapokwenda kwa ajili ya kupata huduma kwa wale wanaoweza kukaa pale.

Lakini wakati mwengine kuna kuwa na matatizo kwamba mgonjwa amekuja na anahitaji apate malazi kwenye kitendo kile, kwa kweli suala hilo halipatikani kwa Hospitali ya Chake-Chake kwa ajili ya kuwalaza watu wenye matatizo ya akili. *(Makofi)*

Kwa kweli suala hili tumelipigia kelele muda mrefu, lakini kubwa zaidi pale anapokuja mgonjwa wa akili ambaye anataka apelekwe Unguja, yaani asafirishwe kutoka Pemba na kuletwa Unguja ndio inakuwa matatizo makubwa zaidi. Mhe. Naibu Spika, mara nyingi wazazi wanakuwa hawana uwezo wa kuwasafirisha wagonjwa wao pamoja na dhamana ya mtu kumpeleka kule Unguja.

Kwa hivyo, unapomtoa mtu Pemba unahitaji kumchukua daktari pamoja na kumchangia nauli yake, yaani mzazi atoe nauli ya mgonjwa wake na daktari ambaye anayemleta mgojwa wake.

Sasa nataka kumuuliza Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, mpaka lini mambo haya yatakuwa mazito, mbona mambo haya hayaeleweki kwa wagonjwa ambao wanaotaka kusafirishwa kutoka Pemba kuja Unguja. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuwa kufanya majumuisho namuomba kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, aje atupe ufafanuzi juu ya suala hili na nani atakayegharamia ni wizara au idara ama mtu mwenyewe binafsi.

Suala jengine ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu uhaba wa madaktari. Kwa kweli tumesikia hapa Waheshimiwa Wajumbe wengi wanazungumzia kuhusu suala zima la uhaba wa madaktari na mimi pia nalia, kwa sababu kila mmoja analia kwa upande wake.

Kwa hivyo, kwanza naipongeza Wizara ya Afya kwa Jimbo langu la Konde kwa kuweza kunijengea hospitali nzuri tena ni kubwa, ambayo kipindi hiki tunataka tuitumie kikamilifu. Lakini ndani ya hospitali ile kuna mapungufu makubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, hospitali ni kubwa tena ni nzuri, lakini ina mapungufu ya wafanyakazi. Kwa mfano, tunao upungufu wa Madaktari wa Maabara, Meno, Macho hatuna, isipokuwa wakunga tunao katika hospitali ile na wanafanyakazi zao kama kawaida. Lakini mimi ninalo ombi kwa Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kama Hospitali hii ambayo iko Konde tena ni kubwa, basi ningemuomba Mhe. Waziri mimi pamoja na Mbunge wangu tunayo kazi kubwa sana katika jimbo lile. *(Makofi)*

Kwa kweli Jimbo la Konde jiografikali ni kubwa sana tena lina masafa makubwa ya ndani. Kwa mfano, tunazo gari tatu ambazo zinatoa huduma za Wazazi na Wagonjwa. Lakini mara nyingi tunapopeleka katika Hospitali ya Konde inakuwa ni rufaa kesi, yaani wapelekwe Micheweni au Chake-Chake na kazi hiyo ni kila siku na kila wakati gari zinakwenda, sasa gari zetu ndizo zinazokuwa *Ambulance*.

Mhe. Naibu Spika, jambo la kusikitisha zaidi wakati wagonjwa wetu hawa wakati tunawapeleka Micheweni pale pale hudaiwa na sisi huduma ya kuweza kuwasaidia na sisi hatuondoki na gari zetu mpaka tuhakikishe Hospitali ya Micheweni inao uwezo wa kumpeleka mgonjwa yule Chake-Chake, basi kama haina uwezo inabidi gari zetu zifanye kazi hiyo.

Sasa mimi naomba kumuuliza Mhe. Waziri katika suala la ugavi lazima kutakuwa na ugavi wa mafuta ambao watakuwa wanapewa katika wilaya. Kwa hivyo, hatujui mafuta hayo yanakwenda wapi kama yanakwenda kwa njia za panya na sisi hatufahamu, lakini mara nyingi utakuta wanashindwa kuwasafirisha.

Mhe. Naibu Spika, kama ni hivyo basi mafuta haya ni bora tupewe sisi na tuwapeleke moja kwa moja na ikija rufaa *case* basi moja kwa moja tuwapeleke Chake-Chake kuliko kuwapeleka Micheweni na halafu wanashindwa kuwapeleka Chake-Chake.

Ikiwa hivyo sivyo basi ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba akiichukua Micheweni kama Micheweni na Konde kama Konde, basi Konde nayo inafanywe kwa sababu idadi ya watu walikuwa hawapungui 25,000 na hivi sasa ninao watu zaidi ya 35,000 katika Jimbo la Konde. Hivyo, kwa nini ile Konde isipewe huduma kikamilifu kama Hospitali ya Micheweni. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, afanye uchunguzi wake wa kutosha katika suala hili.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu ongezeko kubwa tena kwa kasi maradhi ya Kisukari, Saratani, Moyo pamoja na Kibovu cha Mkojo. Kwa kweli inasemekana bado hayajajulikana na mimi nasema kidogo katika masuala haya mnatutia wasi wasi.

Kwa hivyo, ikiwa Hospitali ya Mnazimmoja tunataka kuifanya iwe ya Rufaa, mbona wananchi kwa jumla au jamii inapata matatizo au shida katika kutibu maradhi haya. Kwa mfano, hivi sasa hapa

Unguja suala kubwa la maradhi ya Kisukari limejitokeza miongoni mwa wananchi wetu, yaani ni kubwa sana tena la kupigiwa mfano.

Mhe. Naibu Spika, watu wenye ugonjwa wa Kisukari mpaka hivi sasa sijui huduma ya aina gani wanapata, kwa sababu wanapata usumbufu na wala wizara haijui inafanya nini.

Hivyo, kama anavyosema Mhe. Waziri kwenye maelezo yake kwamba anao Madaktari Bingwa na haidhuru alikuwa akitarajia Madaktari 109, lakini kwa hivi anao Madaktari Bingwa 17, pia anao Madaktari wa MD ambao alitarajia awe nao 55, lakini mpaka hivi sasa anao 18. Vile vile kwa upande wa Wauguzi ambao alikuwa akitarajia awe nao 941, lakini anao 305.

Mhe. Naibu Spika, nini *qualification* zao hao Madaktari, yaani wame-*qualify* juu ya kitu gani ikiwa haya maradhi ambayo niliyazungumza mimi ya Sukari, Saratani, Moyo pamoja na Kibovu cha Mkojo. Sasa hawa Madaktari Mabingwa 17 pamoja na wengine mbona tunashindwa kuwatibu hawa na inabidi tuwafanyie *transfer cases* na kuwapeleka Dar-es-Salaam.

Kwa hivyo, hapa nina wasi wasi na elimu yao waliyonayo Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mtu anaweza kwenda kusoma lakini *qualification* zisiwe sawa sawa. Kwa mfano, tunaweza kuambiwa tunao madaktari wengi, lakini uwezo wao wa kutibu watu wetu ni mdogo sana.

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja afanye *clarification* kuhusiana na hawa madaktari, yaani ni aina gani ya madaktari mbona tunaambiwa tunao madaktari wengi tena wakubwa. Mhe. Naibu Spika, ikiwa tunao madaktari basi itakuwa kuna kasoro ambazo zimetokea, kwa sababu tunaweza kusema kasoro kama vile mambo mawili lazima yawe na *account balance*, yaani bila ya kuwa na vifaa au nyenzo basi uhodari wa Daktari Bingwa utakuwa hauna maana, yaani mambo haya lazima yawe na *account balance*. *(Makofi)*

Kwa hivyo, lazima tuwe na maabara nzuri ambayo ni kubwa tena iliyotimia mambo yote, ndipo hapa daktari bingwa anaweza kumtibu mgonjwa wake, lakini daktari bingwa yupo na wala hakuna nyenzo au vifaa, basi uhodari wake utakuwa ni wa bure na itabidi lazima tumfanyie *transfer case*. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho namuomba atufanyie *clarification* nini hasa mapungufu au shida iko wapi, hivi tatizo ni madaktari au vifaa. Kwa maana hiyo, tukitaka kuweka madaktari bingwa basi tuweka na mambo yao, kwamba daktari bingwa yupo lakini vifaa vyake vipo. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala zima la maradhi ya Malaria. Kwa kweli Malaria nakumbuka kipindi ambacho, yaani zamani miaka ya nyuma.

Mhe. Naibu Spika, Ugonjwa wa Malaria Zanzibar tunaambiwa haupo, yaani umemalizika tunavyoambiwa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, unisikilize mimi na wala makofi ya Waheshimiwa Wajumbe yasikubabaishe malizia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kweli malaria tunaambiwa haipo, yaani imepungua sana. Lakini mbona tunakwenda hospitali bado ugonjwa unaibuka, kwa sababu bado watu wanadai kwamba Maradhi ya Malaria yapo.

Suala la pili ambalo nataka niseme labda hii malaria kuna kitu ambacho kinaleta kizuizi katika haya. Mhe. Naibu Spika, tuseme hii dawa ambayo tunayo hivi sasa, yaani hawa watu walioko majumbani wanaikimbia hii dawa hawaitaki na hawaitaki kwa nini kwa sababu sizo dawa ambazo zilikuwa zikitiwa zamani ndani ya majumba. Kwa kweli dawa hii imeleta adha na kero kwa wazazi pamoja na watoto wao ndani ya majumba kwa kuwashwa, yaani inawasha vibaya sana.

Kwa hivyo, ndio maana watu ndani ya majumba wanakataa kutokana na muwasho mkubwa sana. Kwa mfano, akisahau kuotosha bedsheet kwenye kitanda basi dawa ile kama itapulizwa watu wale hawataweza kulala usiku kucha, kwa sababu watawashwa sana pamoja na kuvimba na wataumia kila sehemu. Hivyo, tumuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la madawa, hatuwezi kugeuziwa dawa nyengine ambayo haitokuwa na muwasho.

Vile vile katika miaka ya nyuma tulikuwa tukipata *fumigation* kwenye majumba. Kwa hivyo, siku hizi mambo ya kupuliza katika maeneo ya nje, kwa sababu mbu hawako ndani na hawako nje, hivyo huku nje hatupati dawa za kuwaua hawa mbu wa malaria.

Mhe. Naibu Spika, taarifa tuliyonayo kipindi cha nyuma ni kwamba mbu anapoingia ndani ya nyuma anapogusa ukuta ndio anapoumia, lakini wale walioko nje je, kwa sababu kuna madimbwi ya maji ambapo mbu wanazalia kila wakati na wala hawa hawapulizi dawa nje. Sasa dawa inapulizwa ndani ya nyumba, lakini nje ya kuta za nyumba haipulizwi pamoja na sehemu za madimbwi ya maji pia haipulizwi.

Kwa hivyo, vipi mambo haya nadhani itakuwa ni *circle* ya mbu, kwa sababu yule amekufa na yule ambaye yuko nje anaingia tena na kuhujumu na mbu wapo. Mhe. Naibu Spika, tuseme ukweli kwa sababu kweli tunataka misaada, lakini na sisi tuliomo ndani tunaumia, ikiwa tunaamini dawa hii inatuathiri, basi ni vyema kufanya utafiti na kujaribu kuuliza wananchi je, mnaonaje dawa hii ni nzuri au vipi, watasema kuwa inatuwasha sana na tutafutiwe dawa nyengine ambayo itakayoweza kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, naheshimu muda wako na naomba nitoe hoja kwamba naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ingawa dakika zimeshamaliza.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, dakika kumi kipindi cha jioni.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante. Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake ambayo ameitoa hapa yenye maelezo mengi sana pamoja na mwelekeo mkubwa katika suala zima la afya kwa jamii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango moja kwa moja kwenye Idara ya Tiba hususan katika Hospitali ya Kivunge. Kwa kweli kama alivyoeleza kwenye kitabu chake humu juu ya azma ya kuleta mabadiliko katika Hospitali ya Kivunge, ili kuwa Hospitali ya Wilaya.

Lakini mimi kidogo natafautina na wazo hili, nafikiri kwanza wangeiboresha ikawa *Cottage Hospital* ikakamilika na baadaye ndio tukenda kwenye hilo zoezi la kuwa Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, hospitali hii imetupwa kabisa na wala hakuna kitu kule, kwa sababu kuna malalamiko mengi sana juu ya hospitali hii na hasa ukizingatia hospitali hii ni ya Mkoa badaya ya Wilaya inavyofikiriwa. Kwa mfano, hata ukitizama ile tathmini ya matibabu juu ya wagonjwa wanaowapa huduma, ukilinganisha na hospitali nyengine, basi nadhani inafanana na Hospitali ya Chake-Chake au Wete, lakini kwa hizi nyengine za *Cottage*, basi hii ndio inayoongoza.

Kwa kweli takwimu hapa zimenionesha ina watu karibu 13,628 waliopewa huduma pale, yaani inakaribiana na Hospitali ya Chake-Chake. Lakini tukiangalia zile huduma zinazotolewa pale ni za kusikitisha sana. Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Kivunge kuna malalamiko mengi sana, huduma pale ni dhaifu sana na hata wale watendaji wenyewe hawapo, hivyo lazima huduma zitakuwa dhaifu. *(Makofi)*

Vile vile tukija kwenye suala la madaktari kwa kweli hatuna na hao wasaidizi wa madaktari tuliokuwa nao, basi labda wawili. Lakini tukiangalia wale watu wanaopewa huduma pale, sasa watu wale lazima tuwaonee huruma, kwa sababu watu wawili wale wataweza kutibu watu wote wanakwenda pale kwa siku, hivyo lazima malalamiko yatakuwepo.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, afanye mabadiliko kidogo katika hospitali hii, atuletee madaktari japo hana na hivyo hivyo afanye maarifa atuletee na kule. Sasa ikiwa hatuletei basi tutaendelea kulalamika na wananchi wetu wataendelea kupata tabu.

Namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho yake basi anipe mkakati wa kuibadilisha hospitali hii na kuwa ya wilaya, yaani anieleze lini itakuwa, kwa sababu humu ameandika ndani ya miaka mitano, mimi naina itamaliza hii mitano na wala hospitali hii bado haijageuzwa.

Kwa hiyo, naomba anieleze mwazo hasa wataanza lini kuibadilisha kuwa Hospitali ya Wilaya na kuanza kwake inaanzia vipi, ili tuweze kujua zile hatua, kwamba tutaanza na hiki na kile mpaka tufike huko. Mhe. Naibu Spika, niliwahi kuuliza katika Swali la Msingi hapa, hiyo Hospitali ya Wilaya ili iwe inahitaji iwe na sifa au hadhi gani na nilipewa maelezo mengi sana. Lakini kwa maelezo niliyopewa na Mhe. Naibu Waziri basi sifikirii kama mmeshafika robo ya nusu, mimi naona haipo hata thuluthi.

Sasa ninamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, atakapokuja hapa basi nieleze ule mkakati wa wizara katika kuhakikisha Hospitali hii inakuwa na hadhi ya Wilaya.

Vile vile kuna suala zima la uzio wa hospitali na hili limekuwa ni kilio kikubwa sana hasa kwa wafanyakazi wa pale hospitali, yaani wanapata matatizo makubwa sana na mimi nakubaliana nao kwamba

kweli kuna matatizo kutokana na kutokuwa na uzio wa hospitali pale. Kwa kweli tusisubiri mpaka tukafika pahala tukaambiwa kwamba jana mzazi alijifungua na baadaye mtoto anachukuliwa na mbu kwa sababu hakuna uzio aa! *(Makofi)*

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kuwa ni vyema kujitahidi angalau kwenye bajeti yake ya mara hii nione umo uzio wa hospitali na unaanza kujengwa haraka iwezekanavyo, ili kuondosha kadhia hii.

Nikiendelea na mchango wangu nije kwenye suala la huduma hasa kwenye Kitendo cha Akinamama pale huduma ni dhaifu. Lakini chanzo kikubwa kinaanza na hao wahudumu wenyewe, yaani hao madaktari hatuna. Kwa mfano, daktari anayekuwepo ni mmoja na Hospitali hivi sasa si *Cottage* ni ya Mkoa. Kwa hivyo, huduma kuzitoa kwa watu wote ni lazima tumuonee huruma, kwa sababu anaweza kufika pahala na kusema sasa nimechoka nakwenda kupumzika na mgonjwa anaingia je, utamfanya nini.

Hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kitengo hiki nacho kiangaliwe, kwa sababu hiki ni Kitengo cha Huduma za Mama na Watoto Wachanga, nadhani kina misaada mingi sana, lakini kule kwetu haifiki. Kutokana na hali hiyo, basi namuomba Mhe. Waziri atusaidie na tuone na sisi kule tunapata hayo mabadiliko ambayo wanayapata wenzetu.

Kwa mfano, kuna jengo la kusubiria wagonjwa na lile halina tatizo nakwenda nalo na mimi nakusaidieni na tutakwenda sambamba na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia tutalimaliza pale, ili wananchi wetu wanaosubiri huduma kwa akinamama watapata sehemu ya kukaa na kusubiri huduma. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, zile huduma zinazotolewa mule ndani, basi hao wanaokuwepo wanalalamika sana. Kwa mfano, wajawazito wanapelekwa pale na huduma hizi tunaambiwa zinatolewa bure, yaani huduma za mama na mtoto, lakini sisi kwetu vifaa vyote

wanatakiwa wakanunue. Lakini wakati huo huo kanunueni vifaa na vikiletwa pale, basi wanasema kanunueni pale na suala hili lilizungumzwa na wenzangu waliotangulia nadhani Mhe. Farida Amour Mohammed.

Sasa kwa nini wanaelekeza pahala pa kununua na wala wasimpe uhuru mtu kununua anapotaka. Kwa mfano, mimi nimeambiwa mke wangu anataka kujifungua kule nimekwenda na vifaa ambavyo nimetokanavyo mjini nakwenda navyo kwa nini havitakiwi, unaambiwa aa! Kanunue pale au vipo hapa tupeni pesa mupewe, kwa nini inakuwa hivyo.

Namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba suala hili alishughulikie na liondoke kabisa, yaani wawe huru na kama wao hawana vifaa basi ni vyema mtu kununua akanunue pale anapotaka na yeye kazi yake ni kumuandikia tu. Kwa hivyo, kumlazimisha vipo hapa na wewe utoe pesa hili litakuwa tatizo ndipo pale hisia zinapokuja kwamba vifaa vile ambavyo vilikuwa vinatolewa bure madaktari wanaviuza na hilo ni tatizo. *(Makofi)*

Nikiondoka hapo niende kwenye suala la wodi hizi. Mhe. Naibu Spika, sijui kama Mhe. Waziri amewahi kutembelea katika Hospitali ya Kivunge au anapita njiani tu wakati anapokwenda Kibeni. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, apate siku aingie bila ya kutoa taarifa na kuzikagua zile wodi wanazolala wagonjwa kama alikwenda na homa basi akifika pale anazidi homa, yaani wodi haziridhishi kwa sababu vitanda vichafu pamoja na wodi zenyewe, vyandarua hamna au ukikiona hicho chandarua basi chafya zinaanza, yaani taabani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, atusaidie na hili, ili liweze kupungua. Kwa kweli hili ni tatizo kubwa sana katika hospitali yetu ile.

Mhe. Naibu Spika, naweza kuendelea kidogo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, utaendelea jioni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha kikao kuna tangazo nimeletewa hapa na Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Mhe. Asha Bakari Makame, kwamba wanawake wote wa CCM tukimaliza kikao hiki cha asubuhi wasubiri humu ndani kuna maelezo muhimu wanataka kuarifiwa.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa wajumbe kabla hatujaanza michango yetu naomba nitoe taarifa kwamba huku kwenye kitabu changu nina wachangiaji 29 na muda wetu tumekusudia leo tumalize majadiliano Ijumaa asubuhi tumwite Naibu Waziri na Waziri wamalize kwa sababu ni siku ndogo, tukimaliza masuala na 4.30 inab akia saa 1.30 sasa hata masuala kidogo tutafupisha ili hii tuimalize siku ya Ijumaa asubuhi. Kwa hivyo michango yote tunaimaliza leo jioni kwa hivyo tupunguze kurejea rejea mtu aende kwenye *point* amalize ampe mwenzake tuna watu ishirini. Kwa hivyo tunammalizia dakika zake Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) dakika zako kumi halafu afuatie Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunijali ukanipa niendelee tena jioni hii ya leo, kwa kuwa muda wetu ni mdogo na unasema tusirejee rejee nimalizie pale nilipopaacha kidogo kwenye hospitali ya Kivunge, namuomba Mhe. Waziri aangalie tena katika suala zima la upatikanaji wa mafuta kwa ajili ya huduma za hospitali, tunafika pahala.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa kaa kidogo, Katibu karibu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa muda niendelee hivi sasa namuomba Mhe. Waziri aangalie utaratibu wa upatikanaji wa mafuta katika hospitali ya Kivunge kwa sababu imekuwa ni moja kati ya kero zetu katika hospitali ile, upatikanaji wa mafuta ni mdogo mno kiasi kwamba wanatokea wagonjwa wa dharura kuweza kusafirishwa kuletwa mjini inashindikana.

Ningemuomba Mhe. Waziri akaliangalia fungu hili ili likatuna kidogo wananchi wakaweza kupata huduma hizi, kama ujuavyo wananchi wetu katika Wilaya ile ni masikini sana uwezo wa kumsafirisha mgonjwa kumleta mjini unakuwa ni mgumu, kwa hivyo suala la gari ipo lakini tatizo linakuwa ni mafuta. Sasa nilikuwa namuomba Mhe. Waziri hili atakapokuja hapa aniambie wameandaa andaa vipi katika bajeti yao ili tuweze kuona uwezekano wa kuhakikisha kwamba wagonjwa wetu wanaopata *transfer* kutoka Kivunge kuja Mnazi Mmoja wanapata usafiri wa uhakika.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye nyumba za madaktari hao wafanyakazi ambao wanaletwa pale Kivunge tatizo lao ni makaazi nyumba zipo lakini zimechoka, mimi nafikiria nyumba zile tokea zilipojengwa mwanzo wa ujenzi wa hospitali ile hazijawahi kugaiwa hata chokaa, sasa unaweza kukuta daktari anakuja lakini hadhi aliyokuwa nayo na kukaa ile nyumba anashindwa ndio kinachomfanya awe anakuja lakini ile hadhi aliyokuwa nayo na kukaa ile nyumba anashindwa ndio kinachomfanya awe anakuja mjini na kurudi, matokeo yake huduma pale zinaanza saa 4.00 asubuhi badala ya saa 1.00 asubuhi.

Unafika pahala daktari anakimbilia sasa niende zangu naweza kukosa gari akaondoka saa 10.00 matokeo yake wagonjwa pale wakikaguliwa mara moja hawakaguliwi tena mpaka siku ya pili, kwa hivyo hili ni tatizo namuomba sana Mhe. Waziri nilizungumza zaidi kwenye suala la madaktari, akiweza kutupatia madaktari wa kutosha

nafikiri kadhia hii itatupungua, nakuomba utusaidie sana katika hilo Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye mpango wa damu salama kuna tatizo pale Mhe. Waziri sijui kama unalijua au vipi kuna watu hawajalipwa mshahara wa miezi sita, kutoka April nafikiria mpaka Septemba hivi ya mwaka jana. Sijui kama Mhe. Waziri analifahamu lakini naomba utakapokuja kutoa majumuisho yako hapa basi unipe ufafanuzi wa suala hili kwamba je kweli, na kama kweli kwa nini imekaa mpaka miezi sita hawajalipwa.

Sasa nije kwenye hospitali ya Mnazi Mmoja donda sugu huli, hospitali hii wenzangu waliopita wamelichangia sana na muda tuliokuwa nao ni finyu mimi niunge mkono juu ya hoja walizochangia wenzangu juu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja matatizo hayo waliyoyazungumza ni kweli yapo, hasa hiyo *I.C.U* matatizo yapo kweli, lakini tuangalie mimi nimetoka hospitali mchana huu basi hata vile vyoo wodi ya pili pale wodi nzima choo kimoja, hivi wagonjwa wote wale wataweza kwenda kujisaidia kwenye choo kimoja vilivyobakia vyengine vimewekewa vitanda vibovu kabisa kwa mba havitumiki. Sasa hata hili nalo linahitaji mfadhili kusafisha vile vyoo tu tukapata kuvitumia, mimi nafikiria Mhe. Waziri uangalie sijui kama umewahi kufanya ziara kule ukatembelea tembelea katika ile hospitali.

Halafu Mhe. Jaku Hashim Ayoub alizungumza hapa kuhusu suala la kitanda cha upresheni ni kweli mimi nina mgonjwa kenda upresheni juzi, leo nimemuuliza naam hakilaliki kama hukwenda na plastiki lako kikatandikwa basi huwezi kukilalia hicho kitanda kama utakuwa na fahamu zako, labda umetolewa fahamu ndio utaenda kulala kichafu mno hakishikiki au hakilaliki, haya masuala ni muhimu na yafanyiwe marekebisho utakapokuja hapa utueleze ni sababu zipi zinazochangia kuwepo kwa hivi.

Mhe Naibu Spika, nikiondoka hapo nije kwa Mkemia Mkuu wa Serikali hiki kitengo Mhe. Naibu Spika, ni kitengo muhimu sana

katika nchi yetu lakini kila nikikitizama ni kitengo ambacho kimewekwa mwisho kabisa, ukiitizama hiyo maabara unayoambiwa ya Mkemia Mkuu pale Mwanakwerekwe ukipita, angalau leo humu kwenye bajeti mmebadilika ndio anataka kwenda Kiwanda cha Sigara. Sasa sijui mkakati wake uko je Mhe. Waziri katika kuhamisha haraka iwezekanavyo tukaanza kuhamia katika hilo jengo jipya na vitendea kazi vipya vikaweko. Wataalamu nina hakika tunao lakini vitendea kazi ndio tatizo. Sasa unakapokuja hapa Mhe. Waziri naomba maelezo ya kutosheleza kidogo ili tuweze kuona kweli kama serikali imedhamiria kukiboresha kitengo hiki na kuhakikisha kwamba kinafanya kazi zake ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi nilikuwa nataka nibakie nusu nusu lakini naiunga mkono ili niwape nafasi wenzangu waendelee kuchangia. Ahsante sana.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia baadhi ya mambo mawili matatu katika bajeti ya Wizara ya Afya, kwanza kabisa nachukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kutujaalia salama, lakini pia kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa namna ambavyo unaendesha shughuli zako kwa ufanisi na kuhakikisha kwamba bajeti kuu ya serikali inapita vizuri.

Lakini pia namshukuru Waziri wa Afya na watendaji wake wote kwa ujumla pamoja na wawakilishi wote waliomo humu ndani kwa namna wanavyoweza kuichambua hii bajeti kwa lengo na madhumuni ya kuisaidia serikali ili iweze kufanya vizuri zaidi katika mwaka wetu wa bajeti 2011/2012.

Mimi nianze katika hoja ya kuaza kasi zaidi katika suala la utafiti nahisi kwamba sasa hivi umefikia wakati wa kuweza kufanya utafiti na kuweza kujua magonjwa ambayo yanawaathiri watu wetu ili tuweze kupata raslimali watu ambayo itaweza kutusaidia na kuweza kuongoza nchi yetu vizuri sana. Katika nchi yetu sasa hivi kuna magonjwa ambayo yamejitokeza kwa kasi sana kama magonjwa ya

BP, Moyo na vibofu vya mkojo kwa wazee wetu wa kiume, maradhi haya sasa iko haja ya kufanya tafiti za uhakika na kuhakikisha kwamba tunaisaidia serikali pamoja na watu wake ili tuweze kupata maendeleo ya kweli.

Pia napenda kuchukua fursa hii kuzungumzia zaidi suala la maslahi ya wafanyakazi katika hospitali zetu, bado nahisi kuna tatizo katika namna ya kuwahifadhi madaktari wetu ambao wanatuondoka kwa wimbi kubwa kabisa, wenzetu wameshatangulia kusema hapa juu ya maslahi ya madokta lakini na mimi nilikuwa nakazania zaidi suala hilo tuweze kuwasaidia ndugu zetu ili tuweze kufika pahala ambapo madaktari wetu wanabakia nchini na kuwasaidia wananchi wetu.

Jengin Mhe. Naibu Spika, ambalo nataka kuchangia ni suala la kitengo cha bandarini katika ukurasa wa 18 kuna kitengo cha afya bandarini, kitengo hiki ni muhimu sana Mhe. Naibu spika, na vyakula ambavyo vinaingia nchini kwetu hapa vinapita katika vitengo hivi na hapa pana watendaji ambao huwa wanachukua *sample* ya hivi vyakula na mambo ambayo yanakuwa yanahusiana na vyakula vya binaadam ili kwenda kuangalia kwa Mkemia Mkuu, baadae kuweza kuruhusiwa ili viweze kutumika kwa wananchi wa kawaida. Cha kushangaza ni kuona kwamba pamoja na harakati hizi zinazochukuliwa na jitihada zote zinazofanywa na serikali lakini bado vyakula vibovu vinakamatwa katika maduka vikiwa vimeingia nchini kupitia katika maeneo yetu ya bandari na kwa muda mfupi kabisa, ningeomba kitengo hichi nacho kifanye kazi vizuri sana ili tuweze kwenda vizuri katika masuala yetu.

Kwa kukimbiza muda zaidi Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika ukurasa wa 80 katika ukurasa huu unasema katika utekelezaji wa mkakati wa kuhakikisha vifo vya kinamama na watoto vimepungua sana katika kipindi hiki, kati ya kinamama na watoto ambao wanafariki kwa hisabu ambayo imewekwa hapa ya 422 tukasema kwamba kuna unafuu kwa vifo vya kinamama na watoto 287 bado hatujafanya, tunaomba juhudi za lazima zichukuliwe tuhakikishe

kwamba tunawadaidia zaidi kinamama na watoto ili tuweze kuondokana na vifo hivi.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nilikuwa nataka kwenda katika changamoto hizi, katika ukurasa wa 90 nimeona mahitaji ya dawa muhimu kwa mwaka hazipunguzi shilingi 3,000,000,000 kiwango kilichotegemewa kutokana na misaada ya wahisani kwa ununuzi, lakini utunzaji na usambazaji wa dawa ni shilingi bilioni 1.5 lakini serikali imetenga shilingi milioni 700. Mhe. Naibu Spika, kiwango hiki ni kidogo sana naiomba sana serikali ifanye utaratibu mwengine hususan katika wizara inayohusika hiyo ili kifungu hiki ambacho ndio kwenye maslahi na kuweza kuwasaidia watu wetu na wananchi kwa ujumla, pafanyiwe marekebisho na kipengele hiki basi kiweze kuzidishwa kuliko kuwa katika hali hii ambayo ipo kwa sasa na itakapokuwa kipengele hiki kipo hivi basi kidogo patakuwa na mtihani.

Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ansate sana Mhe. Naibu Spika, jioni hii na mimi kunipa muda wa kuchangia kidogo hoja ya Wizara ya Afya, mimi kwanza nataka kuanza kwenye hospitali ya Abdalla Mzee ambayo ndio na mimi ninakotoka.

Mhe. Naibu Spika, hospitali hii ipo tokea mwaka 1969 lakini sijaona hata sentimita moja ya ongezeko la jengo, lakini mwaka huu nimefarijika sana kuona kwamba bajeti hii imetenga au imejiandaa kwa ajili ya kujenga wodi ya watoto katika Hospitali ya Abdalla Mzee, nitawashukuru sana nikiona kwamba mbio zao za mwanzo Waziri pamoja na Naibu wake pamoja na makatibu wao zikaanzia pale Mkoani Hospitali ya Abdalla Mzee.

Mhe. Naibu Spika, hospitali hii inatoa huduma nyingi lakini hivi sasa naweza kusema nayo inahitaji kupewa huduma kwa sababu iko taabani sana, imezidiwa nathubutu kusema hii ni moja katika

hospital ya rufaa iliyoko katika Kisiwa cha Pemba, wagonjwa wengi sana wanakuja sehemu ile kutoka sehemu mbali mbali za kisiwa cha Pemba hasa ikitiliwa maanani kwamba pale kuna mabingwa kutoka China. Napenda niwapongeze kwamba tokea miaka yote hiyo tokea mwaka 1969 wanaendelea kuja na kutoa huduma zao na kuchangia dawa hili ni jambo la faraja kwa nchi yetu inabidi tuwapongeze.

Mhe. Naibu Spika, katika hospitali hii kuna mengi ambayo yanachangia huduma zake ziwe duni. Kwanza hilo jengo ambalo nitashukuru nikiona limepatiwa ufumbuzi, lakini hivi sasa kumekuwa na kutokuwa na imani na watendaji yaani kumekuwa na ugonvi mkubwa kati ya watendaji wadogo na wakubwa. Kuna malalamiko mengi wadogo wanasema wakubwa wao hawawatendei haki kwa hivyo ningeiomba Wizara suala hilo ikaliangalia kwa kina.

La pili ni uchafu katika hospitali hii miaka ya nyjma ilikuwa ni ya mfano hasa kwa ule mjengo wake ulivyo, lakini hivi sasa licha ya kuwa ina wafanyakazi wengi wahudumu wa kukata majani na wengineo ni moja katika hospitali chafu sana. Nashukuru kwamba kipindi kidogo baada tu ya kutangaziwa Mawaziri wa serikali ya awamu ya saba wale wahudumu walianza zoezi la usafi, lakini tu kuona huy JD hapiti tena basi mambo yale yote yameachwa hivi saa. Kwa hivyo ningewaomba wakayasimamia hospitali ni usafi ikawa pale panapatikana usafi wa hali ya juu.

Sambamba na hilo hivi sasa kuna madaktari ambao tunawaita wanatokea *Red Cross* na wafanyakazi ambao labda walipangiwa kukata majani, wafanyakazi wale Mhe. Naibu Spika, leo ndio wanaotia *drip* leo ndio wanaopiga shindano ni hatari, kwa hivyo ningeomba hili lisiendelee kwa sababu kunahatarishwa maisha ya watu.

Mhe. Naibu Spika, halafu kuna malalamiko mengi kwa mama wajawazito kwamba wanapokwenda katika lile dungu lile basi unakuta yule daktari ambaye yuko sehemu ile kule ni mwanamme, hiki ni kinyume cha maadili yetu sasa wengine kwa kuogopa hili

wanahiyari wajifungulie majumbani ambapo riski zake zinakubwa ni kubwa zaidi kwa vifo. Kwa hivyo ningeomba nalo hili likashughulikiwa.

Lakini vile vile ni kwamba madaktari wetu tuliokuwa nao sio Hospitali ya Abdalla Mzee tu pamoja na Hospitali ya Chake-Chake ni wageni, ili umtibu mtu sawa sawa unahitajika uwe na mawasiliano baina ya mgonjwa na daktari, madaktari wetu ni wageni aidha watakuwa wanaelewa Kiingereza lakini mgonjwa haelewi kiingereza anaelewa Kiswahili. Kwa hivyo haipatikani hasa mgonjwa ana tatizo gani tunakwenda kwa kubahatisha, nikupe kesi ambayo imenikuta mimi.

Kama kawaida yangu siku moja niliingia hospitali nikamkuta mama anaingia kwa Kizishan kufika pale akakaa kitako sijui kama alimuuliza au alimwambia, lakini kwa lugha ya Kiswahili yule daktari akamwambia kohoa mama yule akakohoa kukohoa daktari moja kwa moja akaandika ana tatizo la kukohoa akampa dawa, lakini hiyo haikuwa ndio kesi. Kumbe yule mama alikuwa hawezi kujieleza kwa sababu hajui lugha, mimi kutokea nikamwita mbona mama unatoka kwa daktari na unafika hapa bado unasononeka akasema mimi tumbo limenishika baada ya kuona vile nikarudi kwa daktari kwa vile na mimi ninacho kiingereza kidogo cha kuokota okota njiani nikenda kumfahamisha.

Nikamwambia *the case is not a chest she is suffering from that and that,* ikabidi amwite alipomwita yule ndani tena kumfanyia utafiti pale pale ikabidi aite timu yake ya *theater* ya kwenda kumfanyia upereshen, sasa haya pia tuyaangalie tunapoleta madaktari wetu kama hawa basi tuwawekee mtu ambae ataweza kuweka mawasiliano kati ya mgonjwa na daktari.

Mhe. Naibu Spika, kuna huduma za *ambulance* magari yapo lakini yanatumika kwa huduma za watu wengine, sasa ili kuokoa hao mama wajawazito kuna baadhi ya wakati wanahitaji wapatiwe huduma ya haraka ya *ambulance* japo kuwa na sisi tunajitole kadiri

ya uwezo wetu kutoa magari, lakini kuna kesi nyengine zinapotokea lazima kuwe na gari inayookoa maisha ya watu *ambulance* zipewe mafuta japo salio dogo. Kuna kesi *serious* zinahitajika kwenda hospitali.

Mhe. Naibu Spika, sasa nakwenda kidogo kwenye hospitali za watu binafsi hizi hospitali hazikuzungumzwa sana Mhe. Naibu Spika, lakini zina mchango mkubwa katika kutoa huduma, lakini huduma zinazotolewa na hospitali hizi zinakuwa ni kubwa na ili kuondoa msongamano katika mahospitali yetu basi na wao wangeshauriwa hawa. Wizara ya Biashara licha ya kuwa serikali imetangaza biashara huru, lakini wamekaa na wafanyabiashara wamewaambia na wameelewa kwamba bei zikipanda wanaoumia ni wananchi kwa hivyo wameweka kitu kama *ceiling* ambacho kinasaidia kila mfanya biashara anaelekea katika mfumo huo, kwa sababu wanajua bei ya mchele huko ni bei fulani. Kwa hivyo wameweka kitu kama *regulator* cha kuweka kukantroli bei ndio maana ukaona bei hazipandi kiholela hivi sasa.

Sasa na Wizara ya Afya nayo licha kuwa kuna uhuru wa kufanya hospitali za binafsi basi nayo ingeliangalia hili kwa sababu *origin* ya dawa na *price* inazifahamu, tukakaa na wenye hospitali binafsi tukawahamisha kama wananchi wetu ni wanyonge wanahitaji msaada ili zile dawa tunapokwenda hospitali tukazipata angalau afadhali, hivi sasa mtoto wa mkulima kama kajikwaa njiani kwa kuogopa tetenasi dozi yake ni shilingi elfu nane hiyo ni ghali. Kwa hivyo tuandae utaratibu wa kumuona kwamba mtu kama hatopata fursa ya kwenda hospitali ya serikali basi awe na uwezo wa kwenda hospitali ya binafsi ili itusaidie katika mazingira kama hayo.

Lakini vile vile hizi hospitali pia zinahitaji kupitiwa mara kwa mara leo inawezekana tu unaumwa na homa ikawa haihitajiki upate dawa za aina kumi, lakini kwa vile wao wapo kwa ajili ya biashara ukenda pale unaweza kuandikiwa dawa kumi kwa vile unakohoa tu wewe, lakini nani wa kuangalia kwamba kile unachokifanya ndicho au sicho hayupo. Kwa hivyo nawaomba Wizara hizi hospitali azipitie

wakati mwengine unaandikiwa *cocilin, cofta* zote ni za kutibu kifua, kwa sababu wanaona kwamba *expire date* iko karibu sasa ili kuziuza dawa zake Mhe. ameshakuja au fulani ameshakuja anaandikiwa tu dawa tano au saba, wakati pengine dawa moja tu yeye ingelimtibu.

Mhe. Naibu Spika, nakuja kidogo kwenye Mkemia Mkuu hichi ni kitengo chenye umuhimu wake kwa sababu kutokufanya kazi kwao ni hasara kwetu na ndio ukaona tuna maradhi mengi, kwa sababu kama hawana utalaam au hawana vifaa vya utendaji kazi basi wagonjwa wataongezeka, kwa sababu wao wataruhusu vyakula visivyo na viwango kupita na sisi kuvitumia matokeo yake msongamano wa watu katika hospitali. Bajeti yao ya mwaka 2010 ilikuwa milioni 15 kwa kisiwa cha Pemba, lakini bajeti yao ya mwaka 2011 ni milioni 7 na sisi tunasema tunataka kutanua huduma hizi sasa hapa kwa watu wa mahisabu mimi ni mtu wa herufi lakini naona kidogo iko kinyume nyume. Naomba kusikia au kuona kitengo hiki basi nacho kimepewa umuhimu wa pekee.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alituomba kwamba sisi kama ni wawakilishi tuwasaidie hao madaktari waliopelekwa Pemba mwezi uliopita kwa kuwapatia sehemu za kukaa, lakini hivi sasa imegundulika kwamba kuna majengo ambayo yako chini ya Wizara ya Afya hasa katika sehemu za Wete, majengo haya inasemekana waliyopewa au wanaoyatumia si wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Kwa hivyo mimi ningeomba pakafanywa utafiti ikajulikana je hili ni kweli au sio kweli baadae tukazipeleka nyumba zile kwa Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, hapo nyuma nilikuwa nikiona utaratibu wa uuzaji wa vitu barabarani sijui ndio mama ntilie au tunawaita nani, zamani ili upewe leseni na Manispaa ulihitajika upeleke kisanduku chako ambacho kitakuwa na vioo kuhifadhi uchafu nzi na wadudu, nafikiri kuna sera Wizara ya Afya inayosimamiwa na Baraza la Mji. Kwa hivyo ningeomba sasa kwa sababu wauzaji wale wamekuwa wengi mitaani na ndio wanaosababisha maradhi ya mripuko, sasa ule

utaratibu ungerejea tena. Kwa mwenye kutaka kuuza samaki, maandazi alazimishwe auze katika sehemu ya kuhifadhi iliyo safi.

Mhe. Spika, kwa hayo machache na mimi naungana na wenzagu kunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi nami nikaweza kuchangia mawili matatu katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia jioni hii ya leo kukutana hapa katika Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kuchangia bajeti ya Mhe. Waziri huyu.

Mhe. Naibu Spika, Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zina umuhimu lakini kwa Wizara hii ya Afya ina umuhimu wa aina yake, kwa nini nikasema hivyo. Wizara hii ya Afya inawagusa wananchi wa Zanzibar moja kwa moja katika shughuli zao za kila siku na sote tulishuhudia kwamba kama huumwi hapa basi unaumwa pengine, kwa hivyo tunaitegemea wizara ya afya katika maisha yetu ya kila siku. Ni wizara muhimu sana, umuhimu wa pekee na kwa sababu hizo ambazo nimezitaja.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wangetegemea wizara hii serikali inatoa vipaumbele vya kutosha katika maeneo yake yote. Wananchi wa Zanzibar asilimia kubwa ni wanyonge hawawezi kumudu gharama za matibabu iwe za ndani na hata zile za nje. Kwa wananchi wa Zanzibar ni mzigo mkubwa. Wizara hii inahitaji kupewa kipaumbele katika maeneo yote.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe hapa wamezungumzia sana juu ya masuala haya. Nami nitapata kugusia baadhi ya maeneo, pamoja na kwamba maeneo hayo pengine yamewahi kuzungumzwa. Lakini waswahili wanausemi wanasema kwamba, **“papo kwa papo kamba hukata jiwe”.** Nije katika Hospitali Kuu ya Mnazimmoja.

Mhe. Naibu Spika, Hospitali Kuu ya Mnazimmoja ndio kimbilio letu sote. Pamoja na kwamba kuna hospitali nyingi, kuna hospitali nyengine zenye sifa kama Hospitali ya Al-Rahma, lakini pale madaktari wao wanaposhindwa kutoa huduma basi kimbilio lao ni Hospitali Kuu ya Mnazimmoja.

Mhe. Naibu Spika, kwa maana hiyo hospitali hii inahitaji kuwa na vifaa vya kisasa, vinavyokwenda na wakati, madaktari wa kutosha, wauguzi wa kutosha wenye huruma na mambo mengine yanayohitajika kihospitali. Lakini inaonekana ni kinyume chake, malalamiko hapa yamekuwa mengi.

Mhe. Naibu Spika, hospitali au matibabu katika nchi yanauhusiano mkubwa sana na uchumi wan chi. Tukiwa hatuna hospitali zenye sifa, tukiwa hatuna hospitali zenye hadhi, basi hata wageni watashindwa kuja hapa kwetu Zanzibar. Hili Mhe. Naibu Spika, lipo, wewe mwenyewe ni shahidi, wakati tulipopata mualiko kwa wenzetu wa *ZATI* ambao wanahusika na masuala ya utalii. Moja kati ya sababu ambazo zinawapelekea watalii kushindwa kuja hapa kwetu ni huduma ya matibabu.

Mhe. Naibu Spika, kama unavyojua sasa hivi dunia kama kisiwa, ni mtandao. Wageni wanapoingia kwenye website na kuona hali ya matibabu yetu hapa visiwani wanafika pahala hayawaridhishi na wanabadilisha muelekeo. Hii ni moja kati ya changamoto ya uchumi wetu. Mgeni mara nyingi hususan mtalii anapokwenda pahala anaangalia maeneo mengi.

Mhe. Naibu Spika, serikali ni lazima ione umuhimu huu katika hospitali hii ya Mnazimmoja. Jambo hili sio la Waziri wa Afya. Mimi matumaini yangu Waziri wa Afya pamoja na wasaidizi wao wangependa kuona hospitali hii inapata huduma zote zinazostahiki. Jukumu hili ni la Serikali Kuu, kuona umuhimu wa kufanya mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, leo kitengo ambacho kimezungumzwa sana na wengi hapa, kitengo cha *ICU*. Kitengo kile ni muhimu na kina umuhimu wa aina yake. Ni kitengo ambacho kinashughulikia wale wagonjwa ambao mahututi wanachungulia kaburini, wangetegemea uhai wao uokolewe pale. Unapopata taarifa kwamba serikali imeshindwa kutoa shilingi milioni 800 kwa ajili ya kukifanyia matengenezo kitengo kile kwa kweli inakuwa ni jambo la kusikitisha sana. Wagonjwa wetu wanapopata matatizo ambayo yanafikia pahala wanahitaji huduma ile waende wapi?

Mimi niiyombe sana serikali pamoja na kilio cha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi juu ya kitengo hiki. Watafute fedha popote pale zilipo ili tuone kwamba kitengo hiki kinapata vifaa vya kutosha, kinapata zana za kutosha ili kiweze kutoa huduma inayostahiki.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo ningepaswa kulizungumzia juu ya maslahi ya madaktari. Mimi nikizungumzia maslahi mara nyingi nazungumzia maslahi ya madaktari. Kama nilivyotangulia mwanzo kusema kwamba maeneo haya ni muhimu na sote tunayahitaji. Pamoja na kwamba serikali ina wataalamu wa aina nyingi lakini mimi nazungumzia hususan madaktari ambao tunawategemea kwa ajili ya kuokoa maisha yetu, kwa ajili ya kuokoa uhai wetu.

Mhe. Naibu Spika, madaktari wanahitaji kuangaliwa ili waweze kufanya shughuli zao ipasavyo. Mhe. Waziri wa Utawala Bora hapa juzi alipokuwa akiwasilisha hotuba yake alituelezea wamezingatia maslahi ya wataalamu na wameweka nyongeza za asilimia 50 ya mishahara yao. Mimi nathubutu kusema asilimia 50 ya mishahara waliyokuwa wakiipata madaktari bado haikidhi haja kulingana na hali halisi ilivyo.

Sote tunafahamu nini wanachokipata madaktari, unapozungumzia asilimia 50 ya madaktari tunaelewa tunakusudia kitu gani pamoja na kwamba Mhe. Waziri alisema kuna tofauti ndogo sana kati ya madaktari wanaokimbilia Tanzania Bara na wale madaktari wa hapa.

Mhe. Waziri wa Utumishi Bara juzi ameongeza mishahara kwa Tanzania Bara. Kwa hivyo watazidi kutukimbia, watazidi kuelemea Tanzania Bara, wakati sisi tukiongeza asilimia 25 wenzetu wamekwenda mbali zaidi. Bado tunahaja ya kuangalia maslahi ya madaktari.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni suala la madaktari kuwepo wakati wa usiku. Suala hili ni muhimu na kwa sababu hospitali ya Mnazimmoja ni hospitali ya Rufaa, kunahitaji madaktari wawepo. Njia ya kuwafanya wawepo pale zipo na tunazielewa. Wenzetu Tanzania Bara madaktari wanakuwepo nyakati za usiku. Kinachowafanya wawepo maana yake kunakuwa na posho maalum ya usiku. Daktari Bara anapokuwa na zamu ya usiku analipwa posho la Shs.10,000/- kwa siku.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri hebu tuwaige wenzetu ili tuone na madaktari wetu wanakuwapo hospitali ya Mnazimmoja. Pamoja na kwamba tumesema wanakaa wanakuwepo. Lakini si kweli madaktari hawakai zamu pale na kwa sababu hatuwawezeshi kuwepo pale, pengine hata hicho kima wanachopewa kama kipo basi ni kidogo. Tufate wenzetu wanavyofanya ili na sisi tuweze kuwaweka pale waweze kuwahudumia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kama unavyojua mara nyingi maradhi yanazidi wakati wa usiku kuliko mchana, hiyo ndio *nature* ya maradhi yanavyokuwa. Madaktari wanatakiwa wawepo pale kwa ajili ya kuwahudumia wananchi. Tutafute njia ya kuwawezesha ili kuona wanakaa pale.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la miradi. Mhe. Waziri ametueleza miradi mbali mbali ukiwemo mradi wa Afya ya Uzazi na Mtoto. Mradi huu Mhe. Naibu Spika, unaumuhimu wa aina yake. Kwa sababu mradi huu unalenga kuzuia vifo vya akina mama na watoto, kwa hivyo ni muhimu. Pamoja na kwamba taarifa zinatueleza kwa mujibu wa takwimu kwamba idadi ya akina mama wanaofariki kwa kujifungua inapungua siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hapa katika *speech* yake ametueleza kwamba naomba ninukuu:-

> "Licha ya mafanikio hayo bado kuna idadi kubwa ya wajawazito wanaojifungulia majumbani chini ya usimamizi wa wakunga wa jadi. Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika mwaka 2010. Taarifa zinaonesha kwamba asilimia 50 ya wajawazito wanajifungulia majumbani hali inayoweza kuhatarisha maisha ya mama na mtoto."

Mhe. Naibu Spika, hebu tujiulize kwa nini nusu ya kina mama hawa wanajifungulia majumbani, badala ya kwenda hospitali. Pamoja na elimu yote hii ambayo inatolewa kila siku. Kuna jambo ambalo kama tutalifanya basi litasaidia akina mama hawa kwenda kujifungulia katika vituo vya afya. Suala la ada wakati wa kujifungua pale akina mama wanapohitaji kufanyiwa upasuaji.

Mhe. Naibu Spika, hili tumelizungumza sana lakini bado wenzetu wa Wizara ya Afya hawajaona umuhimu wa kuondosha hii ada ya Shs. 40,000/-kwa ajili ya akina mama wanaotaka kufanyiwa upasuaji wakati wa kujifungua. Watu wetu ni wanyonge Shs.40,000/- kwa ajili ya jambo hili ni nyingi. Pamoja na kwamba taarifa zinatolewa kwamba si lazima kutoa lakini suala hili ni lazima na limepwa kipa umbele. Sisi ndio wawakilishi wa wananchi tunashuhudia wananchi wetu wanapotujia majumbani mwetu na kutueleza matatizo yanayowakuta wakati wanapotaka kufanyiwa upasuaji kwa ajili ya uzazi.

Mhe. Waziri Shs.40,000/- iondoshwe isiwepo. Mama wakati anapojifungua anakuwa kwenye hali mbaya yupo kwenye *sakaratul –maut*. Leo mama huyu wakati yupo katika hali ile halafu unamtaka atoe pesa kwa ajili ya jambo lile, kwa kweli inasikitisha sana. Tungemuomba sana Mhe. Waziri hili alizingatie sana, atafute pesa popote achangishe michango eneo lolote lakini eneo hili halihitaji kuchangiwa kwa wakati wetu huu. Akina mama wanawategemea

akina baba akina baba hali zao ndio hivyo taabani. Tungemuomba Mhe. Waziri pamoja na ukata aliokuwa nao. Pamoja na upungufu wa fedha alizokuwa nazo katika mahitaji ya hospitali ya kila siku. Pamoja na bajeti finyu aliyowekewa na serikali lakini eneo hili aliangalie kwa huruma. Akina mama hawa awaangalie kwa huruma hasa wakati ule wanapokwenda kujifungua.

Mhe. Naibu Spika, mwisho nimeona kuna mradi hapa. Miongoni mwa miradi ambayo Mhe. Waziri ametuorodheshea ni mradi wa Chuo cha Madaktari Zanzibar. Sote tunafahamu kwamba tuna Chuo cha Madaktari hapa kwetu na Mhe. Waziri ametueleza kwamba kuna mradi wa Chuo cha Madaktari. Nimejaribu kuangalia kwenye kitabu hiki sikuona mradi huu na wala sikujua umetengewa kiasi gani cha fedha. Ni mradi muhimu na unalengo la kuondosha matatizo ya madaktari. Kutokana na upungufu wa madaktari ndio maana serikali ikaamua kuanzisha mradi huu wa Chuo cha Madaktari Zanzibar kwa lengo la kupunguza matatizo ya madaktari. Nilivyoangalia sijaona kwamba mradi huu ukoje, umetengewa kiasi gani. Ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa hebu atupe kwa muhtasari mradi wa Chuo cha Madaktari umekusudiwa nini na ukoje.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho ni Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mradi huu umepata mfadhili na unapesa kiasi cha shilingi bilioni 3. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja kufanya majumuisho hetu tuelezee huu Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja unalenga nini. Hospitali ya Mnazi Mmoja inaonekana ina matatizo mengi. Pamoja na kwamba suala la *ICU* tumelizungumza lakini kuna matatizo katika chumba cha Thieta. Chumba ha Thieta hakina vifaa vya kutosha. Hata eneo la *X-ray* nalo lina matatizo. Jengine madaktari wako wanapokwenda kazini hawavai uniform. Huwezi ukampambanua daktari na anayetibiwa. Haya ni matatizo ambayo yapo katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Spika leo unapokwenda kumpambanua kati ya mtu anayekwenda kumuangalia mgonjwa na daktari, utajiuliza daktari

yupi, anayetibiwa yupi na anayekwenda kumuangalia mgonjwa yupi, kinyume na pale mwanzo. Nimuombe sana Mhe. Waziri mradi huu hetu atueleze umelenga nini? Kwa sababu hospitali yake ina matatizo mengi.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, muda wako umekwenda nilikuwa nina mengi ya kuzungumzia. Naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri. Kama nilivyotangulia kusema kwamba Mhe. Waziri hoja yake hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ni yake lakini mzigo mkubwa upo serikalini. Kama nilivyotangulia kusema kwamba Mhe. Waziri angependa hospitali yake iwe ni nzuri, yenye vifaa vya kutosha madaktari wake waweze kupata maslahi ya kutosha. Wakati atakapo fanya majumuisho atueleze hali halisi ilivyo, asijaribu kubanabana kuonekana kwamba yeye yupo katika hali nzuri. Aeleze hali halisi ya hospitali yake ili tuweze kumsaidia.

Tunajua kwamba ana matatizo mengi na hayawezi kutatuka bila ya kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeshea Hospitali ya Mnazi Mmoja na hospitali nyengine. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, na mimi nishukuru kupata nafasi hii. Mimi nina michango kama nine lakini nitajaribu kuizungumza kwa ufupi ili niweze kutoa nafasi kwa wenzangu na wao wapate muda wa kuchangia kwa utulivu.

Mhe. Naomba nianzie mchango wangu kwa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongochekundu. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada zake za kuanza kufanya ujenzi katika hospitali ile. Pia kwa kufanya marekebisho katika baadhi ya wodi kwa mambo madogo madogo.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu bado namuomba Mhe. Waziri pamoja na jitihada za Kiserikali ambazo zimefanywa bado hospitali ile ina matatizo makubwa. Uzio wa hospitali ile watu wambao wasioitakia mema serikali hii wametoboa matundu na wanapita kwa aili ya kufanya uhalifu katika hospitali ile. Naomba Mhe. Waziri

ajaribu kuliangalia hilo, ingawa kuna baadhi ya maeneo yameshafanyiwa ukarabati lakini bado tatizo lipo na baadhi ya watu wanaingia kufanya vitendo viovu ambavyo havistahiki katika neo lile.

Mhe. Naibu Spika, pia nimuombe Mhe. Waziri aangalie msitu wa hospitali ile. Mheshimiwa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili ina msitu au tuseme mashamba ambayo hayaridhishi kukaa katika eneo kama lile la hospitali la ndugu zetu wanaotibiwa katika eneo lile.

Mhe. Naibu Spika, la pili nilikuwa naomba nichangia katika suala la vijana wetu wanaopata mafunzo kutoka kwa ndugu zetu Waquba. Kuna ndugu zetu vijana wa kizanzibar wapatao 40 walichukuliwa tangu mwaka 2007 kwa ajili ya kupata mafunzo kutoka kwa ndugu zetu wa Cuba. Miongoni mwao hao wawili walitoroka, kuna tarifa Mhe. Waziri atatuthibitishia kama zina ukweli ndani yake au hazina ukweli kwamba kada wanaosomeshwa ndugu zetu wale haitambulikani. Kwa sababu kinaambiwa Chuo hakitambulikani rasmi. Ndugu zetu hao tunategemea mwaka 2014 wanamaliza mafunzo yao pale. Hili Mhe. Waziri atatusaidia kwa faida yetu na kwa faida ya wananchi katika kutafuta taaluma ya kupata madaktari Wazalendo.

Mhe. Naibu Spika, la tatu hili wachangiaji wengi sana wameliongelea na mimi naona niligusie kidogo nalo ni eneo la Mnazi Mmoja. Hapa ni lazima tuseme ni lazima tuiambie serikali hususana katika hospitali yetu hii. Hospitali imekuwa na msongamano mkubwa sana, kwa sababu tunaelekea katika hospitali ya Rufaa. Kuna rai ningeomba nimsaidie Mhe. Waziri juu ya kufanya upanuzi wa Hospitali. Msongamano umekuwa mkubwa, ikiwezekana baadhi ya vitengo viondoshwe.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ifikirie kujenga maeneo ya ziada, maeneo tunayo pembezoni mwa kiwanda chetu cha madawa kuelekea Maisara. Angalau kuna baadhi ya vitengo kama ndugu zetu wa *TB*, au majengo ya watoto tukajenga katika maeneo mengine ili

kuondosha msongamano katika hospitali ile. Zaidi niseme kwamba kila mtu kasema hospitali yetu ndio kimbilio la watu wengi. Mimi nasema hospitali ya Mnazi Mmoja ni kimbilio la wanyonge. Kuna haja ya kuiangalia kwa umakini sana. Mwenye pesa zake Hospitali ya Mnazi Mmoja haendi, lazima tuseme ukweli. Haendi kwa sababu huduma duni.

Mhe. Naibu Spika, lazima tukiri sasa hivi. Kama utakwenda Bandarini kila siku basi maiti wanaotoka Dar-es-Salaam wamekuwa wanaongezeka siku hadi siku. Hii inatokana na kwamba watu wengi wametoka imani na kupeleka wagonjwa Mnazi Mmoja. Kufa ni wajibu lakini watu sasa hivi mauti yao wanaona bora wakafie bara. Kwa sababu unakufa katika hali ambayo unajiridhisha, lakini Mnazi Mmoja hujiridhishi. Sasa hivi ukikaa Bandarini, ukikaa Airport kila siku vitengo hivi maiti wanamiminika. Tuiyombe Serikali yetu ijitahidi.

Wenzangu wameangalia baadhi ya vitengo lakini the all most Hospitali nima ina matatizo. Ukiangalia wazazi matatizo, ukiangalia vitengo vya wagonjwa wa sukari matatizo. Mimi nasema Mhe. Makamo alishtukiza lakini kuna haja Mhe. Waziri angekaa kama siku tatu. Sasa hivi sisi viongozi imekuwa tuna namba za simu za madaktari wote pale. Mimi kiongozi nina namba za madaktari aliyekuwa sio kiongozi namba ya daktari haipati. Au hana uwezo wa kwenda kuchukua daktari. Ili mtu atibiwe mfate daktari. Tunazijua nyumba za madaktari wote sasa hivi. Tunamjua daktari wa Mwanyanya nani, daktari wa Nyerere nani, mgonjwa anafika kufuata huduma anakaa si chini ya masaa 6 daktari anatafutwa hapatikani.

Mhe. Naibu Spika, tutasema mengi katika hapa. Kila mtu akizungumza ataliogolea suala la Mnazi Mmoja. Tuna nia njema serikali ina nina njia, jitihada zipo. Mheshimiwa tunaomba tuitizame kwa jicho la huruma ili tuwasaidie wananchi wetu waliowanyonge ambao kuwa hospitali ile ndio kimbilio lao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja mia kwa mia, mimi na kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Kwahani. Ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Naibu Spika, kwanza nitoe shukurani zangu za dhati kukushukuru wewe. Pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake hii ya bajeti ya Mapato na Matumizi kwa Wizara yake ambayo ameisoma mbele yetu kwa staili ya kipekee, alikuwa akishusha na kupandisha kwa staili yake peke yake. Kwa hili tumpongeze.

Pia nisiwasahau watendaji wake kama alivyowapongeza yeye mwenyewe na mimi nichukue fursa hii kuwapongeza kwa kazi nzito ambayo wamemsaidia mpaka kufikia kuwasilisha hotuba yake.

Mhe. Naibu Spika, na mimi kama walivyochangia wenzangu kwanza nichukue fursa hii nichangie Hosptali ya Wete ambayo mimi mwenyewe nimezaliwa pale. Nitakuwa ni mwizi wa fadhila kama sikuchangia hospitali ile pale. Ipewe *privilege* zote kila kinachostahiki pale kipatikane ili wananchi wa pale wafaidike na matunda yao ya mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, niende kituo changu cha Sebleni kwa kuwa ni kituo ambacho kipo katika Jimbo langu. Mbunge wangu walikuwa ana nia tujenge hospitali katika jimbo letu. Lakini kwa kuwa jambo hili linakwenda na watu na wenzio na kutafuta maamuzi au ushauri. Ushauri tulioupata ni kwamba hospitali zipo nyingi na hata tukijenga hospitali wafanyakazi hakuna. Lakini tuliufuata ushauri huo kutoka kwa Katibu Mkuu ni kwamba vituo vilivyoko katika jimbo letu tuvipe ushirikiano. Mhe. Naibu Spika, kwa vile jirani yangu wa Kwamtipura ana hospitali hapa tumeshazungumza hivyo tuingie pale kwa kuzisaidia kwa hali na mali tukishirikiana pamoja na serikali kuu.

Mhe. Naibu Spika, jengine nitofautiane kidogo na wenzangu kuhusu suala la wauguzi. Kwa kweli hawa watu wanastahiki pongezi za

kutosha, tusiwe na ile ya kwamba tukitoka majumbani mwetu tunatoka na hisia kuwa wauguzi ni wajuba kumbe na sisi wenyewe tunatoka majumbani tukiwa ni wajuba. Mimi mwenyewe Mhe. Naibu Spika, nimezaa mimba nane za hapo kwa hapo, lakini sikupata kunyukuliwa wala kutolewa maneno pale hospitali.

Mhe. Naibu Spika, mimba yangu ya mwanzo nimezaa mwaka 1977 nikiwa na umri wa miaka 17 na mimba yangu ya mwisho nimezaa kwa *scissors* mwaka 1990. Kwa hivyo, kipindi chote hicho nimefika pale hospitali nikiwa na bembelezwa. Siku ile niliyozaa mtoto wa mwisho ambaye nimepata matatizo nilionekana kwamba siwezi kuzaa na mtoto alikuwa ni mkubwa sana alikuwa ni 4.2, lakini kwa usaidizi wa madaktari nikaweza kujifungua mtoto yule. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli uchungu ulikuwa ni mkali sana, lakini hata hivyo nilisaidiwa na mtoto yule yuko hai kabisa juu ya matatizo yote yaliyonipata.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli nilikuwa nabembelezwa walikuwa wananisemesha ili nisipate matatizo, mara walikuwa wananiuliza jina langu, unakaa wapi mpaka nimempata mtoto yule. Kwa kweli wenzetu wana kazi kubwa sana ni lazima tuwapongeze. Mhe. Waziri mimi nataka nikwambie kwamba hapo utakapokwenda kusema nao hawa wafanyakazi useme nao kipolepole kwani hawana matatizo yoyote na sisi wenyewe wananchi tunayo matatizo hayo.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine niseme kuhusu huduma za mama na hasa hawa akina mama wajawazito. Mimi nasema hii michango tungeielekeza kwengine kwa sababu tukiwaelekezea kina mama kama walivyosema wenzangu kuwa hali ni ngumu, na tokea unachukua mimba ile unakuwa unagharamika na hakuna msaidizi. Mhe. Naibu Spika, huko nyuma zamani tulikuwa tunaona na serikali ilipokuwa na uwezo tusiikoseshe shukurani, kwani tulivyoanza huko nyuma na sasa hivi ni tofauti. Mhe. Naibu Spika, mama wajawazito ilikuwa wanapokwenda kupima huwa wanarudi na maziwa, lakini leo kutokana na hali ya uchumi tukubaliane na hilo.

Mhe. Naibu Spika, mimi simjibii Mhe. Waziri lakini jamani tuitizameni na hali yetu ilivyo sasa hivi. Kwa hivyo, mimi naomba tahfifu kidogo kuhusu suala hili la kuwachangisha mama wajawazito, hali inakuwa ni ngumu na mpaka pale unapofika kujifungua huwa unahitaji urejeshe hali yako kwa sababu umeshapoteza damu nyingi, umeshatumia uwezo wako mwingi. Kwa hivyo, hapa inakuwa unahitaji tena nguvu zako.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile wenzangu wameshachangia sana sitokuwa na mengi kuhusu haya isipokuwa wauguzi na wao tuwape sifa zao. Mhe. Naibu Spika, tumeona huko nyuma mataifa mengine wana hali ngumu, mishahara haitoshi lakini bado unawakuta wanafanya kazi na hawa wa hapa kwetu wanastahili sifa na wao wapewe. Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi nichukue fursa hii ya kukupongeza na naunga mkono hoja hii mia kwa mia kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuweza kuchangia mawili matatu. Pia natoa pongezi kwa Wizara ya Afya kwa kuwa na malengo ya kuendeleza afya ya jamii ya kinamama na watoto kwani ndio wenye matatizo makubwa ya kiafya.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la kuzipandisha daraja Hospitali ya Kivunge, Micheweni, Vitongoji, Wete na Abdalla Mzee Mkoani ni jambo la faraja sana kwani wananchi wa maeneo hayo pamoja na majirani zao watapata kufaidika. Mhe. Naibu Spika, ombi langu kwa wizara ni kwamba wakati wa utekelezaji wa mradi huu pia wahusishwe upatikanaji wa wataalamu wa afya, vitendea kazi na madawa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mpango wa serikali kupiga vita malaria hiyo ni hatua nzuri iliyofikiwa hivyo serikali iweze kuzidisha mapambano dhidi ya malaria. Hata hivyo, bado kuna haja ya kutolewa elimu ya afya ili wananchi waweze kuweka mazingira katika hali ya usafi. Mhe. Naibu Spika, nizungumzie magonjwa ya

kisukari na *pressure* magonjwa haya bado yanaendelea sana hapa kwetu Zanzibar. Je, wizara ina mikakati gani kwa kukabiliana na tatizo hili ambalo linahatarisha maisha ya wananchi wetu hapa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia naomba kuunga mkono hoja.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili nikaweza kuchangia. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii nikaweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya. Natoa pongezi kwa Mhe. Waziri wa Afya pamoja na Naibu wake na watendaji wake wote nasema hongera, lakini na pole.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nitaanza na Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja japokuwa wajumbe wengi wameizungumza, lakini na mimi nitatoa mchango wangu.

Mhe. Naibu Spika, Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja inakabiliwa na matatizo ya mrundikano wa wagonjwa wengi, hivyo serikali ifanye bidii kumalizia ujenzi wa hospitali ya Mpendae, Kwamtipura kwa Wilaya ya Mjini na Mbuzini kwa Wilaya ya Magharibi. Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na mrundikano huo wa wagonjwa pia hospitali hiyo inakabiliwa na matatizo ya uhaba wa vitendea kazi na madaktari kuhudumia wagonjwa wengi na hivyo kushindwa kupata muda wa kupumzika.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika Chuo cha Afya Mbweni, chuo hiki ni muhimu kwa kuwaandaa madaktari na wauguzi wetu wa baadae. Mimi naiomba wizara wakipe umuhimu wa kuwa na upendeleo maalum kwa wanafunzi wa kike wale ambao wazee wao hawana uwezo wa kuchangia. Mhe. Naibu Spika, mimi naiomba wizara ichukue dhamana ya kuwasomesha wanafunzi hao hata kama watakuja kulipa watakapoajiriwa.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika Ofisi ya Mkemia Mkuu wakati umefika kwa ofisi hii ya Mkemia Mkuu kuimarishwa kwa kupatiwa

jengo jipya na vitendea kazi. Aidha, ofisi hii ishirikiane na Bodi ya Chakula, Madawa na Vipodozi. Kwa sababu udhibiti wa uingizaji wa bidhaa zilizokuwa na viwango nchini kwa kuzingatia wananchi wetu wengi wameathirika kwa kutumia baadhi ya bidhaa zilizopitwa na wakati na nyengine ambazo hazina viwango.

Mhe. Naibu Spika, vile vile niende katika hospitali ya wagonjwa wa akili. Mhe. Naibu Spika, kati ya wagonjwa 790 waliolazwa wanawake ni 440 na wanaume ni 350 na kwa upande wa huduma za nje jumla ya wagonjwa ni 8,484 waliopatiwa matibabu katika hospitali hiyo ni kati ya hao wanawake walikuwa ni 4,364 na wanaume ni 4,120. Mhe. Naibu Spika, inaonesha hapa kwamba wanawake ndio wengi wanaohitaji uangalifu maalum. Mhe. Naibu Spika, mimi natoa ombi langu kwa Mhe. Waziri kwamba aendeleze kuimarisha hospitali hii ya wagonjwa wa akili.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia namuomba Mhe. Waziri wa Fedha bajeti hii kwa kipindi kijachoaiongezee fungu Wizara ya Afya iweze kutekeleza majukumu yake waliojipangia kwa ufanisi zaidi. Mhe. Naibu Spika, na mimi naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hii ya Afya katika hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Mhe. Naibu Spika, kwanza nitoe shukurani za dhati kwa Mwenyezi Mungu kunijaalia leo kuchangia hotuba hii ya bajeti ambayo nimsifu Mhe. Rais Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuiona umuhimu wake na kumchagua Mhe. Juma Duni Haji kuwa Waziri wa Afya na Naibu Waziri wake Dk. Sira Ubwa Mamboya na Katibu Mkuu wake kuwa ni mtaalamu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais amefanya hivyo kwa makusudi kwa kujua umuhimu wa taasisi hii ambayo moja kwa moja inalenga maisha ya binadamu. La pili Mhe. Naibu Spika, nitoe shukurani za dhati kwa Mhe. Waziri kwa namna alivyokisoma kitabu chake kwa *speed* kubwa lakini kwa uwazi na kufahamika.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanza kuchangia ni kuwa matibabu ni kitu muhimu sana duniani, lakini nilipoangalia kitabu hiki nimesikitishwa kuona kuwa katika fani tofauti za madaktari waliopo ni jumla ya madaktari 1,178 na wakati mahitajio ni 2,543 ikiwa kuna upungufu kwa madaktari 1,365 wa fani mbali mbali. Hii ni hatari hivyo pamoja na sifa yote niliyoieleza hapo mwanzo lakini kuwa hii ndio hali waliioirithi, mheshimiwa ni kusema kwamba tuna matatizo makubwa katika sekta hii ya tiba, pamoja na mambo mengine yanayohusiana na mambo ya afya.

Mhe. Naibu Spika, ninaloomba ni kuwa kwa sababu mapengo haya ni lazima yajazwe na kwa sababu kuna sababu kadhaa zilizosababisha wengine wakaondoka mpaka hali ikazidi kuwa mbaya kuliko hivi. Kwa hivyo, ningeliomba tena kwa heshima zote kwa umuhimu wake wizara hii ionekane kuwa kutafutwa sababu ili pengo hili lijazwe na wale waliopo wabakie na kubakia kwao ni kuongezewa maslahi.

Mhe. Naibu Spika, jambo la pili ni kwamba tumemuona Mhe. Waziri mara tu baada ya kupata wadhifa huu kaondoa kero kubwa na muhimu kabisa kwa Pemba na Unguja na hili ni tatizo la maji lilokuwepo kwa hospitali zote, hili nampongeza sana. Mhe. Naibu Spika, ilivyo tukimuona Mhe. Waziri anafanya kazi kiasi hiki pamoja viongozi wake walioko chini yake na sisi watendaji wajibu wetu ni kuwa tuige, lakini linalonisikitisha ni kuwa pamoja na juhudi yake kazi ya kiutendaji niseme kuwa hairidhishi hata kidogo.

Mhe. Naibu Spika, ni hivi juzi tu kulitokea tatizo dogo kule Hospitali ya Mnazi Mmoja na ikabidi niende baada ya kipindi cha kwanza hapa. Mimi nilisikitishwa tena sana kweli kweli kuona kuwa hawa baadhi ya watu wetu wanaohusika na matibabu hawako makini kwa kuona ni lazima ubinadamu utendeke kwa baadhi ya wakati.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na mtu aligongwa na gari saa 8 mchana na saa 9 alifikishwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa sababu

ya matibabu na alikuwa amezimia hasemi. Nasikitika kusema kuwa na shahidi wangu alikuwa ni Mhe. Mtando tulikuwa pamoja mgonjwa huyo hakushughulikiwa isipokuwa wale waliofika na mgonjwa walilazimishwa kwanza watoe shilingi 50,000 na shilingi 50, 000 ni pesa nyingi sana kwa masikini na walikuwa hawana ikabidi waeke simu yao rehani.

Mhe. Naibu Spika, basi ukafanywa uchunguzi wa mwanzo kwa bahati mbaya baada ya kupata matokeo ikabidi mgonjwa yule abakie mpaka siku ya pili, hajenda kufanyiwa uchunguzi tena na ilikuwa ni lazima apelekwe kwenye *city scan* kwani hali yake ilikuwa ni mbaya sana. Mhe. Naibu Spika, pamoja na umasikini wao ilibidi mgonjwa yule abakie mpaka siku ya pili na sisi mnamo kiasi cha saa 8 tulipofika pale ndio kwanza anatoka kupiga *city scan* na wale wauhusika wa yule mgonjwa wakalazimishwa kutoa shilingi 100,000.

Mhe. Naibu Spika, mpaka jana nilipouliza niliambiwa kuwa yule mtu amepasuka kichwa, damu imeingia kwenye ubongo na pamoja na kuwa hospitali yetu ina uwezo wa kufanya upasuaji wa kichwa lakini kwa hilo haliwezekani tena na ni lazima apelekwe Dar es Salaam. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hii nikusema kuwa daktari ni mtu muhimu sana na hali yetu tunaijua wakati mwengine lazima ubinadamu utumike. Mimi najua city scan imewekwa pale kwa wenye uwezo walipie kwa sababu inaweza ikaharibika wakati wowote na kufanyiwa matengenezo, lakini tulipoelekezwa ni kuwa kwa yeyote ambaye hana uwezo asaidiwe kwa sababu ya kuokoa maisha yake. Lakini hili ndilo lilotokea wala nisije nikaulizwa kwa kutoa ushahidi kwa sababu jina ninalo na wazee ninao, na mimi baada ya kushughulika lakini ikawa hatuwezi kulitatua tena, tena wale madaktari wakawaita mbona wakubwa wanafika hapa pana nini, sisi tukaondoka tukaja zetu.

Mhe. Naibu Spika, hii namueleza Mhe. Waziri ndio hali ya baadhi ya waganga wetu katika hospitali zetu. Kwa hivyo, juhudi yao yote lakini inakwamishwa katika utekelezaji. Hilo ni moja mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, jambo la pili ninalosikia katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja ni kuwa wodi ya wanawake ni ndogo kuliko wagonjwa wanaolazwa katika wodi ile. Mhe. Naibu Spika, hulazimika wagonjwa kulala zaidi ya mmoja katika kitanda kimoja na kwa bahati mbaya na wajawazito wamo humo humo, na bahati mbaya hutokea siku nyengine hata mtu akajifungua katika wodi ile ya wanawake. Kwa hivyo, kama hili ni kweli ningeliomba Mhe. Waziri aone kuwa iko haja yakufanya upanuzi wa wodi hii ya wanawake ili mambo haya yasiendelee kutokea kwani ni ya kutisha.

Mhe. Naibu Spika, niliposoma katika ukurasa wa 10 niliona kuwa idara hii ya uendeshaji na utumishi katika kipindi kilichopita kifungu cha (h) moja katika kazi zake ilikuwa ni kusimamia ujenzi wa majengo mapya yaliyojengwa na wizara pamoja na yale yaliyojengwa na wadau mbali mbali. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kwa vile sisi ni wawakilishi tumechaguliwa na ni lazima tuangalie matatizo yaliyomo katika majimbo yetu na tusaidie pale tunapoweza kusaidia, mwengine tumejitahidi katika majimbo yetu kuwajengea wananchi wetu kwa kushirikiana nao kujenga vituo vya afya angalau kupunguza masafa. Mhe. Naibu Spika, hapa imeandikwa kusimamia, na kusimamia inaweza ikawa na maana tofauti. Mimi ningeliomba kusimamia huku ni pamoja na kusaidia au ni kuona shughuli inakwenda au wanasimamia kwa utaalamu wao tu hawasaidii chochote.

Mhe. Naibu Spika, tumejenga vituo na tulipokuwa tukiuliza maswali hapa majibu tulikuwa tukiyapata takriban ni kwamba hatukushauriwa kwanza hivyo, Wizara ya Afya haitusaidii. Mimi ningeliomba kujua hilo kwani nimepoteza fedha nyingi sana kwa kituo cha Bwagamoyo na Mhe. Waziri katika bajeti yake kubwa hata kukitaja. Mhe. Naibu Spika, mimi nikitaka kujua serikali au wizara ina msimamo gani kuhusu kituo kile.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile tunaogopa kuanza napenda kupitia kwako mheshimiwa kuleta tatizo langu la Kisiwa cha Kokota

ambacho kiko mbali sana na Mtambwe pia kiko mbali sana na Wete. Mhe. Naibu Spika, hata Wizara ya Elimu nawashukuru imeshaanza kujenga jengo kule na inshaallah wanasema safari hii wataliezeka kwa mahitaji ya watu walioko kule wana visiwa. Kwa bahati mbaya kule hakuna kituo cha afya, na kwa vile tumepewa indhari tusianzishe kwa kutegemea wizara itusaidie. Mhe. Naibu Spika, kwa kupitia kwako naomba rasmi kwamba wale watu tena kwa heshima zote wanahangaika hawana pakwenda basi naomba wasaidiwe angalau kupatikana kituo kidogo tu.

Mhe. Naibu Spika, jengine ninalotaka kuzungumza ni kuwa wizara kwa kupitia kitabu chake inatoa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya kanuni na taratibu za kazi ili zieleweke kwa wafanyakazi wote. Mhe. Naibu Spika, hii taarifa ni nzuri lakini kutoa mafunzo ni jambo moja na mimi nisingalipendelea kuwa mafunzo haya yaeleweke tu kwa watendaji, lakini hayo mafunzo yatafsiriwe kwa vitendo. Mhe. Naibu Spika, yakitafsiriwa kwa vitendo naamini mashaka yote haya yaliyopo yanaweza yakapungua na pia ni wakati umeshafika wizara iweke taratibu zake za kanuni kwa yule ambaye kwa makusudi kabisa atasababisha kifo cha mgonjwa wakati uwezo wa kumtibu anao, hivyo zichukuliwe hatua.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nizungumze kuhusu Hospitali ya Wete, mimi nashukuru kitabu kimeeleza kuwa tumeletewa *x-ray* mpya tena ya kisasa na inafanyakazi vizuri. Lakini nililoshuhudia ni kuwa mtu akienda kupiga *x-ray* matokeo huwa anayapata siku ya pili au siku ya tatu. Je, ni kwa sababu ndio inavyofanyakazi au ni kwa kukosekana mtaalamu wa kusoma matokeo ya *x-ray*. Hilo naomba nije nielekezwe.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika Hospitali ya Mkoani pamoja na kuwa humu imeandikwa katika mambo yatakayofanywa ni kujengewa wodi ya watoto. Mhe. Naibu Spika, ile ndio hospitali yetu kubwa na ile ndio hospitali yetu tegemezi. Mhe. Naibu Spika, kauli hii haijatoka leo siku zote tunapokuja hapa tunaambiwa kuwa Hospitali ya Mkoani kutajengwa wodi ya watoto mpaka kiwanja

tumeshakwenda kuoneshwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa umuhimu wake ho spitali ile ilivyo hili suala safari hii litekelezwe.

Mhe. Naibu Spika, katika Hospitali ya Wete tunapokwenda kutibiwa wengine huwa kwa bahati mbaya au ndio Mwenyezi Mungu alivyokwisha mjaalia hupoteza maisha, nasikia tu kwamba kuna chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Wete lakini sijaona kuhifadhiwa maiti. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba maiti wote huwa wanakufa kwenye wote na kuwachukua kuwapeleka kunakohusika kwa wale waliokuwa wanatuhusu. Mhe Naibu Spika, mimi ningeliomba kujua hali ya chumba hicho cha kuhifadhia maiti iko vipi mpaka ikawa haitumiki.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho ni kuwa mazingira ni magumu na siku hizi tunapata wagonjwa wengi sana na wagonjwa wengine ni kwamba hospitali tulizonazo katika majimbo yetu ni vituo tu vidogo vidogo basi. Mhe. Naibu Spika, kama mimi nina vituo vitano lakini vyote ni hivyo hivyo vidogo. Wakati mwengine hulazimika mgonjwa apelekwe ama Chake-Chake au Mkoani. Najua hospitali ya Wete inayo gari ya kuchukulia wagonjwa, lakini ni adimu sana kupatikana gari hii na mgonjwa kumtia katika gari ya abiria sivyo, kiutaratibu ni lazima aingizwe katika gari ile ya wagonjwa na daktari kwa sababu lolote linaweza kutokea. Kwa bahati mbaya gari zetu zinazowahudumia wagonjwa mpaka wazazi washazaa katika gari hiyo, lakini sisi sio wakunga lakini ndio haya tu tena tunakimbia hospitali na wakati huku keshazaa. Ningemuomba Mhe. Waziri kwamba wakati gari zipo basi zitiwe mafuta ya kutosha ili ikitokezea kesi yoyote ya haraka liweze kutumika kwa manufaa ya wagonjwa wetu.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie kuwa yote Mhe. Waziri aliyoyaandika humu yafanikiwe, pamoja na kuwa alisahau kuongeza neno Mwenyezi Mungu nisaidie katika kitabu hiki kitukufu, ahsante.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii kwenye kipindi hiki cha sala ya Magharibi. Pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na hatimaye nimpongeze Mhe. Waziri kwa kitabu chake kikubwa na kizuri na chenye lugha fasaha ya Kiswahili. Hii ni kazi nzuri anayoifanya yeye binafsi pamoja na watendaji wake, kwa ujumla niwapongeze wote. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze na Hospitali ya Abdalla Mzee ambayo ni hospitali yetu kubwa katika Wilaya ya Mkoani na mara nyengine inachukua wagonjwa takriban kutoka wilaya zote za Pemba. Siku chache kabla ya kuja huku Unguja nilikwenda hospitali ya Abdalla Mzee kuwatizama wagonjwa, niliingia kwenye chumba ambacho kinaitwa ni wodi ya watoto, lakini sio ya watoto bali wamewekwa watoto tu kwenye wodi ya wanawake wanakaa. Kila kitanda nilichokwenda ambamo kuna vitanda sita kina watoto zaidi ya wawili waliolazwa katika kitanda kimoja. Kila mtoto ana mama yake. Kwa hivyo wagonjwa ni watatu na mama zao ni watatu, watoto hawa kila mmoja ana magonjwa yake.

Mhe. Naibu Spika, ule msemo maarufu wa afya umekwenda kinyume nyume, kuwa ‘kinga ni bora kuliko tiba’, kwa hapa naona tiba ni bora kuliko kinga. Kwa sababu wale kila mmoja ana magonjwa yake na wengine pengine yule anaharisha na yule ana magonjwa pengine ni ya kuambukiza na wamewekwa katika kitanda kimoja. Kwa hivyo, kuna uwezekano mkubwa wa kuambukizana magonjwa, isitoshe magodoro yenyewe ni mabovu hayafai na bado wanalazwa wagonjwa waliokwenda pale kupata tiba.

Mhe. Naibu Spika, ile dhana ya Muuguzi Mkuu wa Dunia *Florence Night Engle* imekiukwa. Tunauguza kienyeji enyeji tu, hatuuguzi katika maadili ya kihospitali. Kwa sababu haiwezekani, au sio vizuri, kwa sababu ndio imeshawezekana, kitanda kimoja kulazwa mgonjwa zaidi ya mmoja.

Mhe. Naibu Spika, halafu nikenda upande wa wazazi. Kwanza nilikuta kitanda kimoja kina wazazi wawili na kuna mmoja kajifungua watoto wawili mapacha, yeye nafasi yake kapata chini, kwenye saruji pale, nitatumia Kiswahili katandika mbacha, pale ndipo alipolazwa mgonjwa huyo.

Mhe. Naibu Spika, hii maana yake nini, maana yake bado ile hospitali haijakuwa na nafasi ya kutosha ya kuweza kukidhi mahitaji ya wagonjwa wanaokuwepo. Mara moja nilimsikia Mwalimu Nyerere akisema baadhi ya matatizo yetu yanatokana na maendeleo yetu. Sasa ile dhana ya wananchi kushajihishwa na kuelimishwa kwenda hospitali ilifanywa kama ni maendeleo. Kwa sababu nafasi haitoshi, baada ya kuwa tunaendelea sasa kunasababisha matatizo, kwa sababu ndio inafikia pahala kitanda kimoja kulazwa zaidi ya mtu mmoja. Kwa dhana yangu mimi nadhani sio vizuri.

Mhe. Naibu Spika, iko haja kama Mhe. Waziri alivyoeleza humu kuwa anataka kujenga wodi ya watoto. Ningeomba ijengwe tena iwe kubwa kidogo, iweze kuwahudumia watoto wengi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, hospitali hii inataka kupandishwa daraja, lakini 'isijeunga kimo kwa kinu'. Ipandishwe daraja ikiwa ina mahitaji ya kufikia hiyo hatua ambayo inataka kupandishwa. Kwa sababu hivi sasa pamoja na kuwa ni hospitali ya Wilaya ya Mkoani, lakini wodi nyingi utakazopitia kwa wanawake na kwa wanaume basi utawakuta wagonjwa ama wanatoka Kaskazini, Chake-Chake na kwengineko, sio watu wa Mkoani peke yake waliokuwemo mule. Kwa hviyo, hospitali ile imekaa kama ndio hospitali kuu ya Pemba, kwa hivyo ikipandishwa isipandishwe kinadharia, ipandishwe kikweli ili ile dhana iliyokusudiwa na Mhe. Rais iwe ni ya kweli, isiwe ni ya kubeza tu.

Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi ni wajanja. Wakati Mhe. Rais wa Awamu ya Tatu wa Tanzania alipokuja alitembelea hospitali ile ya Abdalla Mzee, kwa wakati huo ilikuwa hakuna madawa, lakini ikawa sasa anakuja Rais na hospitali kavu watu wafanye nini. Mhe.

Waziri watu walichukua maboksi matupu ya madawa yaliyokwisha dawa yale wakaweka kwenye ma-rafu yale. Akaambiwa Rais kuwa hapa hatuna tatizo lolote. Mara nyengine hatua kama hizi ni nzuri tunajenga kuwa tuko tayari, lakini mara nyengine tunajidumaza, kwa nini tusiseme ukweli. Kwa sababu wewe Mhe. Waziri au Mdhamini wa hospitali dawa huleti wewe, kwa nini uogope kusema kuwa dawa hazipo. Mhe. Naibu Spika, ningeomba katika utendaji wetu pia watu wetu tuwe wakweli, kwa sababu ile kudanganya mara nyengine inatukosesha baadhi ya fursa.

Mhe. Naibu Spika, nije katika changamoto kwenye maradhi haya yaliyoibuka ambayo sio ya kuambukiza ya kisukari, saratani, moyo na kibovu cha mkojo. Magonjwa haya hivi sasa zaidi kule kwetu Pemba yametawala ama mtu atakuwa ana hili au ana lile. Ana hiki au ana kile. Kwa hivyo, ningeomba wizara ifanye utafiti, kuna nini. Magonjwa haya zamani yalikuwa ni nadra, lakini leo yamekuwa ndio magonjwa mashuhuri kabisa. Kila unayemuona *pressure 200*, kila unayemuona hanywi chai ana sukari. Chanzo chake au matatizo haya ilikuwaje, maana yameibuka kwenye hii miaka ya karibuni hivi, huko nyuma magonjwa haya yalikuwa ni nadra sana tena sana.

Mhe. Naibu Spika, nije katika kifungu ambacho kinazungumzia kusimamia masuala ya ajira na zile haki na maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Naibu Spika, kama tulivyoona kuwa wizara hii ina upungufu mkubwa sana wa watendaji. Kwa hivyo, tungeiomba wizara hii iajiri ili tupate madaktari wazalendo watakaoweza kubakia kuhudumu katika hospitali zetu.

Kwa mfano hospitali ya Abdalla Mzee tokea ilipoanzishwa mwaka 1969 hadi hii leo hakuna Mzanzibari aliyekuwepo pale kuwa yeye ndiye daktari bingwa, mara zote mabingwa ni Wachina. Ni kweli wameijenga wao na kweli wanatusaidia, kwa nini hatufanyi maarifa na sisi tukawasomesha vijana wetu ili wakabakia madaktari hawa wakawa ni wa kwetu. Pengine inatokana na hii sehemu ya pili. Kabla sijafika huko.

Mhe. Naibu Spika, hii ajira tuwaajiri watu kulingana na mahitaji na fani husika, kwa sababu katika vituo vingi vya shamba kwa kweli wahudumu, *red cross* ndio wanaochukua nafasi ama za kutoa dawa, za kupiga sindano na kwa pale hospitali ya Abdalla Mzee hata mara nyengine huwa wanasimamia kuweka *drip*.

Mhe. Naibu Spika, zamani ukitaka kumchoma mtu sindano, basi ilikuwa mara nyengine kuna daktari mwengine kakaa akiba na ikitokezea kesi ya dharura, kwa sababu kuna wengine baadhi ya dawa inapoingia mwilini zinawadhuru na pengine hata kuanguka, wengine kama dawa ya PPF inawadhuru. Kwa hivyo, mchomaji anaweza akamchoma mgonjwa kisha mgonjwa akaanguka yule mchomaji akahumiwa, sasa kungekuwa kuna daktari mwengine wa akiba wa kuweza kuiokoa ile hali. Hii sio kwa kubahatisha, mimi

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika tano.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Du! Haya. Mhe. Naibu Spika, mimi mara moja katika kung'oa meno, nilikwenda hospitali daktari mmoja ananing'oa na daktari mmoja kakaa akiba. Baada ya muda kidogo nilijiregeza kidogo, basi yule daktari wa akiba alimgeuza yule daktari na akawacha vyombo vyake akaniita Mohammed, Mohammed. Nikanyamaza kimya. Baada ya muda kidogo nikaitika naam! Kwa kweli hivi ndivyo ilivyokua. Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo *red cross* wanachoma sindano, hana mafunzo yoyote, lakini anafuatana tu na daktari inafika pahala unaona na yeye anatibu, tumefika pabaya.

Mhe. Naibu Spika, kumetajwa habari ya haya majengo, nashukuru katika jimbo langu ambalo lina wodi tatu, kila wodi Kengeja, Mtambile na Kangani zinavyo vituo vya afya. Kengeja kituo kizuri kipya kimejengwa hivi karibuni na mpaka naondoka ilikua hakijahamiwa, lakini ilikuwa kimemaliza. Kwa hivyo, ningeombwa kifanywe haraka ili kihamiwe kwa sababu hivi sasa watu wanapata huduma finyu sana. Kwa kule Kangani ningeomba kile kituo

kikuzwe kwa sababu ni kidogo mno, hata zile huduma za mama na mtoto mara nyengine hazipatikani.

Mhe. Naibu Spika, zamani ilikuwa elimu ya afya inatolewa kwa wingi. Mimi binafsi nilipokuwa nikisoma, basi kila wiki ilikuwa madaktari wanapita maskuli ili kutuelimisha na hii iliweza kuondoa magonjwa kadhaa kupitia elimu ya afya maskuli. Kwa hapa imetajwa lakini ningeomba iendelezwe.

Mhe. Naibu Spika, huko nyuma niliomba kutokana na haki yangu mimi ya usemaji ni mbovu, kwa hivyo niongezewe lakini haijakubalika. Naomba nimalizie hapo na niunge mkono hoja ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa na afya na uzima na kuweza kufika wakati huu na kutekeleza majukumu yetu na kuchangia bajeti hii muhimu yenye maisha ya wanadamu.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitokuwa na mchango mkubwa kwa sababu mengi yameshasemwa sitoweza kurejea rejea. Mhe. Naibu Spika, mimi mara nyingi wakati nikichangia bajeti zilizopita, nikiingia katika bajeti ya Wizara ya Afya na bajeti ya Wizara ya Elimu, basi hupenda sana kukariri maneno ya mshahiri mmoja, mshahiri huyu aliyetunga kitabu kinachoitwa taalim. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, mshahiri huyu ana shairi lake zuri anasema *Innal Muaalima Watwabiba Kilaahuma. Layaansihami Idhlam Yukrim.* Hakika ya mwalimu na daktari wawili hawa hawanasihiki ikiwa hukuwatukuza.

Mhe. Naibu Spika, ubeti huu ni muhimu sana tena ni umeti wa kuukariri kila wakati, endapo hatukuwatukuza madaktari wetu ndio pale wanapotuambia kaeni na maradhi yenu na wakututibu hatuna.

Naomba Mhe. Waziri japo ongezeko la asilimia 50 kwa madaktari wetu, bado ipo haja ya kuangaliwa tena.

Mhe. Naibu Spika, tutakapowajali madaktari hawa basi hizi kelele zote mimi nadhani zitaondoka. Kwamba wana lugha chafu, hawahudumii wagonjwa ipasavyo, pengine hakuna tatizo, tatizo ni hili tu. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla najua huu ni mzigo wa serikali. Mimi siku zote nilikuwa nikisema hapa nikimwambia jirani yangu kuwa 'mzigo mzito hutikwa Mnyamwezi', lakini katikwa babu Duni sio Mnyamwezi. Tunamuonea huruma babu Duni kutikwa mzigo huu mzito. Kwa hivyo, tunaomba masilahi ya wafanyakazi yatizamwe ya madaktari wetu. Matatizo yote haya yataondoka.

Mhe. Naibu Spika, kwa haraka haraka nije katika huduma za mama mjamzito. Katika kitabu hiki cha Mhe. Waziri amesema kwamba Baraza lililopita lilizua mjadala mkubwa katika uchangiaji wa upasuaji wa mama mjamzito, kweli na yeye alikuwa ni muumini mkubwa wa suala hili. Swahib yangu mkwe wangu Mhe. Said Ali Mbarouk alikuwa muumini mkubwa wa suala hili na kwa makelele. Mhe. Hamad Masoud alikuwa muumini mkubwa wa hili lilizua mjadala kweli. Lakini kunyamazika kwa bajeti hii sio kwamba tumeridhia bado hali ngumu ya wananchi wetu ipo, ipo hivyo naomba suala hili liangaliwe tena. Hali ni ngumu sana hawamudu wananchi wetu kuchangia Shs. 40,000/= za upasuaji.

Mhe. Salmin Awadh alisema hapa kwamba asilimia kubwa inaonekana kujifungulia majumbani kwa tatizo hili. Tarehe 20 ya mwezi uliopita Mhe. Waziri asubuhi majira ya saa mbili na nusu, nimeshavaa natoka nje nakuja zangu kazini, kufika mlangoni namkuta mama yuko chini ya mlango wangu, ananipigia magoti ananiambia naumwa nipishe ndani. Katoka masafa marefu anafukuzia hospitali, maskini pesa ya daladala ya kufika Mnazi Mmoja hana, nikafungua mlango nikamuweka ukumbini kwangu. Kilichonipata, amakweli ujuzi uwe nao na mawazo japo kidogo yatakusaidia. Sijawahi kupokea mzazi, yaani sijapokea mtoto hata

siku moja. Tarehe 20 nilimpokea mama mjamzito nikampokea mtoto wa kiume.

Mhe. Naibu Spika, mwaka 1993 alikuwepo daktari mmoja tukimwita Bi. Arafa Mussa, Mhe. Jussa anamjua, mpelekee salamu zake. Alituweka kikundi akatufundisha jinsi ya ukunga, ndio iliyonisaidia tarehe 20. Mama yule nikamtia ndani, wakati aita gari haijawahi kuja mtoto huyo hapo, nikampokea mtoto nikamuweka. Nikaanza kumuhoji umeanza kuumwa wakati gani, ulikuwa hapo unategemea nini. Kwa kweli ni masikitiko makubwa mpaka ikabidi mama yule kujifungulia ndani kwangu, nikapokea mtoto nikamaliza nadhani nilifika hapa kazini kama saa 4:30 hivi nilichelewa. Mhe. Naibu Spika, hali ni ngumu. Kwa hivyo, naomba bado japo Baraza hili halikuzua mjadala kuhusu suala hili. Lakini hii hali ifikiriwe.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye ukurasa wa 66, kuna hii bodi ya ushauri wa hospitali binafsi. Kinasema kwamba kimejipangia kutekeleza malengo ya kuwa na programu za kuwaendeleza kiutaalamu wafanyakazi wao. Katika hizi hospitali binafsi Mhe. Waziri hili ni jambo zuri. Kuna wafanyakazi wauza madawa katika hospitali binafsi kwa kweli hawana ujuzi wowote. Kwa hivyo hili ni suala la kufikiriwa na kutizamwa vizuri sana. Mhe. Naibu Spika, unakwenda pale unapewa madawa ambayo, mimi naweza kusema ni ya kukuuwa rohoni. Kwa hivyo, hili ni suala moja la kushughulikiwa.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine nimeona katika hiki kitabu kuna suala la tiba asilia. Tiba asilia nakumbuka tulipitisha mswada wake katika Baraza la Saba. Kuna suala zima la kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa tiba asilia na tiba mbadala. Kwa kweli tiba asilia hivi sasa watu wengi wanakimbilia huko. Katika haya maradhi ambayo tunayaona ni sugu. Kuna bwana mmoja siku moja nilimkuta ana kidonda kibaya sana na watoto wake walimtoa hospitali ya Mnazi Mmoja wakati keshatiwa saini akatwe mguu ule ana sukari. Watoto wake wakamkimbiza, wakasema sisi hatutaki akatwe mguu.

Mimi niliona imani sana nikaona kwa nini mmemtoa hospitali, sasa akishindikana huko. Wakasema basi lakini hatuwezi sisi mzee wetu kuzikwa kiungo kimoja kimoja, akikatwa mguu harudi huyu, leo kazikwa mguu kesho atazikwa mwili mzima. Kwa bahati nimekaa nikamfuatilia nikamuuliza, vipi hali ya mzee, akaniambia twende ukamuone mzee wetu hajambo. Amepata dawa gani, akasema tumempeleka kwenye tiba asilia. Kidonda kile kimepoa na mwenyewe nikamdadisi akasema kweli sukari iko vizuri kabisa.

Kwa hivyo, mimi naunga mkono suala hili la tiba asilia, lakini sasa tunarudi pale pale katika hali yote na kutoa taaluma, lakini hiyo tiba asilia ukenda uuze ng'ombe mzima. Ukimuuliza je hiyo tiba yote umetoa kiasi gani, anakuambia mimi nimetibiwa haya maradhi yote kwa Shs.250,000/=. Ukiwa nayo ndio unapata matibabu, ukiwa huna unarudi nyuma kwenda kukaa pale pale unakufa. Kwa kweli tuko kwenye mitihani binadamu. Tuko kwenye mitihani mikubwa na hali ya kuwa maradhi yametukabili. Kwa hivyo hili ni suala kadiri itakavyotolewa hiyo taaluma na kuwashajihisha waganga katika kufungua hivyo vituo vya afya basi na hili pia watoe taaluma ili kidogo kuwe na uhafifu wa hizi tiba zenyewe.

Mhe. Naibu Spika, jengine nije katika hospitali ya Mnazi Mmoja kuhusu madaktari wa zamu. Suala la madaktari wa zamu pamoja na mafundi kuwepo pale ni suala muhimu sana Mhe. Waziri. Siku moja mama mmoja mtoto wake aliingiwa na mende wa sikio saa 5:00 za usiku, nikatakiwa nimpeleke hospitali, kufika hospitali nikaambiwa daktari wa zamu leo hayupo. Haya nitampata wapi, yuko Bububu ukamchukue. Haya gari, nikaambiwa gari haina mafuta. Kwa bahati nikawaambia mimi gari yangu ninayo, huyo wa kunipeleka huko Bububu nitampata, nikaambiwa utampata. Tukatoka mpaka Bububu Mhe. Waziri, nafika Bububu namgongea mlango mwanamama yule. Vile alivyotoka tu nilipouona ule uso, nikasema hapa hapana mambo, mimi mwenyewe namuonea huruma. Akaniambia mimi siwezi kwenda ninaumwa, nikamtizama anaumwa kweli tumbo la miezi tisa la kujifungua. Akaniambia mimi naumwa, sasa.

Akaniambia nendeni Magomeni yupo *doctor*, tukaja zetu mpaka Magomeni tunafika Magomeni tukagonga mlango mtu kumtoa saa tano au sita ndani keshalala na kumpumzika ni mtihani, yuko huko huko ndani anarusha maneno nje. Mimi sio zamu yangu nendeni Bububu kwa bibi fulani tukamwambia tumesharudi hawezi ana matatizo na kweli anaumwa katwambia kwa upole na hali ya kinyonge, kwa hivyo ametuelekeza tuje hapa anasema mimi sitoki wakati leo sio zamu yangu. Mhe. Waziri mwanamke pekee ni mwenye huruma mama wa *doctor* yule aliinuka juu ya kitanda akamkabili mumewe akamwambia nenda hospitali kamhudumikie mtoto, uchungu wa uzazi aujuaye ni mama peke yake unajua wanawake tuna maneno ya kumlainisha mtu mpaka akaridhika. *(Makofi).*

Mhe. Waziri siku moja imamu aliambiwa hutuba naambiwa namtungia mke wangu kweli mimi hutuba yangu ananitungia mke wangu, akaambiwa anakutungia vipi kweli mwanamke ndio anayetunga hutuba na mwanamke ndio anayemfanya mwanamme aweze kufanya kazi vizuri, baada ya nasaha za mama ndani akatoka *doctor* yule tukenda zetu hospitali, kufika hospitali akamtoa mende suala la dakika mbili tatu lilichukua mpaka saa nane za usiku ndio tunarudi nyumbani. Kwa hivyo ipo haja madaktari wa zamu kulala hospitali ikiwa mama ambae ana zamu siku ile ana matatizo pajulikane mapema daktari gani atashika nafasi ile kwa siku ile, kazi yetu tunafanyiwa madaktari wengine wanasema ehee kuna tatizo jengine limetokea la kiufundi na mafundi hawapo haya kuna kitu gani kilichojitokeza chengine usiku huo. Tunaambiwa lifti imeganda na wahusika hawapo kwa hivyo ipo haja na mafundi kulala pale, mafundi wa aina zote walale matatizo hutokea wakati wowote.

Mhe. Spika, mimi nadhani kutokana na mambo mengi yameshachangiwa na mimi nisirefushe muda wako nimalizie hapo kwa kumuombe kheria Mhe. Juma Duni Haji, kutokana na mzigo mzito aliopewa wa jamii wa afya za binaadam naomba serikali imuunge mkono Mhe. Waziri kwa hali zote, imsaidie Mhe. Waziri

yuko makini sana yule. Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi hii ya sasa hivi kuweza kuchangia, nami nianze basi kumpongeza babu yangu JD pamoja na Naibu Waziri wake Doctor Sira Ubwa Mamboya, vile vile nitakuwa mwingi wa fadhili kama sikuwapongeza wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya kwa njia moja au nyengine walioweza kumsaidia kutengeneza bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwanye Ukurasa wa 14 kutokana na ahadi za Mhe. Rais katika kampeni zake na chama chake kitukufu cha CCM, vile vile katika matembezi yake ya ziara ya hivi karibuni ambayo ametembelea katika majimbo yetu alitoa ahadi ya kuweza kutumalizia hospitali zetu na kuziweka katika kuzipandisha daraja, hospitali hizo zikiwa za Kwamtipura pamoja na Mpendae.

Mhe. Naibu Spika, dhamira sio mbaya ni nzuri zaidi na mimi nimeifurahia zaidi kwa sababu tunaondosha msongamano mkubwa katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja, lakini nitamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa mbele anieleze lini hospitali hii ya Jimbo la Mpendai itamalizika kujengwa. Kama hukunipa majibu tosha yatakayoweza kuwaridhisha wananchi wa Jimbo la Mpendae mimi nitakuwa mgumu kidogo kupitisha bajeti yako.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye hospitali yetu kuu ya Mnazi Mmoja mimi naipongeza sana kwa sasa hivi na hivi tunavyokwenda, kwanza napongeza maabara kuu ina vifaa vya kisasa na Mhe. Waziri ametwambia tunafanya uchunguzi wa test nyingi sana tunakupongeza sana, vile vile tuje kwenye sehemu kubwa wanakotiwa watu mapio pio ile sehemu kitanda chake ukweli akidondoka mtu au ukijikwaa sasa hivi unaweza kupata tetnas pale pale, chumba kile kibaya kinahitaji marekebisho ya hali ya juu. Tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuambie ni lini kile kitanda tulichorithi tokea ukoloni angalau atakibadilisha pale.

Sasa nije kwenye *emergence room* sasa hivi imekuwa ni *empty room, imergence* kupitia *out patient* ni kitu kimoja kizuri na chenye faida kubwa kwa wananchi wetu lakini sasa chumba kile hakina kifaa hata kimoja, ajali zimeongezeka kipindi hiki gari zimekuwa nyingi, vespa zimekuwa nyingi tunataka atwambie atakiboresha vipi na ile sehemu yote ya mapokezi.

Sasa hivi nije kwenye *maternity ward* iko haja kubwa ya kuweza kuipanua tunashukuru serikali ya awamu ya sita imefanya *expansion* na imekuwa nzuri tu lakini bado kutokana na ongezeko la wananchi wetu hivi sasa haikidhi haja, tunamuomba waziri afanye hatua za dharura ili kujenga jengo japo la kujitegemea lenye kukidhi haja na kuweza kuchukua *clinic* za mama waja wazito ikiwemo na sehemu ya *ultrasound* itawasaidia sana wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika,nije kwenye hospitali ya Mental sasa hivi inapakwa rangi ni nzuri kweli kweli *new impending* wanaita lakini jengo lile halikidhi haja, wale ni binaadamu tuliowaweka pale serikali pale au Wizara imeweka utaratibu wa maji ni mzuri na tunaipongeza sana, lakini na wananchi wetu wa mitaa ile iliyo karibu wanapita mle ndani wanabomoa zile paipu wanachukua na wanaiba mpaka unafika wakati maji yanakosekana na yanamwagika ovyo, tunamuomba Mhe. Waziri ule ukuta ambao umetobolewa kama matundu ya pazia basi ufanyiwe haraka ili ujengwe, ili wale wagonjwa waliopo pale waweze kustirika. Wagonjwa wale wa akili ni sawa sawa na watu wengine tunatakiwa tuwaenzi vile vile, kwenye uzio ule mna mwitu mwingi kweli na ile sehemu ni kubwa.

Naishauri Wizara ya Afya ijenge viwanja vya michezo ili kuwapa faraja wale wagonjwa wetu au basi kama haiwezekani kujenga viwanja vya michezo tumuombe Ndugu yetu Waziri wa Kilimo atupe ile mbegu yake ya Merika ili tuweze kuitia pale, pana walinzi pale lakini wamekuwa ni kama maboya tu hawana vifaa vyovyote wamekaa tu hata wanatishiwa maisha yao na wale watu wanaopenya mle wanaotaka kuiba, hawana tochi wale hata siku za mvua wanashindwa kuwa na renkoti kuja kazini kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye kituo kidogo sana cha afya kilichopo Air Port, kituo kile ni muhimu sana lakini hakina ofisi unaweza kushangaa unaweza kumuona kama mtu katiwa kwenye karanginda la jela lile ananing'inia mmoja tu hata nafasi ya kugeuka hana, hakuna hata *ambulance* pale kukitokea *emergence* tunamuomba waziri akiboreshe kitengo kile ili kijulikane kama ni kitengo cha afya kiwe na ufanisi bora.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye utafiti, Mhe. Waziri amesema kuna nafasi ya utafiti inafanyika sasa hivi lakini mimi ningelimuomba achukue hatua madhubuti za kufanya utafiti kwenye maradhi ya sukari, zamani tulikuwa tunasema maradhi ya sukari ni ya kurithi lakini sasa mfumko wa maradhi haya ni mengi na yanapotokea hatujui wapi, tuchukue hatua za dharura tufanye utafiti tuweze kujua kitu gani kinachowadhuru hawa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye maslahi ya wataalam wa afya mimi siiti madaktari tu kwa sababu kila nyanja ya afya ina umuhimu wake, ukija maabara ina umuhimu wake, *pharmacy* ina umuhimu wake, mataktari wana umuhimu wake. Hawa watu tuwaenzi sana na bila ya kuwaenzi au kuwapa huduma bora basi wote wataweza kukimbia na kubakishwa na jumba letu tupu la Mnazi Mmoja, vile vile naiomba Wizara ichukue mikakati bora zaidi ya kila mwaka kupeleka *specialist* mmoja angalau aka-*specialize* kitu kimoja kila mwaka, tukiwa na *vision* kama hiyo basi baada ya miaka kumi tutaona tunao *specialist* wengi kuliko kutegemea wale kumi saba waliosemwa hii itatusaidia sana.

Mhe. Spika, sehemu ya mwisho kabisa mimi nije kwenye *I.C.U* juzi katika suala langu nilipokuwa nikimuuliza Mhe. Naibu Waziri alisema bado wanaendelea kuzungumza na wafadhili kujenga hii *I.C.U* mimi nasema kuendelea kuwasubiri wafadhili kujenga *I.C.U* ni kuweka rehani afya za wananchi wetu. Mwenzangu Mhe. Hamza Hassan Juma yeye alisema ataomba tamko la serikali, mimi naomba niondoe shilingi yangu kwa niaba ya wananchi wa Mpenda. Nafiri ni

kielelezo tosha nafikiri ukiangalia sasa hivi wananchi wanakimbilia Dar es Salaam kupata huduma hii mtu mgonjwa wake akiwa anaumwa sana basi Dar es Salaam, na kila boti zikija asubuhi maiti, jioni maiti wananchi tayari wamekosa imani na hospitali yetu sasa hivi turudishe imani, mimi nadhani iko haja ya kutoa kifungu kwa Wizara ya Fedha tukawapa Wizara ya Afya tukaweza kujenga *I.C.U* yetu ambayo itakuwa imara na hii itawasaidia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nataka kuendelea sana lakini hili suala la *I.C.U* limeniweka pabaya siwezi hata kusema naogopa nisije nikaanza kulia hapa mbele ya Baraza lako tukufu. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja mimi na wananchi wangu wa jimbo la Mpendae. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia jioni hii ya leo kuweza kukutana hapa tukiwa katika hali ya uzima, lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii na mimi nikaweza kutoa mchango wangu mdogo katika wizara hii. Lakini tatu nimshukuru sana na nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Afaya na Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wake wote wa Wizara ya Afya kwa kweli wanastahili sifa na pongezi kubwa.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii mimi napenda niite wizara mama kwa kweli wizara hii ni mama ni wizara ambayo mahitaji yetu yote muhimu yapo katika wizara hii, maana umuhimu wa mtu ni afya kama huna afya hata uwe na pesa vipi huwazi kuzitumia. Mhe. Naibu Spika, kwa nini nimeiita wizara mama miongoni mwetu hapa tulipo sote tutakubali kama mama ndio aliyetuleta hapa ulimwenguni na ndio maana niseme miongoni mwetu hakuna hata mmoja kuweza kuikwepa wizara hii, ni lazima kila mmoja anahitaji huduma katika wizara hii ndio maana napenda kuita jina hilo la wizara mama.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wizara hii na fungu lililotengwa kwa ajili ya kuendesha huduma za wizara hii halitoshi wala halikidhi

haja, nayasema hayo kwa sababu tulipoanza bajeti hapa ile bajeti kubwa ilitueleza kwamba wizara hii imepewa kipaumbele, kama imepewa kipaumbele basi mimi ningeliomba Mhe. Waziri wa Fedha akaliona hili na nalisema kutokana na juzi tulipokuwa kwenye semina na Mhe. Rais wetu, Mhe. Rais ana usemi ambao anausema mara kwa mara na usemi huu unatokana na wasanii wetu, usemi huu hata juzi aliutumia Mhe. Naibu Spika, naomba ninukuu.

Mhe. Rais alisema " *ada ya mja kunena uungwana ni vitendo".* Basi tenda watu wataona yale majisifu tuweke kando na sisi tulisema vizuri tu katika ile bajeti kuu kwa kusema tumeipa kipaumbele wizara ya Afya basi mimi naomba haya yasiwe maneno tu, maneno yawe mafupi na vitendo viwe virefu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze mchango wangu katika ukurasa wa 28 ambapo pale kumeelezewa *program* ya kupambana na maradhi ya watoto, ni kweli tukiweza kufanikiwa hapa tunaweza kuzijenga afya za watoto wetu vizuri na baadae ikawa ndio wazee tunaowategemea katika kuja kushika nyadhifa mbali mbali katika serikali hii. Mimi mchango wangu hapa nilitaka nitoe ushauri tu kwa watoto tunawapowapeleka mahospitalini kutibiwa basi zamani tulikuwa na mpango mzuri tu ambao mtoto akiumwa tu ukimpeleka hospitali basi unatakiwa uende na vyoo vyake ili uchunguzi uanze pale tofauti na hivi sasa unaweza kumpeleka mtoto hospitali ukifika ukaambiwa ana nini anakohowa, anatapika, ana nini matokeo yake homa ikakusumbua kwa muda mrefu pengine ni minyoo tu inawezekana tukianza pale kwa uchunguzi tukaweza kuyajua maradhi ya mtoto na tukaanza tiba sahihi.

Kwa hivyo mimi nilisisitize hili tuanze na utaratibu wa kutumia vipimo watoto homa za minyoo zinawasumbua sana, utakuta mtoto anakohoa wewe unamtibu kifua kumbe ni minyoo, mtoto tumbo linamuumba unampa dawa ya tumbo kumbe minyoo, sasa tukianza na uchunguzi naona tunaweza kufikia pahala pazuri.

Mhe. Naibu Spika, nije katika huduma za wazazi katika kitabu chaka hapa Mhe. Waziri ametueleza kwamba anaandaa utafiti katika suala zima la wazazi kumeonekana kuna wimbi kubwa pale la kufanyiwa upereshen kinamama, mimi nashukuru kama utaanza utafiti huu pale kwa sababu hata na sisi tunashtuka. Watu wengi mitaani tunapata mshtuko huo kuona wazazi wengi sasa wanafanyiwa upereshen tunaogopa isije ikawa ni mradi, hili tuliangalie kuna watu pengine wanaweza kuwa uwezo wa kuzaa wenyewe wanao na ikawa sisi tunawalamisha tu kuwafanyia upereshen, fanya uchunguzi Mhe. Waziri ili tuweze kuligundua hili tuweze kunusuru wazazi hata kuogopa kule kwenda hospitali kujifungua kwa kuogopa kisu.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu uelekee tena kwa wakunga hasa wale wakunga wetu wa vijijini mna majina wenyewe ya kitaalam mnawaita lakini mimi silielewi, wakunga hawa Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niwapongeze sana sana wama msaada sana kwetu, nimuombe Mhe. Waziri kuangalia sana wakunga hawa wanatoa msaada sana kuwasaidia wakunga wako wale katika mahospitali yako. Usiku mara nyingi tunakwenda kuwagongea hawa na wanatufuata wakati hawana malipo yoyote wanatumia uzalendo wao na ubinaadamu wao, hawa mimi nilikuwa naomba uwasaidie angalau kwa kuwapa vitambulisho ili wanapotoka na mgonjwa kule wakishaona mgonjwa huyu hana uwezo wa kujifungua hapa basi wanapokuja hospitali basi watu hawa watambulikane, lakini anakuja na mgonjwa wake akifika nje yeye kama ni mtu ambae hana thamani, hebu tuwape vitambulisho ili na wao wakifika pale waweze kuwaingiza wagonjwa katika mazingira yale aliyokuwa nayo yeye antambulikana na kuthaminiwa.

Mhe. Naibu Spika, pia ni vizuri kuwaongezea taaluma hawa kwa sababu Mhe. Mtumwa Kheri Mbarouk ameeleza hapa kwamba saa nyengine unaweza kuipata kesi usiyoitegemea, kakujia mtu kwako mara moja basi ikawa tayari wewe mkunga ghafla, sasa elimu hii si vibaya nimuombe Mhe. Naibu Waziri kwa vile yeye ni mwanamke mwenzetu akaweza kutupatia angalau kwa uchache na sisi wanawake tulio katika Baraza hili angalau ile elimu ya ukunga. Kwa

sababu aliyoyasema Mhe. Mtumwa nataka niungane nae na mimi nimeshawapokea watoto wawili hali sina ujuzi imetokea hivyo hivyo bahati mbaya nafika pale naanza kumshukuru mungu anisaidie tayari nimepokea na mimi sina ujuzi huo, basi angalau tukuomba Mhe. Naibu Waziri tupatie elimu kwa sababu kuna vitu wakati mwengine vinatokea bila ya kutarajiwa.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu pia niupeleke wizarani pale wakati ambapo mnapata kuandaa mafunzo ya semina kwa kuwaandalia wafanyakazi wetu basi ni vizuri hapa napo tukapaangalia, kwa sababu sasa nyengine pale kunakuwa na udugu inawezekana semina anakwenda huyu kwa huyu inakosekana wale wafanyakazi wengine na wao wakaweza kupata mafunzo yale kama ilivyotarajiwa. Lazima tuwe na mtiririko mzuri wa kuangalia mara hii wamekwenda hawa mara nyengine tubadilishe waende wengine ili elimu ile iweze kusambaa kwa wafanyakazi wote.

Mhe. Naibu Spika, hapa wenzangu wametangulia kusema mengi kwa kuwa na mimi niliona Wizara hii ni wizara nzuri ambayo inatugusa sana hasa sisi kinamama ambapo sasa zote tupo pale wodi ya wazazi, basi pia ningependa kutoa mchango wangu ule mrundikano wa watu ambao wanakuja pale ka ajili ya wagonjwa wao au wazazi wao.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. waziri hili kulifanyia kazi ili wakaweza kupata sehemu wakaitenga kwa ajili ya wale watu wanaokuja kukaa pale kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa wao, kwa sababu mazingira yangezidi kuonekana mazuri lakini inaonekana msongamano kati ya madaktari wagonjwa na wahudumu wa wagonjwa. Kwa hivyo tungepata sehemu mfano mzuri kule hospitali ya Muhimbili pale ukiingia tu pana sehemu nzuri tu ya kukaa kwa hivyo ukifika pale hutaabiki, unakaa unasubiri muda mpaka unafika unapata kuingia kwa mgonjwa wako.

Lakini pia niseme kinachotufanya saa zote tusokotane pale hospitali basi ni kuwapa huduma wagonjwa wetu muwape huduma nzuri saa

nyengine sisi itaweza kutusitisha kusongamana pale, lakini tunachokimbilia pale saa nyengine mgonjwa wangu hajanawishwa hata uso mbio tunatoka tunakimbilia pale, pale huduma ikitolewa vizuri basi hata huo msongamano wa watu wenyewe utapungua. Kwa sababu ukienda ukimkuta mgonjwa wako yupo katika hali nzuri wewe mwenyewe utaridhika na hutopenda kwenda na utakwenda kwa kumjulia hali tu hutokuwa na muda wa kukaa sana pale, labda awe mgonjwa mahututi.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu wameeleza sana kuhusu *I.C.U* hiki kitengo ni muhimu sana hivi karibuni tu mimi nilikuwa na mgonjwa pale, ukweli tukiangalie kwa mtazamo mzuri ili tuweze kuipata ile huduma muhimu ambayo inatakiwa pale mtu aipate, mimi masikitiko yangu yanakuja hata zile fedha ndogo tu mnazokusanya kwamba pia ziende katika mfuko mkuu wa Hazina hili mimi linanisikitisha kwa sababu yapo mambo madogo madogo ambayo nyinyi mnatakiwa kila mara kuangalia na kuyafanyia kazi.

Mfano basi hata mafeni mawili matatu hata yakiharibika haiwezekani kununua nyinyi wenyewe mpaka mkapate pesa huko hili lingeangaliwa na kungekuwa na utaratibu mzuri mukatakiwa kupeleka tathmini yenu kwa matumizi madogo madogo ili fedha zile mukaweza kurekebisha kama vyandarua vibovu basi pia tusubiri. Mambo kama haya tuachiliwe ili tuweze kukidhi haya mambo madogo madogo ambayo yangeweza kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitokuwa na mengi kwa leo lakini na mimi naomba niungane na wenzangu, kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia juu ya mia ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti na mimi nimshukuru allah kwa jioni hii ya leo kuweza kunipatia japo dakika nne au tano na mimi nikatoa mchango wangu, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu na pia niipongeze Wizara ya Afya kwa hotuba yao nzuri iliyojaa mantiki za aina zote.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza ukurasa wa 23 na 24 pale kifungu cha tano nane. Niishukuru wizara kwa kuja kuchunguza damu za wana vijiji wa Tumbe na Shumbaviamboni kwa tatizo zima la homa ya malaria, homa ambayo taarifa zilizopo ni kwamba homa hii imeshamalizika lakini ripoti ya Mhe. Waziri imeeleza hapa kwamba katika vijiji hivi bado homa hii ipo.

Pia nashukuru kwamba ni mepata nafasi ya kuuliza kwa masheha wetu tulionao kwamba tatizo bado linaendelea la homa hii ya malaria kwenye wodi ya Shumbaviamboni, kijiji cha Mgeni Nje, hichi kimechukua tatizo kubwa la homa hii ya malaria. Naishauri sana Wizara ya Afya wakazidi kupeleka wataalamu katika kijiji hicho ili kuliondosha tatizo hilo la homa ya malaria.

Mhe. Naibu Spika, pia nitoe shukurani kwa Wizara ya Afya katika mgao wa madaktari hawa waliotolewa hivi karibuni katika jimbo langu angalau na mimi nikapata wawili kwa kusaidia tatizo zima la madaktari katika Zanzibar yetu. Sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kabisa.

Mhe. Naibu Spika, hili tatizo ni kubwa tena sugu, kwani katika kituo kizima cha Shumbaviamboni tuna daktari mmoja tu pale. Daktari huyo haumwi wala haumwiwi, suku zote yeye yupo kazini. Huyu ni binaadamu sio robot, ni vyema wizara wakaangalia vyema katika kituo hiki angalau akapata msaidizi, siku ambayo akipata matatizo huyu basi ikawa kuna mwengine anaesaidia katika eneo lil.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika ukurasa wa 25 kifungu cha 5 (9) kuna tatizo zima la kichocho na minyoo na mabusha. Mimi ni miongoni mwa jimbo lililoathirika na matatizo hayo. Jimbo langu limezingirwa sana na mito na maziwa, kwa hivyo wananchi wangu wengi wanatumia maeneo hayo.
Mara nyingi ilikuwa Wizara ya Afya inafuatilia sana mashule na vijijini hutoa taaluma ili kuwataka vijana wetu wasiwa na mazoezi ya kukoga sana mtoni. Lakini kwa muda mrefu Wizara ya Afya imeacha suala hili, kwa hivyo matatizo haya na magonjwa haya

yanazidi kuwaelemea hasa vijana wetu wadogo wadogo ambao bado hawajawa na uzoefu wa kuweza kukoga vizuri kwa kuweza kutumia maji yale wakawa wao wanajizamisha mule na kufanya mambo mengine. Naishauri sana wizara ya Afya baada ya kuendelea kutoa ataaluma ili kuwafanya vijana wetu waweze kutumia maji ambayo yanajenga afya zao.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mdogo sana na Mhe. Saleh hapa anataka kuchangia na hoja yake nzito kiasi fulani nimalizie kwa kusema kwamba katika jimbo langu la Tumbe bado lipo nyuma sana kwa vituo vya afya. Ukichukua kama pale mjini Tumbe, mji ambao ni mkubwa kulikoni vijiji vyengine vyote, kituo chao cha Afya pale kimejengwa tokea mwaka 1989, ni kibanda tu sio kituo chenye thamani ya leo. Ni jengo dogo kabisa lina vyumba vitatu vilivyopo. Chumba cha daktari ni hicho hicho na cha kumuwekea mgonjwa ni hicho hicho, kitanda chao tokea mwaka 1989. Mhe. Naibu Spika, ukiliona hilo godoro la kitanda hicho basi utakimbia. Halifai bwana.

Kwa hivyo, ningeliiyomba sana Wizara ya Afya juu ya matatizo yote yaliyopo, juu ya mpango huo waliotoa pesa ndogo ya kuweza kuendesha wizara hii kwa muda mwaka mmoja, lakini na jimbo langu la Tumbe basi kituo kile kifanyiwe marekebisho angalau tupate kituo cha kileo.

Mhe. Naibu Spika, pia ugawaji wa dawa katika eneo lile. Watu wanaokwenda pale ni wengi lakini dawa zinazofikishwa pale ni kidogo, wiki tu dawa za mwezi zimemaliza. Nilioiyomba sana Wizara ya Afya kuangalia kwa jicho la huruma eneo lile ambalo lina watu wengi, pale kwa mwezi tu wanatibiwa watu 10,000 na ziada, kwa hivyo ni watu wengi sana.

Ningelimshauri sana Waziri kuliona tatizo hili la watu wetu wa Tumbe.
Mhe. Naibu Spika, na mimi naunga mkono hoja hii mia fil mia, lakini na pale ambapo walipochangia wenzetu ni lazima Wizara hii

iongezewe posho lao ili waweze kuendesha maisha yetu. Kwa sababu sisi wadogo wote tunatibiwa hapa, pengine wakubwa wanatibiwa kwa mbele, lakini na sisi wadogo angalau tukenda Mnazi Mmoja tuweze kupata tiba ambayo inalingana. Mhe. Naibu Spika, nachangia hoja.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na hatimaye kutupa nguvu na uwezo wa kuhudhuria humu na kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mchache wa shukurani kama sikumpongeza Mhe. Waziri na wataalamu wake kwa kuweza kututayarisha kitu kama hichi ambacho waziri katumia kama masaa 2:15 kutusomea hapa bila ya kumeza mate wala kutetereka. Kwa hilo nampongeza sana Mhe. Naibu Spika.
Nimalizie kumpongeza ndugu yangu Dokta Sira Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kwa umakini wake na umahiri wake katika kufanya kazi yake hii, hasa anapotujibu maswali yetu.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye hoja. Niende moja kwa moja kwenye Ukimwi. Idara hii ya kudhibiti maambukizo mapya ya ukimwi. Mhe. Naibu Spika, mpaka sasa hivi tunavyozungumza ukimwi bado ni tatizo sugu katika nchi yetu. Linaendelea kutupotezea rasilimali watu, ambao ndio msingi mkubwa wa maendeleo ya nchi yetu, tena ndio msingi mkubwa wa maendeleo ya nchi yetu, tena katika umri huu wa watu wanaoweza kufanya kazi. Maana ingelikuwa ukimwi unachukua huu umri wetu siye miaka 60 na kuendelea mbele huko, lakini unachukua hawa wenye nguvu zaidi. Na kwa kweli Wizara ya Afya ipo kazi kubwa mbele yao.

Napenda niipongeze idara hii ya kudhibiti maambukizo mapya ya Ukimwi kwa kuweza kutoa taaluma kubwa katika vijiji vyetu, hata kule Vitongoji Kibokoni wanafika kule, Furaha, Uwandani, wanafika kutoa elimu. Tunashukuru sana, imesaidia taaluma yao.

Kwa sababu Mhe. Spika, hivi sasa huwezi kuozeshwa katika jimbo langu la Wawi ukiwa hujapima Ukimwi, hupati mke hata siku moja. Nashukuru sana Wizara ya Afya kwa kupitia kitengo chake Idara ya kudhibiti maambukizi mapya ya ukimwi kwa kuweza kutuletea hii taaluma kwa kweli imetusaidia sana. Mheshimiwa kwa hili nawapongeza.

Mhe. Naibu Spika, ningeiomba Idara hii ya Kudhibiti maambukizi mapya kuna maeneo hatarishi hawajayaona bado. Kwa mfano katiak maeneo ya wavuvi katika jimbo la rafiki yangu Mhe. Hassan katika Wilaya ya Micheweni, Tumbe, Vitongoji wavuvi tunakwenda kwenye dago *(fishing camp)*unakaa kule kiasi cha miezi mitatu au minne hujarudi nyumbani wewe unagaragara tu huko. Sasa ukirudi kule nyumbani ndio hapo unamkutia mwanamke ametayarisha viluwa, asumini. Mimi nataka Dokta Sira awasaidie wanawake wenzake wa Kojani, wa Tumbe, wa Micheweni, waume zao wakirudi dago kwanza wapimwe. Utawasaidia sana.
Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika hizi hospitali za *cottage hospitals.* Kwanza niende katika *cottege hospital* ya Makunduchi, naisifu sana hospitali ile. Kwa kweli naipongeza Wizara ya Afya nawapongeza wafadhili wetu pale kwa kuweza kutoa huduma nzuri sana kule hospitali ya *cottege* ya Makunduchi. Lakini kuna mapungufu machache ambayo wizara inaonekana imeyafungia macho. Mambo madogo madogo tu lakini wizara imeshindwa kuwa makini pale.

Pale kuna Utrasaund mashine mpya tena ya kisasa thamani yake ni zaidi ya milioni 30, ipo pale. Ile inahitaji kuwepo katika mazingira mazuri, chumba chenye AC , lakini imewekwa pale Makunduchi katika chumba dirisha lake linawekewa kanga hii ya kuvaa, chombo cha mamilioni. Ni aibu. Kama ni wafadhili walioleta msaada ule wakija pale watatufadhili tena. Kama ni fedha za walipa kodi iliyonunua mashine ile si kudharau jasho la wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani chombo cha milioni 40 kukitelekeza katika kakibanda kale ni kudhalilisha nguvu zetu, kwa

sababu zile tumepata kupitia kodi zetu. Kwa hivyo namuomba Waziri wa Afya aende akaiangalie, mashine ile milioni arubaini, tunashindwa kuijengea chumba cha milioni 10 tu tukaiweka. Ni fedheha.

Halafu ile hospitali ya Makunduchi ni lazima tukubali *automatically* ile hospitali sasa ni ya Mkoa. Ukiende *labor* ni kipande hakizidi pima moja, air taited, wafanyakazi hawana hata pa kukaa. Sasa tunaomba kwamba pale Makunduchi iwepo *labor* ya kisasa kabisa. *Microscope* zilizopo ni za kizamani mno, tumekwenda pale sisi wanashindwa kufanya diogsis ya TB wanashindwa kuwaona wadudu, kwa sababu mashine zao ndogo.
Mimi nadhani jamani tuwasaidieni wenzetu wa Kusini, wapelekeeni mambo ya kisasa msikae tu. Mimi nadhani *Microscope* ile haina pesa nyingi. Kwa hivyo tunaomba sana mtuwekee sawa.

Mhe. Naibu Spika, nyumba za madaktari hakuna, pale kuna dentist mzuri na ana *dention* mzuri tu. Kwa kweli ana uwezo yule kijana, lakini kakodiwa kijumba huko Uswahilini mbali huko. Kajengwa ndani huko, huku nyumba hakuna. Yule ni daktari bingwa katika mambo ya meno, ilikuwa nyumba yake ifanyiwe ukarabati pale awekwe. Leo kenda kukodiwa kijumba huko Uswahilini, aibu sana na tunamvunja moyo. Keshekutwa tukimsikia kenda Hindumandali tutamlaumu huyu wakati sisi tumemdharau. Hii ni dharau waheshimiwa. Kwa hivyo tujitahidi sana katika kuwatunza na kuwaenzi hawa madaktari.

Hii *cottage* ya Makunduchi naipongeza sana. Lakini hizi *cottege* nyengine hizi, ikiwemo ya kwetu Vitongoji ni magofu matupu, manesi hakuna, hao madaktari ndio hali kadhalika, ukenda wewe unaambiwa kohowa, eti ndio kipimo, fungua macho, toa ulimi. Jamani hicho ndio kipimo? Mimi nadhani hatujawa *serious* na kama haya mambo hamuyawezi basi tuleteeni sisi back *benchers* huku muone. Tuboresheni bwana, lazima sekta ya afya iwe nzuri kwa sababu hospitali ni gereji huwezi kuwa na gari nzima kama huna gereji nzuri.

Nakwenda Mnazi Mmoja kwenye ICU. Mheshimiwa milioni 800 ndio zitengeneze ICU zimekosekana zaidi ya miaka 30 nyuma tumeshindwa SMZ kutengeneza ICU ya Mnazi Mmoja kwa tatizo la shilingi milioni 800. Fedha mimi naona aibu. Laiti ingelikuwa sisi *back benchers* huku ndio tuliokuwepo madarakani sasa hivi milioni 500 ambazo zinakusanywa pale kwa mwaka. Nakuhakikishia sisi kwa kupitia wananchi kila mfanyakazi wa kiwango cha chini yupo radhi akatwe shilingi 1000, wa viwango vya kati yupo radhi akatwe shilingi 2000. Mchango ule nakuhakikishia ndani ya miezi mitano hii ICU ingekuwa imemalizika. Leo eti tunaambiwa ICU imekwamba kwa sababu ya shilingi milioni 800. Inasikitisha mno.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani hawa tuwape muda watakapokuja katika Baraza lijalo ikiwa ICU haijaanzwa, basi kuna mawaziri waliokuwa hawana wizara watatu nafikiri. Basi itabidi babu Juma akae *bench*, Dokta Sira akae *bench* halafu katika hao waliokuwa hawana wizara tuwape hizo nafasi. Kwa sababu hakuna *priority* kabisa, milioni 800 mnakusanya milioni 500 kwa mwaka kwa nini musianzie hizo kwanza mkanunua kila kitu.

Mhe. Naibu Spika, nakuja katika X- rays katika kazi iliyongumu sana na yenye kuhatarisha maisha ya watu ni X-rays. Wale wanaofanya kazi wanaochezea mionzi pale, wale vijana wanafanya kazi ya kuhatarisha maisha yao, miyonzi itawadhuru. Hakuna *allowance* yoyote wanayoipata pale ya miyonzi. Pale ilikuwa muwape maziwa na muwape maposho mazito mazito ya X-rays. Leo unakwenda pale unachezea mionzi na miaka yote unapewa boflo na chai ya rangi, mimi nimekwenda nimeona boflo na chai ya rangi. Aibu.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa kumpa mtu anachezea miyonzi mkate na chai ya rangi, aibu. Mhe. Naibu Spika, tujaribiwe kiasi cha miezi mitatu muone pale. Wale watakunywa maziwa na watavaa suti wale wanaochezea mionzi.

Twende kwenye afya ya mama na mtoto. Mheshimiwa afya ya mama na mtoto kama kuna watu wanaotaka watunzwe ni hawa. Kwa

sababu huwezi kupata bidhaa nzuri kiwandani kama kiwanda chako hukitunzi. Hawa ndio wanaotufyatulia rasilimali watu akina mama ni lazima tuwaenzi na tuwatunze. Idara hii ya Mama na Mtoto inatakiwa ipewe umuhimu mno na humu wanamofanya kazi wanatakiwa washughulikiwe vizuri.

Waheshimiwa mimi ni mjumbe wa Kamati ya Wanawake. Tumekwenda Mhe. Naibu Spika, kwa mfano huku Mkoani kuna kituo cha kupima hiyo Afya ya mama na mtoto, joto tupu. Akina mama wanakwenda pale na vitumbo vyao wakifika *pressure* inawabana. Aibu.

Namalizia kwa kumwambia Mhe. Waziri lile jengo la gorofa ambalo lilikuwa likitumia kwa kupimia afya ya mama na mtoto lililokuwepo Mkoani mlifanyie ukarabati. Hamna uwezo wa kulifanyia ukarabati, wenzenu ikiwa hawana uwezo wanawapa matajiri wanajenga jengo, halafu wanafanya biashara chini, juu mnatumia nyinyi. Kuliacha vile lile jengo ni kudhalilisha nguvu zetu kwa sababu tumelijenga kwa kodi zetu lile jengo.
Mhe. Naibu Spika, kwa kutaka maelezo ya kina juu ya ICU lini itajengwa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana ndugu wajumbe kwa michango tokea asubuhi mpaka hivi jioni. Lakini bado wamebakia wachangiaji sita. Tukijaaliwa Ijumaa nataka bajeti imalize asubuhi, kwa hiyo nitafanya ushauri na Katibu ili tuweze kupunguza maswali tuanze watu 6 halatu tumkaribishe Naibu Waziri na Waziri amalizie.
Kabla sijaahirisha nina tangazo nimepewa na Katibu wa CCM kwamba wanawake wote wa CCM Wawakilishi tukimaliza kuahirisha kikao wabakie kuna masuala muhimu.

Baada ya hayo naakhirisha kikao hiki mpaka Ijumaa tarehe 8 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 08/07/2011 Saa 3:00 za asubuhi)